# Nipashe

Alhamisi Septemba 19, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580027

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Mashine ukaguzi KIA haifanyi kazi miaka 3

UKURASA 3


ama

ALHAMISI SEPTEMBA 19, 2019

AFYA NA MAZINGIRA

Mikwamo kijamii, mazingira duniani yaisukuma UNESCO kugusa kila eneo (Ukurasa 16)


Mamia wanyanyaswa kijinsia vyuo vikuu (Ukurasa 14)

Daktari anayeanza mafunzo kazini anasimulia 'kimbembe' darasa uzazi (Ukurasa 20)

Maajabu tiba ya Askofu Mkuu Ruaw'ichi kutoka KCMC - MOI (Ukurasa 14)

UKURASA 13

# Askari kupiga kura siku moja kabla uchaguzi



Mbowe, Zitto, CUF wapinga vikali wakitahadharisha kwamba... *Endelea ukurasa wa 2*



## 45 MBARONI KWA KUUZA PETROLI NYUMBANI

UKURASA 3

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma (SACP) Gilles Muroto (mwenye glovu), akionyesha waandishi wa habari jana, madumu na mapipa yenye zaidi ya lita 5,000 za mafuta ya petroli na dizeli, baada ya kukamatwa kwa njia ya wizi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mloganzila yarekebisha maumbo wagonjwa

UKURASA 2

**MICHEZO** SAMATTA AANDIKA REKODI KALI ULAYA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Askari kupiga kura siku 1 kabla uchaguzi

Na Mwandishi wetu

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imesema inatarajia katika Uchaguzi Mkuu ujao, watendaji wake na askari wa vikosi vya ulinzi na usalama wapige kura siku moja kabla ya uchaguzi wenyewe.

Imesema lengo ni kuyapa makundi hayo haki ya kupiga kura na kutekeleza majukumu yake ipasavyo siku inayofuata ya uchaguzi.

Hata hivyo, suala hilo limepingwa vikali na baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani, wakidai kuonyesha hofu ya utaratibu huo kutumika kuchakachua matokeo halali ya kura za wananchi.

Mkurugenzi wa (ZEC), Thabit Idarous, alisema kura hiyo itawahusisha vikosi vya ulinzi na usalama na watendaji wa tume hiyo ili watumishi hao watekeleze majukumu yao siku ya uchaguzi.

Aliyasema hayo wakati akifunguwa mafunzo ya siku tatu kwa waandishi wa habari kuhusu kuandika habari za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Idarous alisema hatua hiyo ya kura ya mapema imetokana na marekebisho ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar Na. 4 ya Mwaka 2018 ambayo inatoa nafasi kwa makundi hayo.

Alisema marekebisho hayo yamekuja baada ya kubainika askari makundi hayo hayaitumii haki ya kidemokrasia kupiga kura na kuwachaguwa viongozi kutokana na kutingwa na majukumu ya kazi katika siku hiyo.

"Marekebisho hayo sasa yatawapa nafasi baadhi ya watendaji waliokabidhiwa majukumu muhimu, kupiga kura siku moja kabla ya Uchaguzi Mkuu kufanyika," alisema.

Wakati ZEC ikieleza hayo, vyama vya upinzani vimepinga vikali utekelezaji wa sheria hiyo, vikionyesha wasiwasi wa kuwapo kwa udanganyifu kuhusu kura zitakazotokana na makundi hayo.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, viongozi wa vyama vya ACT-Wazalendo, CUF na Chadema walidai sheria hiyo ilipitishwa kwa nia ya kupendelea upande mmoja na kwamba vyama vya upinzani havikushirikishwa.

**MBOWE ANENA**

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alidai changamoto kubwa ni uhuru wa tume za uchaguzi za pande zote mbili.

Mbowe alidai tume hizo (ZEC na NEC) zinatumiwa vibaya kusaidia na kubeba upande mmoja pasipo kuzingatia sheria na kulinda maslahi ya wadau wote.

Alidai ndani ya tume hizo wameajiriwa makada wa chama cha siasa na wakati mwingine vyombo vya dola vinatumiwa kupiga kura kwa maslahi ya upande mmoja.

Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alidai jambo hilo limekuwa likifanyika hasa upande wa Zanzibar kwa askari kutoka Tanzania Bara kupelekwa visiwani huko kwenda kulinda amani lakini baadaye kutumika tofauti.

"Kwa utekelezaji wa sheria ya kupiga kura siku moja kabla, maana yake ni kuhalalisha wapige kura za ziada kwa ajili ya kupata ushindi kwa chama tawala," Mbowe alidai.

Kwa mujibu wa Mbunge huyo wa Hai, mambo hayo yanafanyika kwa mpango maalumu ili siku ya kupiga kura vyombo vya ulinzi na usalama viwe na kazi ya kuwadhibiti wapinzani washindwe kupata haki kisheria.

"Tunataka tume huru ya uchaguzi ili haya mambo yafikiwe kwa maridhiano, watu wanaingia kwenye uchaguzi mkiwa hakuna mwafaka wowote, si sawa," Mbowe alishauri.

INAENDELEA UK.8



Wataalamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Tawi la Mloganzila kwa kushirikiana na mtaalamu mbobezi wa upasuaji kutoka Korea Kusini, Prof. Jeong Kim, wakifanya upasuaji wa kurekebisha viungo na makovu katika kambi maalum iliyoanza juzi na kuhitimishwa leo. PICHA: MARY GEOFREY

# Mloganzila yarekebisha maumbo ya wagonjwa

Na Mary Geofrey

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) Tawi la Mloganzila, imefanya kambi maalum ya upasuaji wa kurekebisha viungo vilivyojikunja kutokana na makovu na ajali za moto kwa wagonjwa tisa kati ya 11 wenye matatizo hayo waliyojitokeza. Kaimu Mkuu wa Idara ya Upasuaji na Magonjwa ya Mfumo wa Mkojo, Dk. Erick Muhumba, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu kambi hiyo, alisema wamefanikisha upasuaji huo kwa kushirikiana na Daktari Bingwa wa Upasuaji Rekebishi (Plastic Surgery) kutoka Korea.

Alisema kambi hiyo ilifanyika kwa siku tatu kwa wagonjwa ambao walipata vidonda kutokana na kulala muda mrefu wakiwamo wagonjwa wa kisukari, waliopata ajali na kubaki na makovu makubwa na viungo kujikunja kutokana na ajali za moto.

"Tulianza jana(juzi) tumefanya upasuaji kwa wagonjwa watatu leo (jana) tunaendelea na wagonjwa wengine watatu hadi kesho (leo) tutakuwa tumemaliza kambi kwa kuwafanyia upasuaji wagonjwa tisa kati ya 11 waliojitokeza kutokana na muda," Dk. Muhumba alisema.

Alibainisha kuwa upasuaji wa aina hiyo unafanyika kwa takriban saa nane na wanahamisha ngozi na kupandikiza eneo lenye kovu, kufanya upasuaji na kuunga viungo vilivyoungana kutokana na ajali ya moto.

Alisema upasuaji huo pia umeshirikisha madaktari kutoka Hospitali za Mwananyamala, Ilala na Temeke na kwamba lengo pia ni kuwajengea uwezo madaktari wa ndani. Daktari Bingwa wa Upasuaji Rekebishi, Laurian Rwanyuma, alisema nchini kuna upungufu wa madaktari bingwa wa upasuaji huo, akibainisha kuwa kwa sasa hawazidi 10 na mara nyingi wamekuwa wakitegemea madaktari bingwa kutoka nje kuja kushirikiana na wa ndani kufanya upasuaji wa aina hiyo.

Alisema kwa miezi mitatu wanapokea wagonjwa 15 wanaohitaji kufanyiwa upasuaji na kurekebishwa. Alibainisha kuwa gharama za upasuaji kwa wagonjwa hao ni Dola za Marekani 120 ukilinganisha nchi nyingine ambazo zinafanya kwa Dola za Marekani 3,000. Daktari Bingwa wa Upasuaji Rekebishi kutoka Korea, Joeng Kim, alisema ni mara ya pili kwake kuja nchini baada ya mwaka jana kufanya kambi ya wiki moja ya kufanya upasuaji katika Hospitali ya Mloganzila.

Alisema wanakuja nchini kufanya upasuaji na kubadilishana uzoefu na madaktari bingwa wa Tanzania.

Aliahidi kuwa Korea itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kubadilishana uzoefu kufanya upasuaji wa aina hiyo ambao umegawanyika katika sehemu mbili za upasuaji wa kurekebisha maumbo kama makalio, matiti na sura na upasuji wa kutibu makovu na kuziba vidonda.

# Malinzi adai hakuwahi kuandika madai ya fedha

Na Hellen Mwango

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, amedai mahakamani hakuwahi kuandika madai ya fedha alizolikopesha shirikisho hilo, lakini alilipwa kwa kuwa ilikuwa ni taratibu na namna ya uendeshaji wao.

Malinzi alitoa madai hayo jana wakati akihojiwa na upande wa Jamhuri kuhusu ushahidi wake kwamba alilipwa fedha alizoikopesha TFF kihalali.

Kesi hiyo inaendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamaba na Rushwa (Takukuru) Leonard Swai, alimhoji mshtakiwa huyo kuhusu fedha alizolipwa kama aliandika malalamiko kabla ya kufanyika malipo hayo.

Mshtakiwa alidai kuwa TFF ilikuwa ina utaratibu huo wa kumlipa na ilifahamu kwamba ameikopesha fedha hizo.

Alidai kuwa mbali na kuikopesha TFF, aliwahi kufadhili mbio za marathoni kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati huo kiongozi wa michezo alikuwa marehemu Joel Bendera na baadaye alishika nafasi hiyo William Ngeleja.

"Bunge lilifadhili mbio za marathoni miaka saba kuanzia mwaka 1997 mpaka 2004," alidai Malinzi.

Hata hivyo, alidai kuwa Spika wa wakati huo pamoja na Mwenyekiti wa Bunge hawakumbuki ila anayemkumbuka ni kiongozi wa timu hiyo marehemu Bendera na Ngeleja.

Alidai kuwa nyaraka zote zinazohusu ufadhili wa michezo mbalimbali ikiwamo ngumi za kulipwa zitakuwapo ofisini kwake katika Kampuni ya Cargo Star's.

Hakimu Kasonde alisema kesi hiyo inaendelea leo kusikilizwa utetezi wa washtakiwa.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine ni aliyekuwa Katibu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF, Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya.

Katika kesi hiyo mashahidi 15 wa upande wa mashtaka walitoa ushahidi na tayari aliyekuwa Rais wa TFF, Malinzi ameanza kujitetea.

Katika kesi hiyo washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa USD 173,335.

## HABARI KITAIFA

# Kifaa cha ukaguzi KIA hakifanyi kazi miaka 3

**Na Mary Mosha,** MOSHI

IMEELEZWA kuwa kifaa maalum cha ukaguzi wa mizigo ya wageni katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) hakifanyi kazi kwa miaka mitatu sasa kutokana na kuharibika.

Hali hiyo inasababisha watalii na wageni kupoteza mizigo yao, huku baadhi ya watendaji wakidaiwa kutokuwa waaminifu wakati wa usomaji wa kamera inapopotea mizigo ya wageni hao.

Changamoto hiyo iliibuliwa jana katika kikao cha pamoja kati ya wadau wa utalii wanaotumia uwanja huo, uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, alisema serikali ililazimika kuitisha kikao hicho baada ya kuibuka malalamiko ya wadau wa utalii wakati wa mapokezi ya faru tisa, kati ya 10 wenye vinasaba vya faru wanaopatikana Tanzania, waliorejeshwa nchini Septemba 10, wakitoka Afrika Kusini.

"Siku ile tulipopokea wale faru, tulipokea malalamiko kutoka kwa wadau wa utalii ambao walikuwa wakilalamikia upotevu wa mizigo na Visa zao katika mfumo mpya wa njia ya mtandao (e-Visa).

"Walisema hiyo kwao ni changamoto kubwa ambayo inakwamisha biashara ya utalii nchini kwani utalii unahitaji ufanisi na uaminifu," Kanyasu alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (Tato), Emmanuel Mollel, alisema: "Asilimia 90 ya wageni wanaoingia nchini wakipitia KIA hueleza masikitiko yao ya kupotelewa na mizigo yao na kusimama muda mrefu wakisubiri kuhakikiwa Visa zao, wanatumia zaidi ya saa tatu."

Alisema kitendo hicho huwachukiza wageni kutokana na kuchoka na hivyo kulalamika na hawapendi jambo hilo kujitokeza kwa kuwa linaweza kuua soko la utalii nchini.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, kuharibika kwa 'screen' (kiambaza) hiyo kwa miaka kadhaa sasa ni changamoto kubwa kwa wadau wa utalii na watalii wenyewe katika kujua ratiba za ndege na katika kupata taarifa mbalimbali," alisema.

Mdau mwingine wa utalii kutoka Kampuni ya Zara Tanzania Charity, Bernard Sihini, alisema kuharibika kwa kifaa hicho na ukosefu wa dawati la taarifa ni mtihani

INAENDELEA UK. 8



Sehemu ya ufukwe wa Coco, eneo la Oysterbay ambao Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, inatarajia kufanya maboresho na kuweka mazingira safi na kuwapa wafanyabiashara ndogondogo waliopo muda wa mwezi mmoja na nusu kuondoka ili kupisha maboresho hayo. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# 45 mbaroni kwa kuuza petroli kwenye makazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU 45 wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa kosa la kufanya biashara ya kuuza mafuta ya petroli na dizeli katika makazi yao bila leseni.

Watu hao wamekamatwa katika operesheni iliyoendeshwa na jeshi hilo na pia kukamata lita 2,118 za petroli na dizeli lita 2,327 zilizokuwa zikiuzwa katika makazi ya watu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu operesheni hiyo jijini hapa jana, alisema imefanyika chini ya Wakuu wa Polisi wa Wilaya zote (OCD) za mkoa huo.

Alisema lengo la operesheni hiyo ni kukomesha biashara ya mafuta hayo ambayo hivi sasa imekuwa ikishamiri katika makazi ya watu kinyume na sheria.

Alisema biashara hiyo ni hatari kuendelea kufanywa katika makazi ya watu kwa kuwa inahatarisha maisha kutokana na kuwa na uwezo mkubwa wa kulipuka kutoka na aina ya mazingira inavyohifadhiwa.

"Lazima wananchi wajifunze kutokana na tukio lililotokea kule kwa wenzetu wa Mkoa wa Morogoro, lori la mafuta liliporipuka na kuuwa vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa na kulitia hasara taifa ya kuwatibia majeruhi," alisema Kamanda Muroto.

Pia Kamanda Muroto aliwataka watuhumiwa hao 45 waliokamatwa kuacha kuendelea kujihusisha na biashara hiyo kinyume cha sheria.

"Nitowe wito kwa wanachi, vijana hawa tulio wakamata wengi wao umri ni kuanzia miaka 18 hasi 38 umri ambao ni nguvu hivyo basi waachane na tabia hiyo na kufanya shughuli nyingine itakayo waingizia kipato," alisema.

Katika operesheni hiyo wilayani Mpwapawa, jeshi hilo lilikamata watuhumiwa saba, Chemba watuhumiwa watano, Bahi (1), Kongwa (8), Chamwino (13), Kondoa (2) na Dodoma jiji (7).

Katika tukio jingine Kamanda Muroto alisema wamekamata noti bandia zenye thamani ya Sh. 1,920,000 katika kijiji cha Chinugulu wilayani Chamwino mkoani Dodoma kwenye mnada.

Vilevile jeshi hilo linamshikilia Happy Gidioni (42), mkazi wa Kizota jijini Dodoma akiwa na pombe haramu ya moshi (gongo) lita nane na misokoto 20 ya bangi na bangi kavu isiyosokotwa nusu kilo.

# Wahukumiwa kunyongwa kuua kwa kukusudia

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, imewahukumu kunyongwa hadi kufa vijana watatu baada ya kukutwa na hatia ya kuua kwa kukusudia.

Waliohukumiwa ni Nathaniel Elias (31), Moses Kasitu (26) na Elias Mzumbwe. Akitoa hukumu hiyo Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Dk. Adam Mambi, alisema mahakama imetoa hukumu hiyo kutokana na kuridhishwa na ushahidi wa upande wa mashtaka ili adhabu hiyo iwe fundisho kwa wengine ambao wanapenda kujipatia mafanikio kwa njia za mkato kwa kusababisha mauaji. Awali, akisoma shauri hilo Jaji Mambi, alisema washtakiwa hao walitenda kosa hilo Julai 25, 2014 eneo la Mpemba katika Halmashauri ya Mji wa Tunduma Wilaya ya Momba, mkoani Songwe. Jaji Mambi aliongeza kuwa washtakiwa walimvamia na kumuua Vascal Njowela, akiwa ametoka dukani alikokuwa akifanya biashara na alikuwa akielekea kwa bosi wake kupeleka mauzo ndipo alipokutana na wauaji hao akiwa getini kwa bosi wake huyo na kumuua kwa kumpiga risasi, na kuchukua kiasi cha Sh. milioni moja.

Wakili wa utetezi Jastian Mshokolwe, adai kuwa kulingana na ushahidi uliotolewa na mashahidi wa mashtaka hana budi kukubaliana na hukumu hiyo huku akisema nafasi ya rufani kwa wateja wake bado ipo. "Sinabudi kukubaliana na hukumu hiyo, lakini nafasi ya kukata rufaa kwa wateja wangu bado ipo, haki itaendelea kutafutwa katika ngazi za juu," alisema Mshokolwe.

Naye Wakili wa Serikali, Shindani Michael, kwa upande wake ameishukuru mahakama kwa kutenda haki kwa hukumu hiyo ili iwe fundisho kwa wananchi wengine wenye nia ya kufanya makosa kama hayo.

Nje ya mahakama, wananchi kwa upande wao, wakiongozwa na Adam Juma, walipongeza mahakama hiyo kwa hukumu hiyo, wakisema kuwa vitendo vya ukatili katika mkoa huo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara na kwamba kwa adhabu hiyo anaamini wataogopa kutenda mauaji.

"Ni ukatili mkubwa uliofanyika kuua na kupora fedha tena milioni moja, huu ni unyama usio na kifani, tumechoka kusikia mauaji yakiendelea mkoani kwetu, maana kila kukicha utasikia auawa kwa wivu wa mapenzi, mara dereva bodaboda auawa na kuporwa pikipiki, hii ni aibu," alisema Juma.


Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@gmail.com**

*Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30*

615421902

# Kabendera adai kukabiliwa tatizo la pingili za mgongo

**Na Hellen Mwango**

MWANDISHI wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera anayekabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha wa zaidi ya Sh. milioni 100, ameiambia mahakama kuwa amepata matibabu na majibu ya awali yameonyesha ana matatizo ya pingili za mgongo. Pia, amedai kwamba amepata vipimo vya damu majibu yake anatarajia kupata mwisho wa wiki.

Madai hayo aliyatoa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile wakati akimpa taarifa kuhusu kupata huduma za matibabu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa

INAENDELEA UK.8



Meneja Mapato wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka jijini Dar es Salaam, Edgar Zawayo (kushoto), akishuhudia bwawa linalotumika kuhifadhi maji yaliyoibwa kwa ajili ya umwagiliaji eneo la Mbweni jana. Watuhumiwa wanashikiliwa na polisi wakisubiri kufunguliwa mashtaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




## Jela miaka miwili kwa kufanyakazi bila kibali

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemhukumu Meneja wa Kampuni ya Fuel Security Co. Ltd., Malcom Doherty, kulipa faini ya zaidi ya Sh. milioni 11 au kwenda jela miaka miwili baada ya kukutwa na hatia ya kufanyakazi nchini bila kibali, kutoa taarifa za uongo na kujiingiza kwenye ajira bila kibali.

Mshtakiwa huyo raia wa Uingereza amehukumiwa juzi katika mahakama hiyo.

Hukumu hiyo, ilitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Alisema mahakama imemtia hatiani mshtakiwa huyo katika mashtaka yote matano yaliyokuwa yakimkabili.

Alisema mshtakiwa amekutwa na hatia kwa mashtaka yote na kwamba atalipa faini ya Sh. 500,000 kila kosa kwa makosa mawili au kwenda jela mwaka mmoja mmoja.

Pia, alidai kuwa mshtakiwa atalipa faini ya Sh. 100,000 au jela mwaka mmoja kwa makosa mawili.

"Mahakama yangu inakuhukumu kulipa faini ya Sh. milioni 10 au kwenda jela miaka miwili baada ya kukutwa na hatia ya kujiingiza katika ajira bila kibali," alisema Hakimu Simba wakati akitoa adhabu hiyo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa aliingia nchini bila kibali, kuishi nchini bila kibali na kuwandanganya maofisa Uhamiaji kuhusu uraia wake. Kutokana na makosa hayo atatumikia kifungo cha mwaka mmoja jela au kulipa faini ya Sh. 500,000 kila kosa.

Mashtaka mengine ni kutoa taarifa za uongo kuwa yeye ni Mtanzania wakati akijua si kweli, kwa kosa alitakiwa kulipa faini ya Sh. 100,000 au jela mwaka mmoja. Mshtakiwa huyo alishindwa kulipa fedha hizo na amepelekwa gerezani.

Katika utetezi wake, mshtakiwa huyo aliiomba mahakama msamaha kwa kuwa ni raia mwema, ana mke ambaye ni Mtanzania na kwamba aliibiwa hati yake ya kusafiria.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa huyo anadaiwa kutenda makosa hayo, Oktoba 19, 2017 katika Ofisi za Uhamiaji Wilaya ya Kigamboni , Dar es Salaam.

## TMA yatoa darasa SADC

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya hali ya hewa nchini (TMA) imesema imekuwa mstari wa mbele kutoa utaalam wao kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, SADC.

Akizungumza jana kwenye mkutano unaoendelea wa Mawaziri wa nchi za SADC na Mamlaka za Hali ya Hewa, Kaimu Meneja wa Utabiri wa TMA, Wilberforce Kikwasi, alisema kuwa huduma za hali ya hewa zinazotolewa na TMA ni msaada mkubwa kwa nchi wanachama wa SADC katika kufuatilia mabadiliko ya hali ya hewa na namna ya kukabiliana nayo.

"TMA katika mkutano huu tunawaonyesha wenzetu namna tunavyofanya kuchakata na kutoa taarifa za hali ya hewa kwa wananchi.. nchi yetu inatumika kimkakati katika ukanda huu na hii ni kutokana na miundombinu tuliyonayo ambayo serikali imetusaidia sana," alisema Kikwasi.

Aidha, alisema wananchi wana nafasi kubwa ya fursa za kiuchumi kwa kufuatilia na kuzitumia taarifa za hali ya hewa.

"Biashara pia zinategemea sana taarifa za hali ya hewa.. na shughuri nyingine pia za kimaendeleo, TMA tunawashauri wananchi wafuatilie taarifa tunazozitoa," alisema.

Pia aliesema TMA imekuwa ikipata uzoefu kwenye mkutano huo kwa nchi ambazo zimepitia majanga yanayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Kuna nchi kama Msumbiji hivi karibuni wamekumbwa na kimbunga, tunapata uzoefu na kujifunza namna walivyokabiliana nacho," alisema.

Alisema maendeleo ya wakati ujao kwa Tanzania, SADC na nchi zote za Afrika zinategemea zaidi taarifa za hali ya hewa, hivyo wadau na wananchi kwa ujumla wanapaswa kuzifuatilia.

Mkutano huo wa mawaziri wa SADC unafanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na mawaziri wa nchi hizo pamoja sekta ya hali ya hewa na Tehama.

## TANGAZO


game
Tsh 16000 DEALS
NOW AVAILABLE AT GAME TANZANIA
DEALS VALID FROM 20 SEPTEMBER UNTIL 20 NOVEMBER
Tsh16 000 EACH
Maq Handwash 3kg
Tsh16 000 EACH
Maq Auto Washing Powder 2kg
ANY 2 FOR Tsh16 000
Maq Softener Assorted
ANY 7 FOR Tsh16 000
Dettol Soap Assorted 175g
4 FOR Tsh16 000
Famasi Hand Wash 500ml
5 FOR Tsh16 000
Fruitree Juice 1l Assorted
4 FOR Tsh16 000
Lentheric I Love Vanilla 125ml
6 FOR Tsh16 000
American Garden Baked Beans
2 FOR Tsh16 000
Weetbix Mini Chocolate 450g
Tsh16 000 EACH
De Nigris Apple Cider Organic 500ml
10 FOR Tsh16 000
Bullet Energy Drink 250ml
2 FOR Tsh16 000
Milk Powder Tin 400g
2 FOR Tsh16 000
Heinz Ketchup 855g Glass Bottles
7 FOR Tsh16 000
American Garden Tomato Ketchup
5 FOR Tsh16 000
Eet Sum More 200g
Tsh16 000 EACH
Calvet VDP Assorted 750ml
5 FOR Tsh16 000
American Garden Mushroom
4 FOR Tsh16 000
Luminarc Cadix Dinner Plate 25cm
3 FOR Tsh16 000
Luminarc Dinner Plate
Game is committed to offer you the best service with the lowest price. In the unlikely event that you find the same product advertised by a competitor at a lower price, we guarantee to beat that price! . T's & C's apply.
DEALS VALID 20 SEPTEMBER - 20 NOVEMBER 2019
ITEMS AVAILABLE WHILE STOCKS LAST
All prices listed are in tanzanian shillings . All prices include VAT
TANZANIA, DAR ES SALAAM
SHOPPING HOURS
View this catalogue online at www.game.co.tz
Walmart
Save money. Live better.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali itupie jicho hizi 'pre form one'

**WANAFUNZI** zaidi ya 900,000 wamehitimu darasa la saba mwezi huu na sasa kinachoendelea ni maandalizi ya kujiunga na masomo ya sekondari kwa kidato cha kwanza.

Wakati wazazi na walezi wakifikiria hatua ya kuwaandaa watoto kwa masomo ya sekondari, shule za binafsi za sekondari zinaanza kufurahia mafanikio makubwa yanayofuata kwani kama wawekezaji wanaingia kwenye maandalizi ya 'pre form one.'

Wawekezaji binafsi wa sekta ya elimu wanakubaliana nasi kuwa kinachofuata sasa ni maandalizi ya kuwakaribisha vijana kujiunga na kozi za 'pre form one' kwenye shule mbalimbali kwa lengo la kuwasaidia kujiandaa na kujiunga na hatua ya sekondari mwakani.

Huu ndiyo msimu shule zinapoonza kutangaza gharama za kujiunga na kozi za miezi mitatu za kujiandaa na kujizoeza na mazingira ya kidato cha kwanza.

Wazazi na walezi wanaanza kutozwa fedha za chakula, malazi na mafunzo kwa watoto hawa ambao wengi wanakwenda kuishi bweni.

Hatukatai wala hatupingani na matayarisho hayo, ila kila kitu kikizidi kinakera. Mzigo wa kuwatoza wazazi fedha za maandalizi hayo ni mkubwa mno na kwa shule nyingine gharama hufikia hata Sh. 300,000 hadi Sh. 500,000.

Wahusika wanafundisha watoto lakini wakati mwingine tunaona kuwa hakuna sababu ya kuwaumiza wazazi kiasi hicho. Tunajiuliza hivi kuna nini kikubwa hata kutoza gharama kubwa kiasi hicho kwa miezi miwili na nusu ya kukaa na watoto hao shuleni?

Kuna shule zinazoanza kuwaweka watoto kuanzia Oktoba hadi Desemba kwa gharama hizo za kati ya Sh. 300,000 hadi Sh. 500,000 wakiambiwa wanafundishwa na kuandaliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Wengine hutakiwa kufika shuleni na magodoro, sare, vitabu na gharama nyingine nyingi ambazo lengo lake ni kutunisha mfuko wa shule. Ili kuondokana na usumbufu kwa wazazi kununua mahitaji hayo hupewa bajeti ya Sh. 400,000.

Tunaona kama wazazi na walezi, nao wanahitaji kufahamu taarifa za kutosha kuhusu gharama wanazotoa kwa ajili ya kugharamia programu za 'pre form one'.

Kwa hiyo taratibu za kujua na kufikia gharama hizo ni lazima pia zifanyike kwa utaratibu unaokubalika na unaoeleweka na kukubalika kwa wazazi na walezi.

Aidha, ni vyema pia kufahamu watoto wanaandaliwa kwenye eneo gani ambalo wakifika shuleni kuanza kidato cha kwanza litakuwa lina tija kwao.

Tunasema hivyo kwa sababu huenda hakuna kingine cha tofauti watoto wanachojifunza mbali na kupewa ufahamu kuhusu masomo ya kidato cha kwanza.

Ina maana gani kutangaza kozi za 'pre form one' na kuwafundisha watoto, Kemia, Historia, Fizikia, Bailojia na lugha za kigeni kwa miezi michache ya mwanzo kabla ya kujiunga na kidato cha kwanza kwa kisingizio kuwa ni maandalizi ya kuingia kidato cha kwanza?


Ndiyo maana tunaona ni lazima suala la maandalizi ya 'pre form one' sasa yawe wazi.

Ikumbukwe kuwa japo maandalizi hayo hufanywa zaidi na shule za binafsi, ukweli ni kwamba kuna vikundi vingine ambavyo huandaa mafunzo hayo ambayo si rasmi.

Tunaomba kwa sababu imeonekana kuwa ni suala lenye tija kwa taifa ni vizuri serikali ni wadau wa elimu wakiwamo shule za sekondari za binafsi na za umma wakakutana na kupanga yanayotakiwa kuwamo kwenye mafunzo ya 'pre form one.'

Tunashauri utaratibu uanze sasa kwa kuwa hatujachelewa hilo linawezekana ili kuondoa mkanganyiko huo ambao unahitaji ufafanuzi na utaratibu unaokubalika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Chuki ya Weusi A/Kusini Afrika inavuna ilichopanda

Na Gaudensia Mngumi

**UHASAMA** na chuki dhidi ya wahamiaji kutoka nchi mbalimbali za Afrika wanaoishi Afrika Kusini ni tatizo linaloonyesha udhaifu uliomo ndani ya viongozi wa Afrika walioongoza nchi zao baada ya uhuru zaidi ya miaka 50 iliyopita. Kutopendana na kuchukuliana kama maadui miongoni mwa Waafrika kunadhihirisha kuwa kinachoitafuna Afrika ni umaskini unaotokana na uongozi mbaya uliotawaliwa na ufisadi na ukandamizaji kwa muda wote tangu uhuru miaka ya 1960.

Afrika inayokaribia kuwa na watu takriban bilioni moja, inakabiliwa na changamoto kubwa ya kuwageuza vijana wake wenye munkari, jazba na wasio na uvumilivu wala subira kuwa mtaji kwa ajili ya uwekezaji wenye tija.

Hata hivyo, bara halitaweza kuwatumia vijana wala nguvu kazi hiyo kuwa rasilimali ya kujipatia maendeleo kwa vile uchumi wa nchi pamoja na rasilimali zilizokuwa ziwaendeleze zimehujumiwa na viongozi na kuliacha bara kuwa fukara licha ya kuwa na utajiri mkubwa usio na mfano. Vijana hawana kazi, chakula, elimu, makazi, mavazi wala hawajui hatma yao ndiyo maana wamekuwa chanzo cha uhasama, chuki, vita na kutumika na yeyote anayetaka kulihujumu bara hili.

Kinachotokea Afrika Kusini leo ni matokeo ya viongozi kutokuwajibika kuwapa huduma za kijamii na kiuchumi pamoja na kuwaandaa vijana wa bara hili ili wajitegemee na kuwa raia bora na viongozi wenye maono na mikakati kwa ajili ya Afrika.

Ndiyo maana viongozi wa bara hili wanastahili kubeba lawama kutokana na vijana kuwa chanzo cha chuki barani hapa kwa kuwa serikali zimeshindwa kuleta maendeleo kwenye nchi zao.

Aidha, viongozi kushiriki kuhujumu bara hili tangu uhuru hadi sasa. Watu wanapojiuliza ni kwanini vijana kutoka sehemu mbalimbali wakimbilie Afrika Kusini? Ukweli ni kwamba kwenye mataifa yao hakuna huduma muhimu kama kazi, chakula, elimu, makazi na hatma (future) kwa ajili ya watu wake.

Chanzo cha tatizo hilo ni nini? Kila mmoja ana jibu lake, lakini linaloweza kutolewa haraka ni viongozi waliojitajirisha na kushirikiana na mafisadi kuhujumu utajiri wa Afrika badala ya kutumikia umma.

Matatizo ya uongozi yaliyokuwa Ethiopia, Somalia, Eritrea na Djibout yalisababisha maelfu ya vijana kuvuka mpaka na kuingia Tanzania yakielekea Afrika Kusini kupitia Malawi na Zimbabwe.

Maelfu ya wakimbizi hao wanakamatwa kila mwaka nchini, wengine wakiwa ndani ya malori na hata miili ya wahamiaji hao inatelekezwa porini na kuliwa na wanyama na ndege.

Shida za kiusalama, chuki za kikabila na udini unatikisa pia Nigeria, Togo na Jamhuri ya Afrika ya Kati na kusababisha maelfu kukimbilia Afrika ya Kusini.

Kuna viongozi wa kitaifa walioshiriki mauaji ya kimbari ili kutokomeza kabila ambalo kwa asili halikubaliki kwenye nchi na uongozi uliokuwa madarakani. Hawa nao wanajijua.

Afrika Kaskazini kuna makabila ya asili ambayo hayapewi nafasi ya kuongoza taifa wakiwamo Watuareg ambao muda wote wanadharaulika na hawakubaliki.

Hao nao ni chanzo cha wahamiaji kuondoka Afrika Kaskazini na kutumbukia ndani ya Bahari ya Mediteranean.

Vita visivyo na sababu huko Congo navyo vinasababisha wahamiaji hao kujipeleka Afrika Kusini. Ukweli ni kwamba wakuu wa nchi wanaoshiriki kwenye wizi na uporaji wa mali za umma badala ya kujenga uchumi na kuleta maendeleo wabebe lawama za sasa kwani wanaisababishia Afrika ivune ilichopanda.

Wakuu wengi wa nchi za Afrika walikuwa ni waporaji wa mali za umma, mafisadi, wenye wivu, wasioheshimu haki za binadamu, wauaji, watesaji na walitumia muda wao mwingi kutawala na kujitajirisha bila kujali hatma ya vizazi vijavyo.

Kinachotokea Afrika leo ni picha halisi ya jinsi viongozi walioliongoza bara hili baada ya uhuru walivyoshindwa kuviandaa vizazi vya baada ya uhuru ili kuwa sehemu ya kuendeleza uchumi wa mataifa yao.

Licha ya chuki dhidi ya wahamiaji huko Afrika Kusini, mataifa mengi ya bara hili na marais wao wanaendeleza sera za chuki na kuendekeza ukabila wala si umoja wa kitaifa.

Ni bara ambalo dini inatumiwa kuongeza chuki, uhasama na hata mauaji. Chuki dhidi ya wahamiaji ni uthibitisho kuwa hakuna aliye tayari kuishi kwa furaha na kwa upendo na jirani yake, awe wa taifa jirani au kabila analopakana nalo ndani ya taifa lake.

Mgogoro ulioko Sudan Kusini baina ya Rais Salva Kiir na makamu wake Riek Machar, ni kielelezo kingine cha uongozi mbaya wenye sura za chuki za kikabila utakaohatarisha hatma ya Afrika kwa siku zijazo.

Ni jukumu la Afrika sasa kukaa na wataalamu wake na kutafuta mikakati, mbinu na rasilimali za kutumia utajiri uliopo ili kuondokana na changamoto zinazozua uhasama unaoendelea Afrika Kusini.

# Bil. 1/- zasakwa kwa matibabu watoto moyo

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametangaza kutafuta Sh. bilioni moja kwa ajili ya kuokoa maisha ya watoto wanaosumbuliwa na magonjwa ya moyo ili ifikapo mwezi Desemba waweze kusherehekea sikukuu wakiwa na afya njema.

Makonda alitoa kauli hiyo jana katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) wakati wa uzinduzi wa kambi inayoshughulikia matatizo ya moyo ijulikanayo kama Small Heart Foundation ambayo ilianza kazi Septemba 13.

Kambi hiyo imehusisha wataalamu kutoka Shajiah Charity Group waliokwenda JKCI kutoa matibabu kwa wagonjwa wenye matatizo ya moyo wa kuzaliwa na kutoa mafunzo kwa madaktari wa taasisi hiyo.

Makonda alisema anataka ifikapo mwezi Desemba wawe wamepata fedha hizo ili ziweze kuokoa maisha ya watoto waliopo JKCI ambao anaamini wakati wananchi wakisherehekea sikukuu nao wawe na furaha.

"Kuna watu wanahoji, Makonda huwa anapata wapi fedha za kusaidia. Nchi hii ni tajiri na watu wa nchi hii ni tajiri wanachotaka ni mtu mwaminifu, mwadilifu anayeomba fedha kwa mtumizi sahihi.

"Balozi huyu (Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Khalifa Abdulrahman), ana marafiki wengi lakini wanakaa naye kunywa kahawa, mimi nimekaa naye kunywa naye kahawa amesaidia matibabu ya watoto hawa, nimekaa naye amesaidia wanafunzi 100 wanasoma kidato cha tano.

"Wewe kaa naye kwa kwa ajili ya mtoto wako mmoja akasome, atakwenda kusoma na matokeo yake atafaulu kwa sababu utakuwa umeitumia nafasi yako ya uongozi kwa faida yako binafsi. Ukitumia kwa mafanikio ya wengi, Mungu atakuinua."

Makonda alisema Novemba na Desemba itakuwa ni miezi ya shukrani hivyo ipo kamati maalum ambayo miongoni mwake yupo Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, ambapo watatafuta Sh. bilioni moja kwa ajili ya matibabu ya moyo kwa watoto.

"Benki zipo 56 tutatafuta benki kumi kila moja itoe Sh. milioni 20, kampuni za malori kumi nazo kila moja ikitoa Sh. milioni 10, tukipata kampuni 50 mwezi wa Desemba wakati watu wakisherehekea sikukuu na mtoto mwenye tatizo la moyo afurahi kwa kurejeshewa uhai wake," alisema.

Makonda alisema kwa kushirikiana na balozi huyo wanafanya utaratibu wa kuwapatia bima watoto wadogo wanaofanyiwa upasuaji JKCI ili wasipoteze maisha kwa kukosa fedha wakati wakiendelea na kliniki zao.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alishukuru kambi hiyo hiyo pamoja na Makonda kwa kazi kubwa inayofanyika ya kutafuta wafadhili wa watoto katika matibabu ambapo hadi sasa 30 wameshafanyiwa upasuaji.

Naye, Balozi Abdulrahman alisema nchi za Falme za Kiarabu zinajali kwa kupeleka misaada kwa nchi rafiki.

Kwa upande wake, Prof. Janabi alisema katika kipindi cha miaka mitatu kati ya wagonjwa 65, mmoja ndiye walimpoteza lakini wengine wanaendelea vizuri.




Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kushoto) na Balozi wa Umoja wa Falme za Kiarabu nchini, Khalifa Abdulrahman Mohammed Al Marzooqi, wakizungumza na watoto, kwenye hafla ya kuhitimisha matibabu ya moyo, yaliyoratibiwa na Sharjah Charity Group-Umoja wa Falme za Kiarabu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwanasiasa afungwa miaka 99 kwa utapeli

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemhukumu mwanasiasa, Salma Issa Mntambo, kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka 99 baada ya kupatikana na hatia ya makosa 17 yaliyokuwa yakimkabili ikiwamo kuwasilisha nyaraka za uongo na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Salma aligombea ubunge Korogwe Mjini kupitia ACT-Wazalendo mwaka 2015

Kadhalika mahakama hiyo imesema inakwenda kutafakali na kufanya utafiti mpaka Oktoba 2, mwaka huu itatoa uamuzi kuhusu mshtakiwa kutoa fidia.

Hukumu hiyo ilisomwa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kevini Mhina.

Alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi watano wa upande wa Jamhuri bila kuacha shaka wamethibitisha makosa 17 kati ya mashtaka 24 yaliyokuwa yanamkabili.

"Mahakama hii imekutia hatiani katika makosa 17 kati ya 24, utakwenda jela miaka mitano kwa kila kosa kwa makosa matatu ya kuwasilisha nyaraka za uongo,"alisema na kuongeza.

"Pia mahakama hii inakutia hatiani kwa makosa 14 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu hivyo mshtakiwa utakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka sita kwa kila kosa". Alisema. Hakimu Mhina wakati akimsomea hukumu hiyo katika ukumbi namba tatu wa mahakama hiyo mapema jana.

Akifafanua hakimu alisema mshtakiwa atatumikia adhabu hizo sambamba na kwamba atakaa jela miaka sita.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa alikuwa akikabiliwa na mashtaka 24 hata hivyo ametiwa hatiani katika mashtaka 17 yakiwamo ya kutakatisha fedha jumla ya Sh. Bilioni 1.027,000,000 kutoka kwa Ridhuan Mringo huku akijua fedha hizo zimetokana na zao la makosa tangulizi ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuwasilisha nyaraka za uongo.

Katika kosa la kughushi, mshtakiwa Mntambo anadaiwa kati ya Juni mosi 2003 na Oktoba 31, 2011 maeneo yasiyojulikana wilayani Ilala, mkoani Dar es Salaam kwa nia ya udanganyifu alighushi risiti yenye namba 001226 ya tarehe 10/06/2003 ili kuonesha kwamba Ridhuan Mringo alinunua nyumba ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) iliyopo Plot namba 710 Mtaa wa Mfaume Upanga kwa Sh. milioni 70 wakati akijua ni uongo.

## Maofisa Tanroads waachiwa huru

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma imewaachia huru washtakiwa wawili, Mhandisi Ofisi ya Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads), Geofrey Mutakubwa (44) na Mkurugenzi wa Kampuni KAGECO Civil Works and Building Contractors Company Ltd, Theonest Bagasingire (52), baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha makosa 12 yaliyokuwa yakiwakabili.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Flora Mtarania na washtakiwa wote waliachiwa huru.

Mtarania alisema washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na makosa 12 kati ya hayo 11 ni ya ukiukwaji wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11/2017 na kosa moja la utakatishaji fedha Sh. milioni 24.4, kinyume na sheria namba 12/2006.

Alisema upande wa mashtaka ulidai kuwa mshtakiwa wa kwanza na wa pili walikuwa wakitumiana fedha kuanzia mwaka 2013 hadi 2018, lakini cha kushangaza hawakueleza fedha hizo badala yake walieleza kuanzia mwaka 2017 na 2018 na kwamba kuna upungufu ambao ulitolewa na upande wa mashtaka, pia katika kesi za jinai upande wa mashtaka ndiyo unatakiwa uthibitishe kosa au makosa na ukishindwa kufanya hivyo ni faida kwa washtakiwa.

Hakimu alisema upande wa mashtaka umeshindwa kuthibitisha makosa ya rushwa na utakatishaji fedha, hivyo mahakama hiyo kuwaachia huru washtakiwa wote. Alisema upande ambao haujaridhika na uamuzi huo rufani ipo wazi.

Upande wa mashtaka uliongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Jamhuri kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kigoma, Boniface Kamwesigile na upande wa utetezi ulikuwa ukiongozwa na mawakili watatu wa kujitegemea, Diocles Rutahindurwa, Raymond Kabuguzi na Ignatus Kagashe.

Awali, akisoma hati ya mashtaka Mwendesha Mashtaka wa Jamhuri kutoka Takukuru, Kamwesigile alidai kati ya Febuari 2017 na Januari 2018 maeneo ya Mkoa wa Kigoma, mshtakiwa wa kwanza Mutakubwa, alitenda makosa sita ya kutumia mamlaka vibaya, kujipatia manufaa yasiyo halali, kujihusisha na vitendo vya rushwa katika manunuzi na kujihusisha na vitendo vya rushwa katika mikataba.

Pia mshtakiwa wa pili, Bagasingire anakabiliwa na makosa matano ya kujihusisha na vitendo vya rushwa katika manunuzi na mikataba.

Kamwesigile aliendelea kueleza mahakamani hapo kuwa washtakiwa wote kwa pamoja walitenda kosa la utakatishaji fedha Sh. 24,600,000 kupitia akaunti za benki ya CRDB Tawi la Kigoma, Urambo, Tabora na Ubungo jijini Dar es Salaam huku wakijua kuwa fedha hizo zilikuwa ni mazao ya rushwa.

# Askari kupiga kura siku 1 kabla uchaguzi

INATOKA UK. 2

**ZITTO AFUNGUKA**

Kiongozi Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema tangu awali walishaweka wazi kuwa mabadiliko ya sheria hiyo yana changamoto kubwa na yanaweza kuleta mtafaruku mkubwa visiwani huko kwa kuwa Baraza la Wawakilishi na serikali haijaridhiwa na wote.

"Baraza la Wawakilishi ni la chama kimoja, uamuzi umefanywa na upande mmoja na hatua walizochukua za kufanya mabadiliko ya sheria ni wa maslahi ya chama kimoja.

"Mabadiliko haya hayana maana, yatazuia vyama kukagua uhalali wa kura, hayaambatani na daftari, tofauti la watu wa vikosi, hapatakuwa na mawakala wa vyama kwenye kambi za jeshi," alisema. Zitto ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini, alisema kutokana na uzoefu wa uchaguzi wa Zanzibar, maridhiano ili uchaguzi ujao ufanyike kwa hali ya amani, ni muhimu yakahusisha CCM na vyama vya upinzani.

"Baada ya uchaguzi uliopita kufutwa, CUF na vyama vingine havikuunga mkono, hadi sasa hakuna mazungumzo yoyote kuhakikisha matatizo hayatajirudia, na sasa wamekuja na jambo lingine linalokwenda kuweka tatizo kubwa zaidi," Zitto alitahadharisha.

Zitto alisema utaratibu wa baadhi ya makundi kupiga kura siku moja kabla unafanyika kwa baadhi ya nchi, lakini akasisitiza kuwa tatizo kubwa ni mazingira hatari ya siasa za Tanzania yatakayochagiza uchaguzi kuvurugwa na kuhatarisha amani.

"ACT-Wazalendo tunaona mazungumzo yatakayopelekea mashauriano ni muhimu ili tuwe na uwanja sawa wa uchaguzi, ili Wanzanzibar wapate mtu aliyechaguliwa na wananchi wenyewe.

"Ni muhimu kutaka kuwa na mazingira ya kuwezesha uchaguzi uwe huru na haki, uchaguzi wa Zanzibar umekuwa na vurugu na kumwaga damu.

"Hadi sasa, haki ya uchaguzi wa Zanzibar haijakuwapo, ni muhimu mazunguzo kuwapo. Hadi sasa, hatutambui serikali na Baraza la Wawakilishi, ni muhimu pande zote zikubaliane badala ya tume kujiamulia, naamini Wazanzibar hawatakubali haki yao kuporwa tena," Zitto alidai.

**KAULI YA CUF**

Msemaji wa Chama cha Wananchi (CUF), Abdul Kambaya, alidai uamuzi wa ZEC kutekeleza sheria hiyo ni mbaya kwa mustakabali na ustawi wa demokrasia siyo tu visiwani Zanzibar bali kwa Tanzania nzima.

"Vyombo vya usalama visijengewe utaratibu wa kuhusishwa moja kwa moja katika uamuzi wa mgombea gani awe kiongozi kwa nafasi yoyote katika uchaguzi, kufanya hivyo kutajenga chuki miongoni mwa wananchi," Kambaya alitahadharisha.

HABARI ZAIDI UKURASA WA 23




Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (wa kwanza kulia), Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta, Luteni Kanali mstaafu, Dk. Haroun Kondo (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), wakifurahia uzinduzi wa uwakala wa huduma za kibenki kati ya Shirika la Posta na NBC, jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# NBC yatanua huduma zake kupitia Shirika la Posta

**Na Ecock Charles**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imeingia makubaliano ya uwakala wa huduma za kibenki na Shirika la Posta nchini, ili kupanua wigo wa huduma za benki hiyo sambamba na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kifedha hasa maeneo ya vijijini.

Hatua hiyo inatajwa kuwa itaongeza wigo wa mtandao wa utoaji huduma za kifedha kwa njia ya kijiditi, huku ikienda sambamba na azma ya serikali ya kupanua ushiriki wa wananchi katika shughuli za kifedha (financial inclusion).

Akizungumza katika hafla ya utiaji saini mkataba wa kutoa huduma za kubenki kati ya Posta na NBC jijini Dar es Salaam jana, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, alisema kupitia mtandao wa ofisi za Shirika la Posta nchini lenye mtandao wa matawi 370, kutaiwezesha Benki ya NBC kuwafikia maelfu ya wananchi nchi nzima katika utoaji wa huduma zake za kibenki kwa gharama nafuu.

"Ushirikiano huu kati ya NBC na Posta utawezesha ukusanyaji wa kodi na maduhuli ya serikali kwa urahisi zaidi. Kwani ulipaji wa kodi na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali yatafanyika katika mazingira salama na rafiki kwa wananchi kupitia ofisi za Posta. Wafaidikaji wa ushirikiano huu kati ya NBC na Posta sio tu wateja bali watakuwapo wastaafu, wanafunzi, wakulima, wazazi, na wafanyabiashara, alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema ushirikiano huo utawawezesha kutumia mifumo ya kidijitali na wingi wa ofisi za posta katika kutoa huduma za kibenki nchi nzima.

"Kwa sasa NBC ina mawakala wapatao 2,000, hivyo kuungana na Shirika la Posta, kupitia mtandao wa ofisi zake 370, kutatuwezesha kuongeza idadi ya wananchi watakaofikiwa na huduma za kibenki kwa urahisi," alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo, ni utekelezaji wa maelekezo ya serikali kwa benki za kupeleka huduma ya kifedha kwa wananchi hasa walioko mikoani na vijijini.

Posta Masta Mkuu, Hassan Mwang'ombe, alisema kwa kuanza shirika hilo na NBC wataanza kutoa huduma katika ofisi 99 zilizo maeneo mbalimbali nchini.

"Huduma hizi ni zile zote za kibenki, kukusanya mapato ya serikali, kuhamisha na kutuma fedha, kufungua akaunti pamoja na huduma nyingine za kibenki.

"Katika kuimarisha shirika kibiashara na kurahisisha wananchi wapate huduma kwa ukaribu shirika tayari linashirikiana na taasisi kadhaa ikiwamo Benki ya Posta, Necta, MSD, Tanesco, NIC, mifuko ya hifadhi ya jamii, mashirika na kampuni mbalimbali," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta nchini, Luteni Kanali mstaafu Dk. Haroun Kondo, alisema kulingana na mageuzi ya kimfumo na maboresho mbalimbali yanayofanywa sasa na shirika hilo, yatatoa nafasi bora kwa taasisi na kampuni mbalimbali kuvutiwa kuweka ofisi au kuingia ubia wa kutoa huduma au uwakala wa huduma zake.

# Kabendera adai kukabiliwa tatizo la pingili za mgongo

INATOKA UK. 4

upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Wakili wa utetezi Jebra Kambole alidai kuwa amesikia hoja ya serikali, lakini anaiomba mahakama kumsikiliza mshtakiwa kuhusu taarifa ya matibabu yake.

Hakimu alimhoji mshtakiwa kuhusu malalamiko yake ya matibabu kama yamefanyiwa kazi au la.

Mshtakiwa alidai kuwa juzi alipelekwa Hospitali ya Amana na kufanyiwa vipimo mbalimbali ikiwamo kupigwa X-ray na damu.

"Mheshimiwa majibu ya awali yameonyesha nina matatizo ya pingili za mgongo na majibu ya damu natarajiwa kupata mwishoni mwa wiki," alidai Kabendera.

Alidai kuwa kwa sasa ameshapata huduma ya vipimo anasubiri matibabu na kwamba hana malalamiko mengine.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Oktoba Mosi, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019 katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173,247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Shtaka la tatu anadaiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

# Kifaa cha ukaguzi KIA hakifanyi kazi miaka 3

INATOKA UK. 3

kwao katika kupokea wageni kutoka mataifa mbalimbali.

Akijibu hoja za wadau hao wa utalii, Mkurugenzi wa Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji wa KIA (Kadco), Christopher Mukoma, alisema changamoto hizo wanazifanyia kazi.

"Hicho kifaa maalum kimechukua muda mrefu kuwekwa kutokana na Sheria ya Ununuzi ya Umma kufanyiwa mabadiliko, lakini kwa sasa tumeshamaliza taratibu zote na siku yoyote kuanzia sasa kifaa hicho kitawekwa katika uwanja huo," alisema.

Sheria hiyo ya mwaka 2011 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2016.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alikiri kuwapo kwa upungufu katika sekta ya utalii na kikiomba kikao hicho kuunda kamati ndogo itakayoshughulikia mambo mbalimbali yanayoikabili sekta ya utalii na viwanja wa ndege vya KIA na Arusha.

"Kutokana na changamoto za utalii kuelezwa hapa, nakiomba kikao hiki kikubali uundwaji wa kamati ya watendaji wa viwanja vya ndege, kampuni binafsi za utalii na watendaji wa serikali wakiwamo maofisa Idara ya Uhamiaji ili ni kuona namna ya kuboresha utalii nchini," Gambo alishauri.

Mkuu wa mkoa huyo pia aliwataka wadau wa utalii kuacha chuki za kibiashara na kupendana wao kwa wao ili kuleta mabadiliko ya sekta ya utalii.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolph Mkenda, alisema kikao hicho kililenga kushughulikia usalama na ufanisi wa biashara ya utali nchini.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa: Tutazitekeleza ahadi zote alizozitoa JPM

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema ahadi zote zilizotolewa na Rais John Magufuli ikiwamo ujenzi wa barabara ya Mikumi-Ifakara kwa kiwango cha lami zitatekelezwa, hivyo amewataka wananchi waendelee kuiamini serikali yao.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa Mji wa Ifakara pamoja na Wilaya ya Kilosa alipokuwa katika siku ya nne ya ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro.

"Kila alichokiahidi Rais John Magufuli nitakisimamia kuhakikisha kinatekelezwa, hivyo wananchi endeleeni kuiamini serikali yenu. Serikali yenu ipo makini na ina dhamira ya dhati ya kuwaletea maendeleo kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020 inavyoelekeza."

Waziri Mkuu alisema serikali iko makini na inaendelea kuchapa kazi kwa lengo la kutatua changamoto zinazowakabili wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini yakiwamo ya Mkoa wa Morogoro.

Pia, alisema kila mtumishi wa umma anatakiwa ahakikishe anafanya kazi kwa bidii ili kuiwezesha serikali kutimiza lengo lake la kuboresha maendeleo ya wananchi kwenye maeneo mbalimbali nchini hususani ya vijijini.

Waziri Mkuu alisema iwapo watumishi wa umma watatimiza majukumu yao ipasavyo, changamoto nyingi zinazowakabili wananchi kama upatikanaji wa maji zitakuwa historia kwa kuwa serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema watumishi wa umma wanapaswa kuwa na nidhamu ya fedha za serikali zinazopelekwa katika maeneo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ikiwamo ya afya, elimu na maji. "Sina mzaha na watakaotafuna fedha hizo."




Mafundi wakijenga shimo la majitaka ya vyoo vya Shule ya Sekondari ya Busambara, katika Kata ya Busambara, Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ambayo inatarajia kuanza kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Watumishi wanaotelekeza vituo afya usiku kutumbuliwa

**Na Gurian Adolf, KALAMBO**

MKUU wa Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, Julieth Binyura, ametishia kuanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi kwenye vituo vya afya na zahanati nyakati za usiku ili kubaini iwapo huduma za afya zinatolewa nyakati hizo.

Akizungumza juzi kwa nyakati tofauti katika vijiji vilivyopo katika kata za Lyowa na Matai akiwa kwenye ziara ya kutatua kero katika kata hizo, alipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi kuwa baadhi ya watumishi wa afya hawapatikani vituoni nyakati hizo.

Alisema ni lazima watumishi wa idara ya afya wawe wanaingia zamu zao kazini kama taratibu zilivyo, kwani baadhi yao wamekuwa wakitoroka zamu za usiku, hivyo kusababisha ukosefu wa huduma nyakati hizo.

Binyura alisema kuwa ili kukabiliana na tabia hiyo, ataanza utaratibu wa kutembelea maeneo hayo nyakati za usiku, na kwamba mtumishi atakaye atabainika kutoroka zamu yake na kurudi kulala nyumbani, atachukuliwa hatua kali.

Alisema kuwa serikali imeboresha sekta ya afya kwa kujenga miundombinu na kuhakikisha dawa zinapatikana, hivyo wajukumu la kuhakikisha wanahudumia wagonjwa kama taratibu za kazi zao zilivyo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Efraim Mwalemba, aliwaomba madiwani wa halmashauri hiyo kushirikiana na watendaji wa vijiji katika kukusanya na kusimamia mapato ya halmashauri.

Alisema kwa sasa serikali inahitaji mapato ili kuboresha huduma za jamii, hivyo ni jukumu lao kuhakikisha wanawasimamia watendaji katika kukusanya mapato ili yasivuje kwa kuwa wao ndio wana wawakilisha wananchi kama serikali itashindwa kuwatatulia changamoto wa kulaumiwa ni wao kwa kuwa hawakusimamia mapato yao vizuri.

# Miradi Tasaf kuwatumbua wakurugenzi

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, amesema serikali haitasita kuwang'oa wakurugenzi ambao wanashindwa kwenda vijijini kufanya shughuli za Mfuko wa Maendeleo (Tasaf) kwa kudai mpaka wapewe posho.

Gwajima alitoa angalizo hilo katika ziara yake ya kukagua, kutathmini na kuangalia changamoto za mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Tasaf katika mkoa wa Pwani.

Alisema mpango wa serikali ni kuwasaidia wananchi wanyonge kuwaondoa katika hali ya chini na kuwapeleka katika hali ya kati na kuhakikisha kila Mtanzania anafanya shughuli za maendeleo kwa lengo la kufikia uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda, hivyo kuwapo kwa baadhi ya watumishi kushindwa kuunga mkono malengo hayo kwa kusubiri posho ni kukwamisha malengo ya serikali.

"Tunajua uwapo wa mpango wa kunusuru kaya maskini ni miongoni mwa mipango ya serikali ya kuwakomboa wananchi wake hasa wanyonge, tumekuwa tukipata malalamiko baadhi ya viongozi katika halmashauri mbalimbali nchini wakiongozwa na baadhi ya wakurugenzi, ambao wanaunyanyapaa mpango huu, hawataki hata kwenda vijijini kuona shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na walengwa eti mpaka wapatiwe posho," alisema Gwajima.

Alisema anaamini kwamba wakurugenzi na viongozi wazuri na wazalendo ni wale wanaotanguliza mbele maslahi ya taifa na si vinginevyo.

"Kikao chochote kinachofanywa na mkurugenzi katika halmashauri na haongelei habari za Tasaf akiona kwamba hicho hakina maana wakati amesaini makubaliano yake, huyo hatufai na anapingana na maono ya Rais na ya serikali ya kuwakomboa wanyonge na kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati na viwanda," alisema.

"Tumeshuhudia viongozi wakiwamo wakurugenzi ambao anaweza akaenda kutekeleza shughuli za mradi 'A' wa serikali ambako hukohuko kuna mradi wa Tasaf, lakini anashindwa hata kutamani kujua maendelea katika miradi ya Tasaf eti tu kwa sababu hajapewa posho, nataka niwaambie kwamba serikali ya sasa inawataka watendaji kutekeleza ajenda zaidi ya moja, kwa sababu miradi yote lengo lake ni moja."

Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu Tasaf, Andrew Kibona, alisema ushiriki wa viongozi katika nyanja mbalimbali hususani katika kuwasimamia walengwa katika shughuli mbalimbali wanazozitekeleza, itasaidia kwa kiwango kikubwa walengwa kukua kiuchumi ili waondoke na kuwaachia wengine.

# Wananchi walilia chanjo ya ng'ombe

**Neema Emmanuel, KARAGWE**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameagiza kuundwa kwa timu ya wataalamu itakayokwenda wilayani Karagwe mkoani Kagera kuchunguza aina ya dawa ya chanjo inayotumika kuchanja ng'ombe.

Pia imeelezwa kuwa dawa hiyo imekuwa ikiwasababishia madhara ya kubabuka ngozi na vifo.

Ulega alitoa agizo hilo kwa kitengo cha utafiti cha magonjwa ya mifugo cha Kanda ya Ziwa kinachosimamiwa na Dk. Ally Shaka katika ziara wilayani Karagwe mkoani Kagera, baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wafugaji na wawekezaji wa ranchi ya Kikulila wilayani humo pamoja na wananchi wa kijiji cha Katanda Kata ya Kihanga.

Ulega alimwagiza Ofisa Mifugo wa Kanda ya Ziwa kuacha kukaa ofisini badala yake aende wilayani Karagwe kushirikiana na timu ya wataalamu wa mifugo kuchunguza dawa hiyo ambayo imekuwa kero kwa wafugaji, ambao wanadai mifugo yao inakufa na kubabuka ngozi.

"Chunguzeni hii dawa ili tupate jibu kwani malalamiko haya ni ya msingi na si ya kubeza, ng'ombe ni uchumi wetu...hivyo pale dawa zinapotumika na kuleta madhara kwa mifugo ya wananchi wafugaji wanyonge kama hao ni hasara kwao na kwa Taifa," alisema Ulega na kuongeza:

"Mfugaji huyu wa hali ya chini ng'ombe wake akifa ni pigo kubwa, hivyo tufanye uchunguzi wa kina ili tubaini tatizo na ikibainika dawa ilikuwa bandia basi hatua zichukuliwe haraka, na endapo waliochanja sehemu ambazo hazistahili basi hatua itajulikana."

Wakati huo huo, aliagiza Shirika la Ranchi za Taifa (Narco) zinapotokea fursa za uwekezaji katika sekta ya mifugo wafugaji walioko kwenye ushirika kupewa kipaumbele kwanza kabla ya kuwapatia watu wengine kutoka nje ya maeneo hayo.

Karim Amri na Jossam Ntangeki, wafugaji na wawekezaji katika ranchi ya Kikulula, huku Audax Mwombeki pamoja na Sabi Lwazo ambao ni wakazi wa kijji cha Katanda Kata ya Kihanga wilayani Karagwe walitoa malalamiko yao kwa Ulega.

Walisema baada ya mifugo yao kuchanjwa kupitia wataalamu wa halmashauri, baadhi walipata madhara ya kuvimba ngozi kupata malengelenge, na wengine wakifa. "Tunashauri tupewe ruhusa tununue dawa ya chanzo sisi wenyewe yenye viwango tuwaletee halmashauri tuwalipe ada ya kuchanja watuchanjie kuliko kutumia hizo dawa zao bandia na kuchanja ng'ombe wetu na kutusababishia hasara," alisema Sabi Lwanzo na kuongeza:

"Mimi ng'ombe wangu wawili walikufa na hata kwa jirani yangu walikufa."

# BoT yafunguka madai sarafu mpya ya 3,000/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania imesema hakuna sarafu ya Sh. 3,000 iliyotengenezwa kama taarifa zinavyosambaa kwenye mitandao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwenye vyombo vya habari na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki ya BoT, taarifa hizo siyo za kweli na sarafu hiyo siyo mali ya benki hiyo.

Taarifa iliyosambaa mtandaoni ilionyesha kuwa mwezi Julai mwaka huu, BoT ilitoa sarafu ya kumbukumbu ya visiwa vya Dokdo yenye thamani ya Sh. 3,000.

"Benki Kuu inapenda kuufahamisha umma kuwa taarifa hizi si za kweli na sarafu hiyo siyo mali ya Benki Kuu ya Tanzania na haijatolewa na BoT kwa njia yoyote ile," ilisema taarifa hiyo na kuongeza kuwa:

"Benki Kuu haijawahi kuingia mkataba na kampuni yoyote kutoa sarafu hiyo."



Mwonekano mpya wa kuvutia katika eneo la Victoria, Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam, baada ya kushamiri kwa ujenzi wa majengo ya ghorofa. **PICHA: JOHN BADI**

# Majaliwa atilia shaka gawio serikali kiwanda cha sukari

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, amesema hajaridhishwa na gawio la Sh. milioni 800 linatolewa na kiwanda cha sukari cha Kilombero ambacho uzalishaji wake ni mkubwa ikilinganishwa na kiwanda cha sukari cha Moshi (TPC) ambacho kinatoa gawio la Sh. bilioni 15 kwa mwaka.

Waziri Mkuu aliyasema hayo juzi alipotembelea kiwanda hicho, akiwa katika siku ya nne ya ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro. Alivitaka viwanda vya sukari nchini kuzaliza sukari ya kutosha ili kukidhi mahitaji.

Akizungumzia kuhusu vibali vya uagizaji wa sukari, Waziri Mkuu alisema serikali iliamua kutoa nafasi ya kuagiza sukari kwa wenye viwanda ili kuepuka ujanja uliokuwa ukifanywa na baadhi ya wafanyabiashara, ambao walikuwa wakiagiza sukari kutoka nje ya nchi ambayo nyingine ilikuwa haina ubora.

Hata hivyo, Waziri Mkuu, alisema Tanzania bado kuna uhitaji mkubwa wa sukari hususani ya viwandani, hivyo kusababisha serikali kutoa vibali kwa wamiliki wa viwanda kuagiza sukari kutoka nje ya nchi. "Viwanda vya ndani vya sukari vihakikishe vinaongeza uzalishaji wa sukari ya viwandani ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alisema mahitaji ya sukari kwa mwaka huu nchini yameongezeka hadi kufikia tani 710,000 ikilinganishwa na tani 610,000 za mwaka jana.

Amesema ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa viwanda vipya vinavyotumia sukari ya viwandani, ambapo kwa sasa mahitaji ya sukari ya viwandani yamefikia tani 165,000.

Alisema mahitaji ya sukari za majumbani kwa sasa ni tani 545,000, ambapo kiwanda cha Kilombero kinazalisha tani 134,000, kiwanda cha Manyara tani 6,000, kiwanda cha Mtibwa tani 39,000 na TPC cha Moshi tani 100,000.


Naibu Waziri huyo alisema ili kukabiliana na upungufu wa sukari, serikali imeweka mkakati wa kuanzishwa kwa viwanda vipya vya sukari vya Bagamoro ambacho kitaanza kuingiza awamu ya kwanza ya sukari sokoni tani 35,000 ifikapo mwaka 2022 na kiwanda cha Mkulazi kinatarajiwa kuzalisha tani 200,000 na cha Mbigili tani 50,000.

Akitoa taarifa za kiwanda hicho Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari, Balozi Amry, alisema Kampuni ya Sukari ya Kilombero imezingatia kikamilifu wito wa serikali wa kukuza uzalishaji na kuweka mipango thabiti ya upanuzi wa uzalishaji wa kilimo cha miwa na kiwanda cha kusindika miwa. Mradi huo utagharimu Sh. bilioni 700.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu ametoa wiki mbili kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa awe amechimba visima katika kata ya Ruaha kwa ajili ya kuwawezesha wakazi wa eneo hilo kupata majisafi na salama.

Ameyasema hayo baada ya wakazi wa kata hiyo kusimamisha msafara alipokuwa akielekea kata ya Malolo. Alisema halmashauri hiyo inakusanya zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa mwaka, hivyo inatakiwa kutenga kiasi cha fedha za mapato kugharamia miradi ya maendeleo ya wananchi.

Waziri Mkuu alisema, serikali inatekeleza kampeni ya Rais John Magufuli ya 'kumtua mama ndoo kichwani', ambayo inalenga kuwaondolea wananchi tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa kuhakikisha huduma hiyo inapatikana karibu na maeneo yao.



## Aagiza vikundi wenye ulemavu kupewa mkopo

**Na Woinde Shizza, LONGIDO**

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Joseph Nyamuhanga, ameziagiza halmashauri zote nchini, ambazo bado hazijatekeleza sheria ya kutoa asilimia 10 ya mapoto ya ndani kwa wanawake, vijana na walemavu kutenga fedha hizo na kuzigawa kwenye makundi hayo, kuanzia sasa.

Aliyasema hayo wakati alipotembelea kikundi cha watu wanaoishi na ulemavu cha Tumaini Ushiriki kilichopo wilayani Longido mkoani hapa.

Akiwa Tumaini alijionea mambo mbalimbali yanayofanywa na kikundi hicho ikiwamo unenepesha wa mbuzi kwa ajili ya kuwauza kwa faida.

Nyamuhanga alisema kuwa serikali haitamfumbia macho mkurugenzi yeyote wa halmashauri ambaye atashindwa kutekeleza sheria hiyo ya kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa makundi hayo.

Aidha, alieleza kuwa njia pekee ya kuisaidia serikali ni kuwawezesha wananchi wake kiuchumi kwa kuhahikisha wanapata mikopo hiyo, itakayowainua kiuchumi.

Aliipongeza halmashauri ya Longido kwa kutekeleza sheria hiyo kwani hadi sasa wameshaviwezesha vikundi hivyo, kwa kuwapatia kiasi cha Sh. milioni 50.

Pia alikisifu kikundi hicho, kwa kufanya kazi ya kunenepesha mbuzi kwa ajili ya kuwauza na alisema kazi hiyo itawaongezea kipato mara dufu.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo Katibu wa Chama cha Watu wenye Ulemavu wilayani Longido, ambaye pia ni mwanachama wa kikundi hicho, Emanuel Taraiya, aliishukuru serikali kwa kuwajali, kuwawezesha na kuwaendeleza kwa kuwapa mkopo watu wenye ulemavu.

Aidha, aliiomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kuwapa elimu watu wenye ulemavu ili wasikae ndani badala yake watoke nje na wapaze sauti kutokana na walemavu wengi kutokuwa na elimu ya kutambua haki zao.

Katibu wa Kikundi cha Tumaini, Kitoitoi Ole Ndwati, alisema kuwa kikundi chao kinafanya kazi ya kunenepesha mifugo kwa ajili ya kuiuza katika masoko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.

Alisema kikundi hicho, kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosa masoko, mazingira magumu ya kufanyia kazi, kuwa na mitaji midogo na ushuru wa mifugo kupanda kwa kiasi kikubwa hali inayowafanya kukosa wateja wa kununua mifugo yao.

Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Longido, Grace Mgase, alisema awali walipoanza mpango wa ugawaji wa mikopo hiyo, makundi ya watu wanaoishi na ulemavu yalikuwa yamesahaulika na iliwawia vigumu kupata mikopo hiyo.

Alisema baada ya changamoto hiyo kujitokeza mwanzo waliitatua mapema kwa kuwatafuta na kuwakusanya watu wenye ulemavu na vilipatikana jumla ya vikundi 11 na vyote vilipatiwa mkopo huo.

# Migogoro ya ndoa kikwazo malezi, makuzi ya watoto

**Na Jaliwason Jasson, MANYARA**

MSHAURI wa malezi na makuzi pamoja na maendeleo ya awali ya watoto kutoka Shirika la Children in Crossfire la nchini Ireland ya Kaskazini, amewatahadharisha wanandoa kuwa migogoro ina athari kubwa kwenye malezi ya watoto.

Davis Gisuka, amewatahadharisha wanandoa wenye migogoro kuimaliza kwani inaweza kusababisha madhara kwa watoto wadogo walio na umri wa chini ya miaka mitano.

Tahadhari hiyo, aliitoa wakati akizungumza na mwandishi wa Nipashe kuelezea namna migogoro ya wanandoa inavyoathiri malezi na ukuaji wa watoto wadogo.

Alitoa wito kwa jamii kutatua migogoro ya kifamilia bila ya kusababisha au kuleta madhara kwa watu wengine.

Kwa upande wake wakili wa kujitegemea Nickson Maganya, alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 sura ya 29 imezungumzia namna ya kuwasaidia watoto endapo ikitokea wazazi wakaachana.

Mwanasheria huyo, alisema migogoro hiyo, inapotokea kwa wanandoa, madhara na athari zinazowakuta watoto kwa kukosa malezi ya baba na mama ni kitu ambacho ni muhimu kukiepuka.

"Mtoto anaweza kukosa elimu kutokana na mgogoro ambao husababisha familia kusambaratika hivyo watoto mara nyingi wanajikuta wakiishi katika mazingira magumu na nyakati nyingine wanapelekwa kulelewa na watu ambao hawahitaji kuiishi nao," alisema Muganya.

Aidha, alisema sheria inaeleza kuwa wanandoa wanapotengana mahakama inapaswa kuzingatia maslahi ya watoto ikiwa wana umri chini ya miaka saba.

"Nashauri wanandoa wavumiliane na kuacha tabia zitakazosababisha migogoro kwenye familia zao, kwani kuachana kunatokana na mambo yao binafsi siyo njia ya kutatua tatizo," aliongeza Muganya.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Babati, Mathias Focus, alisema kila robo ya mwaka wa fedha, ofisi yake imekuwa ikipokea migogoro ya ndoa kati ya 20 mpaka 50. Focus alisema, migogoro mingi ya ndoa inatokea kipindi cha njaa kwani wanaume wengi wanazitelekeza familia zao, kutokana na ugumu wa maisha.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema hata kipindi cha msimu wa mavuno ukiwa mzuri migogoro hiyo bado inakuwapo kutokana na baadhi ya wanaume kuvuna mazao, kuyauza na kuoa mke wa pili.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula (wa pili kulia), akipongezwa na mkazi wa Kata ya Komolo, baada ya kuzindua Shule ya Msingi Nadoilchukin juzi, iliyojengwa na kukarabatiwa kwa Sh. milioni 134 na Taasisi ya ECLAT. **PICHA GIFT THADEY**

# Ashauri mfumo elimu ubadilike

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MDAU wa elimu na sheria ameiomba serikali kubadili mfumo wa uendeshaji wa shule za msingi ili uendane na ule wa shule binafsi zinazotumia Kiingereza kama lugha ya mawasiliano ili taasisi hizo ziweze kutoa elimu bora.

Wakili Albert Msando, ambaye ni kada wa Chama Cha Mapinduzi, alitoa rai hiyo, wakati wa mahafali ya 11 ya Shule ya Msingi Yakini, inayotumia Kiingereza kufundishia ,iliyopo Kisongo jijini Arusha.

Alisema kuwa elimu inayotolewa na shule za msingi na sekondari za serikali inatakiwa kuimarishwa ili iendane na ile yenye viwango inayopatikana katika shule binafsi.


"Ni kweli kabisa wala sio jambo la kuonea aibu elimu zetu zinazotolewa kwenye shule za msingi na sekondari za serikali bado zipo chini na ni duni huwezi ukalinganisha na elimu inayotolewa katika shule za watu binafsi," alisema Msando.

Meneja wa Shule ya Msingi Yakini, Christian Kimaro, alisema shule hiyo, ina mafanikio makubwa ya ufaulu kutokana na mpango mkakati waliyojiwekea ya uendeshaji wa shule.

Licha ya kuwa na mafanikio ya kielimu ngazi ya mkoa na wilaya, alisema shule hiyo inakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa maktaba.

Katika mahafali hayo, wadau mbalimbali wakiongozwa na Msando, walichangia zaidi ya Sh. milioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa maktaba.

Jumla ya wanafunzi 76 walihitimu elimu ya msingi na kutunukiwa vyeti na kati yao wapo wanafunzi wanaosomeshwa kwa msaada wa shule hiyo.





# Upatikanaji maji Rombo chini ya asilimia 50

**Na Godfrey Mushi, ROMBO**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitilya Mkumbo, amekiri kuwapo kwa hali mbaya ya upatikanaji wa huduma za maji katika Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro ambayo ni chini ya asilimia 50.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, tayari wizara hiyo imetangaza mpango wake wa kutumia kiasi cha Sh. bilioni 10, ili kunusuru hali hiyo isiendelee kuwaumiza wananchi katika vijiji 40 vyenye hali mbaya zaidi.

Profesa Mkumbo, alikuwa akizungumza jana katika mahojiano maalumu na kituo kimoja cha redio katika Manispaa ya Moshi.

"Bahati mbaya Rombo, kwa Mkoa wa Kilimanjaro ndiyo ambayo ina hali mbaya sana ya upatikanaji wa maji ambayo ni chini ya asilimia 50, ukilinganisha na Siha yenye asilimia 80 na Hai asilimia 80.

"Wizara ya Maji imeliona hili na serikali inakwenda kutekeleza mradi mkubwa sana wa maji ambao utapeleka kwenye vijiji 40 vya Rombo na tunawakabidhi mradi huo Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (Muwsa) watafanya hiyo kazi."

Kwa mujibu wa Prof. Mkumbo kwa kuanzia mwaka huu, wizara hiyo imetenga Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kuanza utekelezaji na katikati ya mwezi Septemba na Oktoba mwaka huu, serikali itakuwa imetangaza zabuni ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika Wilaya ya Rombo.

Hali hiyo inatajwa kutishia ukuaji wa kiuchumi wa vijiji vilivyopo katika Wilaya ya Rombo kutokana na kukosekana kwa huduma ya maji kwa miongo kadhaa sasa.

Nyakati za kiangazi, Wilaya ya Rombo huathiriwa zaidi na uhaba wa maji kutokana na kupungua kwa ujazo kutoka mita za ujazo 27,000 hadi kufikia 18,000.

Taarifa zaidi za serikali, zinaonyesha kuwa mahitaji ya maji wilayani humo ni mita za ujazo zaidi ya 40,000, lakini upatikanaji wa maji ni mita za ujazo 27,000.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (kushoto), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kushoto), walipofanya ziara ya kutembelea jengo la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, kutambua changamoto zinazowakumba watalii wanapowasili. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo. **PICHA: WMU**

# Same yadhibiti ujauzito kwa wanafunzi

**Na Godfrey Mushi, SAME**

TAKWIMU za wanafunzi wa kike katika shule za sekondari za Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro kukatisha masomo yao kutokana na ujauzito, zimeshuka kutoka wastani wa mimba 95 kwa mwaka 2017, hadi kufikia mimba 10 kwa mwezi Juni 2019.

Mwaka 2017, serikali wilayani humo ilikiri kasi ya wanafunzi wa kike kufukuzwa shule kutokana na kupata mimba iliitikisa, baada ya wasichana 100 kufukuzwa, wakiwamo 95 wa sekondari na watano wa shule za msingi.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, jana alitangaza kupata 'ahueni' akisema idara ya elimu imethibitisha rasmi kupungua kwa takwimu za mimba shuleni.

Alikuwa akifunga mafunzo ya rejea kwa walimu na watendaji kutoka shule 19 za Same zilizoanza kama shule za majaribio katika utekelezaji wa mradi huo wa kupambana na mimba za ututoni.

"Kutokana na kuongezeka kwa matukio ya mimba na ukatili wa kijinsia kwa mwaka 2016/2017 katika Wilaya ya Same, naomba nilishukuru sana Shirika la Empower Tanzania ambao walijitokeza kutoa elimu shuleni kwa kushirikiana na serikali. Idara ya elimu wameniletea taarifa ya kupungua kwa takwimu za mimba kutoka 95 kwa mwaka 2017, hadi kufikia 10 Juni 2019," alisema.

Mwaka 2016, wanafunzi zaidi ya 200 walikatisha masomo yao mkoani Kilimanjaro kutokana na ujauzito katika kipindi kisichozidi miezi minane.

Akizungumza kabla ya kufungwa mafunzo hayo, Elibariki Kisimbo ambaye ni Mkurugenzi wa Shirika la Empower Tanzania, alieleza masikitiko yake jinsi mtoto wa kike anavyokosa ulinzi kutokana na matukio mengi ya kikatili kuhusisha watu wa familia zao.

"Mpango huu ni maalum kwa ajili ya kutatua tatizo, kwa sababu elimu tunayoitoa itamfanya binti ajilinde mwenyewe, hata ikitokea mtu anayemwamini amemgeuka. Tunataka mpango huu ufike kwenye shule zote wilayani humu kwa sababu elimu hii inaonyesha mafanikio makubwa," alisisitiza.

Kwa mujibu wa Kisimbo, mimba za utotoni ndiyo adui namba moja anayechangia Same kufanya vibaya kwenye matokeo ya mitihani ya taifa kila mwaka na kujikuta ikiangukia kundi la mkiani.

# Msimamizi uchaguzi Moshi, Vunjo atangazwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MSIMAMIZI mpya wa uchaguzi katika majimbo ya uchaguzi ya Moshi Vijijini na Vunjo, mkoani Kilimanjaro ametangazwa rasmi, baada ya uteuzi wake kuthibitishwa na mamlaka husika nchini, Septemba mwaka huu.

Aliyeikwaa nafasi hiyo muhimu wakati taifa likielekea katika uchaguzi wa serikali za vijiji na mitaa, baadaye mwezi Novemba mwaka huu ni Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Moshi, Juma Tukosa.

Uteuzi huo wa Tukosa ulifanywa na ngazi ya taifa Septemba 9, 2019 na taarifa rasmi zimewasilishwa kwa viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa.

Taarifa iliyopatikana jana na kuthibitishwa na Ofisa Uchaguzi wa wilaya hiyo, Patrick Nyavanga, inaeleza kuwa msimamizi huyo ameanza kazi yake rasmi kwa kutangaza majina na mipaka ya vijiji 157 na vitongoji 700 vitakavyoshiriki uchaguzi huo.

Mei mwaka huu, Mahakama Kuu ya Tanzania ilipiga marufuku wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya nchini kusimamia uchaguzi, baada ya mahakama kufuta sheria iliyokuwa inawapa wakurugenzi hao mamlaka ya kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Uamuzi huo utailazimisha Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuteua watu wake, badala ya kutegemea wateule hao wa Rais, iwapo hautabadilishwa na Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

Katika uamuzi wake, Mahakama Kuu ilisema vifungu 7(1), kinachowapa wakurugenzi mamlaka ya kusimamia uchaguzi na 7(3) vya Sheria ya Uchaguzi vinakwenda kinyume na matakwa ya kikatiba ya uhuru wa Tume ya Uchaguzi.

Kuna taarifa kwamba baada ya kuthibitishwa kuwa msimamizi wa uchaguzi, Tukosa alitangaza majina na mipaka ya maeneo yote yatakayoshiriki uchaguzi wa wenyeviti wa vijiji, wajumbe wa halmashauri za vijiji na wenyeviti wa vitongoji katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi.

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, ina jumla ya vijiji 157, vitongoji 700, kata 32 na majimbo mawili ya uchaguzi.

**Taarifa iliyopatikana jana na kuthibitishwa na Ofisa Uchaguzi wa wilaya hiyo, Patrick Nyavanga, inaeleza kuwa msimamizi huyo ameanza kazi yake rasmi kwa kutangaza majina na mipaka ya vijiji 157 na vitongoji 700 vitakavyoshiriki uchaguzi huo.**

ama
ALHAMISI SEPTEMBA 19, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 16

**Mikwamo kijamii, mazingira duniani yaisukuma UNESCO kugusa kila eneo**



Ukurasa 14

Mamia wanyanyaswa kijinsia vyuo vikuu



Ukurasa 20

**Daktari anayeanza mafunzo kazini anasimulia 'kimbembe' darasa uzazi**



# Maajabu tiba ya Askofu Mkuu Ruaw'ichi kutoka KCMC - MOI

Ukurasa 14

## Mamia wanyanyaswa kijinsia vyuo vikuu

WAKATI ikidai kuwa mstari wa mbele katika haki ya kijinsia ndani ya maisha ya kila siku, kuna malalamiko ya kuwapo mamia ya mabinti Waingereza wasomao katika vyuo vikuu wananyanyaswa, imeelezwa.

Inadaiwa kuwapo walalamikaji 700 wanaonyanyaswa kijinsia na tuhuma zinazohusiana na ngono katika mwaka uliopita wa masomo, sehemu kubwa wakiahidiwa mbadala wa kusaidiwa kimasomo.

Katika vyuo vikuu vya nchini humo vinadai kuwa na madai kama hayo rasmi 11tu katika mwaka wa masomo uliopia na huingizwa katika michakato ya kisheria, ingawa kuna malalamiko upande wa pili, hakuna hatua inayochukuliwa.

Sheria za Uingereza zina miongozo maalum ya namna vyuo vinapaswa kuchukua hatua kuripoti jambo hilo Polisi kwa ajili ya sheria zaidi.

Mwanafunzi anayedai kunyanyaswa kijinsia, anasema, alipofikisha suala lake juu katika sheria, alishangazwa kurudishwa chuoni akakutane na anayemlamu kumnyanyasa, kwa maelekezo kwamba bado kuna fursa ya kuyamaliza chuoni, jambo analodai kumshangaza.

Pia, kuna mwanafunzi wa kike aliyewasilisha malalamiko kwa, alitakiwa kukesha maktaba, baada ya kwenda kulalamika alihofia kurudi bwenini, huenda angevamiwa, kwani alishafanyiwa jambo kama hilo. **BBC**



Wanafunzi wa kike wa chuo kikuu nchini Uingereza. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Maajabu tiba ya Askofu Mkuu Ruaw'ichi kutoka KCMC - MOI

- Yawekwa rekodi ya gharama na ujuzi
- Prof. Kahamba: Mwaka twapokea 100
- Asimulia kinachomsibu, chanzo chake



Rais John Magufuli (wa kwanza kulia), alipomjulia hali Muhashamu Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Askofu Yuda Thadeus Ruwa'ichi (aliyelala kitandani), katika chumba cha uangalizi maalumu. Anayefuata, ni Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface na madaktari mabingwa wa MOI. **PICHA: MARY GEOFREY**

**Na Mary Geofrey**

ITAKUMBUKWA kuwa Agosti 15 mwaka huu, Muhashamu Askofu Yuda Tadeus Ruwa'ichi alitangazwa rasmi kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki, Jimbo Kuu la Dar es Salaam.

Hiyo ni baada ya Muadhama Polycarp Kardinali Pengo, kutangaza kung'atuka madarakani mwaka huu, baada ya kiongozi Mkuu wa Kanisa hilo duniani, Papa Francisko kuridhia ombi lake.

Zikiwa zimetimia siku 27 tangu aanze kutumikia nafasi hiyo ya juu katika Kanisa hilo lililoenea duniani kote, Muadhama Askofu mkuu Ruwa'ichi, alipatwa na maradhi yaliyomfanya alazwe katika Hospitali ya Rufani ya KCMC, mkoani Kilimanjaro.

> **"Tunashukuru hali ya mgonjwa inaendelea vizuri tofauti na kabla hatujamfanyia upasuaji.**

Wakati akiwa katika hospitali hiyo anafanyiwa upasuaji wa kichwa kutibu tatizo lililomsumbua, kukatokea ulazima wa kitaalamu, kutokana na kukwama kiufundi, hali iliyolazimu ahamishiwe katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili(MOI), jijini Dar es Salaam.

### UFAFANUZI KITAALAMU

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa MOI, Prof. Joseph Kahamba, anasema, awali KCMC walimfanyia upasuaji Muhashamu Askofu Mkuu Ruwa'ichi, lakini hali yake iliendelea kuwa mbaya.

Anasema, baada ya kufanyiwa vipimo husika, walibaini kuwapo tatizo lenye uhitaji wa huduma iliyopo MOI kwa ajili ya matibabu zaidi.

Kwa mujibu wa Prof. Kahamba, Muhashamu Askofu Mkuu Ruwa'ichi, alisafirishwa kwa ndege usiku na alipofika MOI, walianza kumfanyia vipimo na kubaini tatizo hilo.

"Ilipofika saa 7:00 usiku tulimuingiza chumba cha upasuaji na ulifanyika hadi saa 10:00 alfajiri chini ya madaktari bingwa wa upasuaji watatu," anaeleza Prof. Kahamba.

Inaelezwa ndege hiyo ilitolewa na Rais Dk. John Magufuli, kufanikisha safari hiyo na mgonjwa kufika MOI usiku wa kuamkia tarehe 10 mwezi huu.

Kwa mujibu wa Profesa Kahamba, iwapo ingetokea hajapata ndege hiyo, angelazimika kukodi kutoka ama Afrika Kusini au Kenya kwa gharama ya Dola za Marekani 300,000 (Sh. milioni 690) kwa ajili ya usafiri na kama mgonjwa angelazimika kwenda kutibiwa nchini Afrika Kusini, angelipa gharama ya kulala kwa siku ni Dola za Marekani 1,000 (Sh.milioni mbili na laki tatu).

"Kama mgonjwa angekaa hospitali kwa siku 10 ina maana angelipa Dola za Marekani 10,000 (Sh. milioni 23 za kitanda) ambazo ni takriban Sh milioni 30, gharama ambazo ni kubwa bila kujumlisha matibabu," anasema na kuingeza:

"Haya ni mafanikio makubwa ambayo MOI tunajivunia kutoa matibabu ambayo awali wagonjwa walikuwa wanayafuata nje ya nchi."

### KINACHOMSIBU, TIBA

Prof. Kahamba anasema, ugonjwa uliompata Muhashamu Askofu Mkuu Ruwa'ichi, siyo kiharusi kama wengi walivyoufananisha, bali ni damu kuvimba kwenye ubongo, ambao kitaalam unaitwa 'Chronic Subdural Haematoma'.

"Tunashukuru hali ya mgonjwa inaendelea vizuri tofauti na kabla hatujamfanyia upasuaji. Alifika hapa usiku wa kuamkia Septemba 10, akitoka Hospitali ya Rufaa ya KCMC mkoani Kilimanjaro," Prof. Kahamba anasema.

### NAMNA WANAVYOMTIBU

Prof. Kahamba anasema wameunda timu ya wataalamu saba wanaomfanyia uchunguzi wa kina katika kuhakikisha afya yake inarejea kama ilivyokuwa awali.

Anataja fani za wataalamu wanaomfanyia uchunguzi Askofu Mkuu ni madaktari bingwa watatu wa magonjwa ya: Ubongo, Dawa za Usingizi na Magonjwa ya ndani.

Pia, kuna wataalamu wanne ni wa masuala ya; chakula na lishe, mazoezi tiba, uchunguzi na uuguzi. Prof. Kahamba anaendelea: "Wataalamu hawa saba wa uchunguzi watafanya kazi hiyo ili kuhakikisha afya ya Askofu inarejea katika hali yake ya kawaida na huwa tunafanya kwa wagonjwa wengine wanaopata tatizo kama hili,"

AFYA

# Maajabu tiba ya Askofu Mkuu Ruaw'ichi kutoka KCMC - MOI



Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Eusebius Nzigilwa, (aliyevaa mavazi meusi), akimjulia hali Muhashamu Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface na wa bingwa wa upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na mishipa ya fahamu wa MOI, Prof. Joseph Kahamba.

### CHANZO NINI?

Prof. Kahamba anasema, sababu za ugonjwa huo hazijulikani, lakini ni tatizo linalowatokea watu wengi mara nyingi, katika mazingira ya vyanzo kama kuumia kichwani, shinikizo kubwa la damu linaloweza kusababisha mishipa ya damu kupasuka.

Lingine analitaja kuwa, matumizi ya dawa zikiwamo za kupunguza maumivu ambazo zinasababisha damu kulainishwa na kuvimbia kichwani.

Prof. Kahamba, anasema mgonjwa asipopata matibabu ya haraka damu, hatari yake damu inaendelea kuvuja kichwani na ujazo wake unapoendelea kuzidi, unachangia mgandamizo kwenye ubongo na athari kuongezeka kusababisha mgonjwa kupoteza maisha.

"Mgonjwa wa namna hii anapaswa kupata matibabu ya haraka iwezekanavyo na mtu akishagundua ugonjwa huu anapaswa kupata matibabu ya dharura," anafafanua Prof. Kahamba.

Anataja dalili ya ugonjwa huo inalingana na upande ambao tatizo linakuwa kwa mtu kichwani. Anataja dalili za jumla ni; kuumwa kichwa, kizunguzungu, dalili za kutapika na kukosa nguvu mkono na mguu mmoja.

### KILICHOKO MOI

Prof. Kahamba anasema, ugonjwa huo wa 'Chronic Subdural Haematoma' gharama za upasuaji nchini ni Sh. milioni nne, lakini kwenda nje ya nchi zinagharimu takriban Sh. milioni 20, ambazo ni wastani usiopungua mara tano ya gharama za sasa.

Aidha, anasema MOI wastani wao wanawafanyia upasuaji wagonjwa wawili kila wiki na takribani 100 kwa mwaka katika mafanikio hali zao kirejea vizuri.

"Ugonjwa kama huu unatibika MOI bila shida na tunafanya upasuaji kwa wagonjwa wengi hadi 100 kwa mwaka na wagonjwa wote wanapona na gharama zetu zote hadi malazi ni ndogo zinafika Sh. milioni nne, kulinganisha na nje ya nchi ambazo zinafika hadi Sh. milioni 20 kwa kila kitu," Prof. Kahamba.

### JPM 'AWAPA TANO'

Saa chache baada ya Muhashamu Askofu Mkuu Ruwa'ichi kufanyiwa upasuaji tarehe 10 ya mwezi huu, Rais Dk. John Magufuli, alimtembelea na kuipa pongezi uongozi wa MOI kwa huduma alizozisifu kuwa 'nzuri.'

Rais Dk. Magufuli anatamka:"Niliongea na Askofu Msaidizi wakati huo wameelezwa na hospitali ya KCMC kwamba ni lazima Askofu Ruwa'ichi apelekwe MOI, palikuwa hakuna usafiri wa kumleta lazima wachukue ndege ya 'ambulance' (ya kubeba wagonjwa) ya kumleta.

"Ndege lazima ukodi Afrika Kusini au Kenya, basi wakati wanahangaika, nikasema madaktari wajiandae nitatuma ndege, ndipo nikatuma ndege haraka haraka ikaenda ikamchukua."

> "Ndege lazima ukodi Afrika Kusini au Kenya, basi wakati wanahangaika, nikasema madaktari wajiandae nitatuma ndege, ndipo nikatuma ndege haraka haraka ikaenda ikamchukua.

Rais Dk. Magufuli, anaungana na kauli kutoka MOI kwamba aina na kiwango cha matibabu ya upasuaji mkubwa MOI inatoa hivi sasa, awali haikupatikani nchini.

Katika kauli na pongezi yake. Dk. Magufuli, anawaambia madaktari na wauguzi wa MOI, kwa anatambua kazi kubwa wanayofanya na amewahidi kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa taasisi hiyo, kwa ajili ya kununua vipandikizi vya wagonjwa wanaopatiwa matibabu hapo.

### MKURUGENZI MOI

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicius Boniface, anamshukuru Rais Dk. Magufuli kwa kutoa fedha hizo na kuhakikisha kuwa zitasaidia katika matibabu ya Watanzania wengine.

Anasema idadi ya viongozi wa serikali wakitanguliwa na Rais Dk. Magufuli walienda kumjulia hali juzi na Mwakilishi wa Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Fancis, ambaye aliendda jana.

Dk. Boniface anawataja wengine ni Balozi wa Vatican nchini, Askofu Mkuu Marek Solczynski, Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Eusebius Nzigilwa na maaskofu wengine.



Muhashamu Askofu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Yuda Thadeus Ruwa'ichi. **PICHA ZOTE: MARY GEOFREY**

Aliahidi kuwashauri ndugu zake kutengeneza kitabu cha watu waliokuja kumuona, ili waandike salamu zao za kumtakia afya njema na kumuombea, ili kupunguza idadi ya wanaoingia wodini.

Mkurugenzi Mtendaji huyo wa MOI, anasema wakati huo alipokuwa katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU), anapaswa kupata muda mzuri wa kupumzika kwa ajili ya kuangalia afya yake na kwamba waliwazuia kumuona, wakihofia pia maambukizi ya magonjwa.

Prof. Kahamba katika rai yake anawataka waumini wa kanisa hilo kuwa watulivu na kumuacha kiongozi huyo apumzike wakati akiendela kupatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa taarifa za MOI, tangu juzi alitolewa kutoka chumba cha uangalizi maalum ana sasa amelazwa katika wodi ya kawaida na anafanyiwa mazoezi ya mwili.

*Makala hii inatokana na taarifa rasmi za MOI za katika mkutano na waandishi wa habari na nyinginezo kuhusu afya ya kiongozi huyo mwandamizi wa kidini.

MAZINGIRA

# Mikwamo kijamii, mazingira duniani yaisukuma UNESCO

• Kumlinda ndege Penguine aishiye barafuni



Ndege aina ya King Penguine, wapatikanao katika ukanda wa barafu, Bara la Antarctica pekee. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

BARAZA Kuu la Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) litakutana kwa wiki mbili kuanzia Novemba 12 hadi 27 mwaka jana, kwa ajili Mkutano wa Kawaida wa 40.

Ni mkutano unaotanguliwa na mingine mikubwa kadhaa ya kimataifa iliyoanzia katikati ya mwaka, ikiwa maandalizi ya mkutano wake mkuu.

Ikiangaliwa ajenda ya mikutano hiyo, inaendana na sekta ambazo UNESCO inasimamia au inafuatilia na kutoa mchango wa uendeshaji wake duniani.

Maeneo kadha tu ndio yaliyoachwa, hata pale mashirika kamili ya Umoja wa Mataifa yanapokuwapo, ajenda zinagusa hapo.

UNESCO kwa jumla ni mkusanyiko, kwani liko Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshulika na Elimu (UNICEF), lililojielekeza zaidi kuwaangalia watoto na kurahisisha kazi ya kuoanisha maeneo yanayoingiliana.

Kwa njia hiyo, mashirika yanayohusika na sayansi, hata utamaduni, ikiunganishwa na maeneo hayo, inaangukia kuwa kazi ya UNESCO.

**Kupitia ramani, maeneo ya Kusini ya bara la Marekani Kusini na Australia, kama barafu na ndege wa aina moja zaidi, Penguin wapo wakiwa na sifa ya kukaa katika barafu.**




Vikao vya UNESCO vikiendelea.

Kwa mfano, katika mambo ya kale ni wazi kuna kuingiliana na elimu (utafiti), halafu sayansi (mbinu za utafiti, maeneo yanayofaa) na utamaduni, kwani yanagusa maisha na kujitambua kwa jamii tofauti. UNESCO ina kazi pana na katika maeneo mengi.

### MIKUTANO ILIVYO

Tangu mwanzo wa mwezi huu, kumekuwapo mikutano kadhaa ya kimataifa ya kuandaa mazingira ya kisaikolojia, baadhi wakiita kujiandaa kiimani baada ya kuelewa kwa undani changamoto zinazoikabili dunia katika wakati uliopo.

Kuna mkutano unaogusa elimu moja kwa moja utakaofanyika Paris, sambamba na Mkutano Mkuu wa Mpango wa Kumbukizi Duniani ambao UNESCO itatoa tuzo za jitihada za kueneza kusoma na kuandika kwa mwaka huu.

Mikutano mingine miwili imefanyika wiki iliyopita, Septemba 3 hadi 5 huko Georgetown, nchini Guyana kuhusu Utamaduni na Chakula: Mikakati Bunifu ya Maendeleo Endelevu; na Kulinganisha Uelewa Kote.

Pia, upo mkutano ulioanza Septemba 3 hadi 6, huko Bishkek, Kyrgyzstan, ambao unahusu mada: Kuhamasisha Ufahamu wa Asili na Njia za Kutatua Matatizo; Kufuatilia Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Udhaifu, nusu ya washiriki wake wanamazingira na wengine wabobezi elimu ya jadi.

Wakati mkutano unaendelea, mwingine utaanza huko jijini Seoul, Korea, unaohusu: Mafunzo ya Maendeleo na Kurekebisha Mipango ya Kiutawala ya UNESCO, kuhusu maeneo ya Kumbukumbu ya Dunia.'

Ni hadhara inayoendana na nyingine jijini Paris, yenye ajenda ya mwaka 2019, ikiitwa Michezo UNESCO na Dukaraha la Malengo ya Maendeleo Endelevu, maarufu "UNESCO Sport and SGDs Fun shop.'

Kuna mkutano wa pili wa Septemba 6, wa kuhabarisha watu kwa jumla na usio na uwakilishi maalum. Ni kwamba, unawakusanya watafiti na washauri wa elimu na hifadhi ya kumbukizi duniani, wakati huo huo jijini Paris.

Suala la kueneza kusoma na kuandika, inaelekea linapewa kipaumbele katika mikutano tangulizi ya UNESCO, hasa matukio ya jijini Paris.

Nje ya mikutano hiyo, ipo Siku ya Kimataifa ya Kusomesha (International Literacy Day) Septemba 9, katika makao makuu ya UNESCO.

Kingine ni mradi wa UNESCO wa Maktaba ya Digitali ya Wazi kuhusu michezo ya jadi. Yote inaelezwa kuwa sehemu ya juhudi za asasi hiyo kufikia amani duniani, kwa kujenga uhusiano wa karibu na ushirikiano kati ya mataifa.

Mkutano Mkuu wa Mwaka ni wa Kamati ya Kimataifa ya Maeneo ya Hifadhi ya UNESCO, uliofanyika Baku nchini Azerbeijan, mnamo Juni 30 hadi Julai 10 iliyopita.

Tanzania ilishiriki katika nafasi ya mjumbe wa kamati hiyo, ikiungana na Uganda kwa upande wa nchi zaAfrika Mashariki, Angola na Zimbabwe kwa nchi wanachama za SADC, wakiungana na wajumbe kutoka Afrika kwa jumla; Tunisia na Burkina Faso.

Wananchi, pia walihudhuria hadhara tano ambazo ni sehemu ya mkutano huo, mmoja ukiwa wataalamu vijana wa masuala ya kutunza maeneo ya kumbukumbu. China ilipangwa kuwa mwenyeji wa mkutano wa kamati hiyo mwaka ujao.

Inaelezwa, tangu mkutano wa mwaka jana, maeneo mawili ya kitamaduni yameongezwa katika orodha ya maeneo kumbukizi yanayosimamiwa na UNESCO, pamoja na maeneo sita kitamaduni katika orodha hiyo. Zote ziko katika mpangilio tofauti, saba ni ya kitamaduni.

Wakati taarifa hiyo inatolewa Julai 5, UNESCO ilishaongeza maeneo matano ya kutunzwa kama hifadhi ya kumbukumbu; mawili ya kimaumbile nchini Ufaransa na Iceland.

Maeneo mengine ni nchi za Brazil, Burkina Faso na Irak, ambako kamati iliridhia kupanuliwa eneo la hifadhi kumbukumbu, lililounganisha nchi mbili za Albania na Macedonia ya Kaskazini, yaani kusini ya Bara la Ulaya.

Ikifafanua kuhusu nyongeza hizo, taarifa ya ukurasa wa UNESCO katika mtandao ilisema kuwa maeneo ya 'French Austral Lands and Seas' (Nchi za Kusini na Bahari za Ufaransa) ambao ziko katika bahari ya Kusini (inavyoitwa na wataalamu kwa inaunganisha bahari za Atlantiki, Hindi na Pacific zisizokaliwa na watu) ni maalum sana.

Anasema, maeneo hayo yana miinuko isiyo ya kawaida Kusini ya Bahari ya Hindi, ikiwa mikusanyiko mitatu ya visiwa pamoja na visiwa 60 vidogo vinavyopakana na baridi kali la Antarctic.

### VIUMBE ADIMU

Shirika hilo linasema, eneo hilo kwa jumla linachukua hekta milioni 67 lenye ndege na wanyama wanyonyeshao baharini wengi, kuliko eneo jingine duniani.

**Nje ya mikutano hiyo, ipo Siku ya Kimataifa ya Kusomesha (International Literacy Day) Septemba 9, katika makao makuu ya UNESCO.**

Wingi wa ndege wa aina ya King Penguins na 'Yellow nosed albatross' ni wa kipekee katika dunia, huku umbali wake kutoka eneo lenye makazi ya binadamu zinayapa hifadhi ya kipekee na kutoa mwanga wa mtiririko wa mabadiliko ya maumbile ya ndege hao. Ni eneo maalum kwa kufanya utafiti wa kisayansi.

### MAENEO PEKEE

Mtu anapofuatilia maeneo mengine yaliyoingizwa katika orodha ya hifadhi kumbukizi chini ya UNESCO, anapata picha pana na isiyojulikana sana duniani, kulinganisha na uhalisia.

Kupitia ramani, maeneo ya Kusini ya bara Marekani Kusini na Australia, kama barafu na ndege wa aina moja zaidi, Penguin wapo wakiwa na sifa ya kukaa katika barafu.

Hazina ya kimaumbile, ilikuwa inafahamika kwa wataalamu zaidi, hivyo utalii wa nyanda za baridi baharini itabaki kuwa tatizo.

# Msongo wakati wa ujauzito huishia maradhi ya akili

**Na Mwandishi Wetu**

WATAFITI wa Uingereza wamefanya kazi yao na kubaini msongo wa mawazo unapokithiri kwa mjamzito, unajenga nafasi kubwa ya mtoto atakayezaliwa awe mwenye matatizo ya akili.

Kwa mujibu wa utafiti huo, matatizo hayo ya akili kwa mtoto uwezekano wake unajitokeza katika umri kabla ya mzaliwa kutimiza umri wa miaka 30.

Wataalamu wanafafanua kwamba, msongo wa mawazo kwa mama unapokuwa katika kiwango cha juu kupindukia, basi uwezekano wa matatizo yake kiafya yanahama taratibu katika maisha ya mtoto atakayezaliwa baadaye.

Ni utafiti uliofanyika kwa wajawazito 3,600 nchini Finland wakifutalia matokeo ya afya ya kali ya watoto wao. Katika ufuatiliaji huo yaliyoangaliwa yanajumuisha mambo kama hali mbaya ya fedha.

Jarida la Utafiti la Afya ya Akili ay Uingereza, inasema sehemu kubwa ya waliohusishwa katika utafiti huo, ni kinamama waliozaliwa mpaka katika zama za kati ya mwaka 1975 na 1976.

Hata hivyo, haijawa bayana kama matatizo hayo ya akili yanatokana na ama watoto kurithi kupitia njia ya vinasaba au matatizo ya ubongo kuathirika kwa jumla.

Kimsingi, ni mtazamo ulioweka kando athari kama historia ya mama kama aliwahi kuvuta sigara na kumrithisha mtoto na historia nyinginezo za kurithishana kupitia ubongo.

Dk. Trudi Seneviratne,



Mjamzito katika maisha ya msongo. **PICHA : MTANDAO**

mtaaluma kutoka kitivo cha chuo kikuu kinachosimamia taaluma ya akili, anaeleza: "Kama msongo haujakamilishwa, kuna nafasi kubwa ya kusambaa baadaye, hivyo ni jambo nyeti la kuzungumzia"

"Hatutaki wazazi wasifikiri tu kwamba wanawaharibu watoto, lakini kiwango kikubwa cha msongo kinatuathiri," anasema Dk. Seneviratne.

Kuhusu namna msongo wa mawazo unapunguzwa kwa mtu katika kipindi hicho cha uzazi, ni kwamba mjamzito anapaswa kuungwa mkono katika kipindi chote na kupewa mbinu za kukabili matatizo yake.

"Wanahitaji kupumzika, kuomba ushirikiano na kuongea na yule ambaye anahisi anafaa kuwasiliana naye," anasema mtaalamu huyo, akisisitiza umuhimu wa mlo kamili na kulala, huku marufuku kubwa ikiwa katika uvutaji sigara.

Mtaalamu mwingine, Ross Brannigan, kutoka chuo kiitwacho Royal College of Surgeons kilichoko Ireland, anasema:"Somo hili linatuangazia umuhimu wa kusaidia matatizo ya afya ya akili kwa kinamama na familia."

Anasema, katika matibabu ya akili ni jambo muhimu sana tabibu au msaidizi wake kudadisi kama mhusika aliwahi kuugua maradhi ya kichwa au la, katika historia yake ya maisha, kwani ina tafsiri kubwa katika hilo.

AFYA

# Mamilioni waliohamia mbadala kielektroniki, madhara kwao pa

• Misiba tata yaibua maswali yanayoelea • Bangi na zajitokeza kivingine • Wataalamu wakali wakihoji ya

Na Michael Eneza

***"...Walitumia sigara mtandao zenye 'nicotine' (kiungo cha kawaida cha sigara)...baadhi wanasema walitumia sigara mtandao yenye kemikali inayoitwa THC ambayo ina 'marijuana' (bangi laini zinazouzwa Marekani) kuweza kuwapatia hisia za ulevi au 'nishai'.... hadi wiki moja iliyopita inaripotiwa mbali na vifo vya 12, zaidi ya watu 450 walishapata madhara makubwa katika mapafu..."***



Mhusika akivuta sigara ya kieketroniki. **PICHA: MTANDAO.**

KUNA jipya nchini Marekani ambalo sasa ni 'habari ya mjini' kuhusu kuongezeka vifo vya vijana wanaoshiriki mchezo wa ulevi mpya kimtandao.

Suala ni kwamba, mtu anazoea sigara yenye aina fulani ya unyevu. Hiyo inaitwa sigara ya kielektronikia au maarufu 'e -cigarette'

Hicho ni kifaa mithili ya sigara iliyowekewa mvuke na mvutaji anatumia kama vile sigara ya kawaida kwa mbwembwe na burudani nyinginezo ya uvutaji, lakini kamwe haina uhusiano na tumbaku.

Tendo la kutumia sigara hiyo na kupumua 'moshi wa mvuke unamfanya mvutaji afaidi, kana kwamba anavuta na sigara hizo ziko za aina nyingi, mithili ya sigara za kawaida na kiko, utengenezaji wake ukipitia mitindo na awamu mbalimbali kuligana na wakati.

Ni hali iliyochangia kupatiwa jina 'vaping' kwa maana ya kutumia kitu chenye mvuke (vapor). Bado inaelekea ni nchini Marekani, ulevi huo ndiko ulikoshika kasi zaidi na vifo tayari vimeshari- potiwa vingi.

### WATAALAMU WABISHA

Bado kuna mjadala wa kitaalamu kama sigara hizo zisizo na vimelea vya nikotini, ambavyo vinapatikana katika tumbaku na vina athari kiafya au la.

Jambo pekee lililo bayana ni kwamba hadi sasa inajulikana pamoja na manufaa yake kumnusuru mvutaji kumuweka mbali na athari za kuacha sigara, hailinganishwi na kuacha kabisa.

Shaka nyingine inayoanikwa kitaalamu ni kwamba, vijana wanaotumia sigara hiyo bandia, wako katika nafasi kubwa ya kutumbukia katika matumizi ya sigara ya kawaida.

Mamlaka ya Chakula na Dawa Nchini Marekani (UF DAS), iko katika msimamo wake kwamba mbadala huo wa nikotini (tumbaku) ambayo ni 'e- cigarette' ni salama zaidi.

### MAONI WATAALAMU

Wakati baadhi ya wataalamu wa afya wanataka sigara hizo na kupatikana kwake katika mtandao kupigwe marufuku kuna wanaosema jitihada kama hiyo ya kuepeneza sigara za kielektroniki itazaa madhara zaidi, badala ya ahueni inayotarajiwa.

> **Dai ni kwamba, ingebidi sigara hizo zikaguliwe kwa kina na Mamlaka ya Chakula na Dawa ipate kibali kabla ya kuingizwa sokoni kuuziwa mteja mmoja mmoja.**

Jarida linaloheshimika la uchumi la kila wiki nchini Uingereza, The Economist lina maoni ya wachumi Marekani, wanakosoa sera za utawala wa Rais Donald Trump, kupunguza hatua au hitaji la kuthibitishwa kwa bidhaa, kabla ya kuwekwa sokoni.

Dai ni kwamba, ingebidi sigara hizo zikaguliwe kwa kina na Mamlaka ya Chakula na Dawa ipate kibali kabla ya kuingizwa sokoni kuuziwa mteja mmoja mmoja.

Hiyo ni baada ya watu sita kuripotiwa kufariki kutokana na kuvuta sigara oevu za kimtandao. Maofisa wa afya katika majimbo tofauti ya Marekani, walianza kutoa sauti zao kuwa 'ku-vepa'kukomeshwe.

### VIFO VYAMEA

Hadi wiki moja iliyopita, inaripotiwa mbali na vifo vya 12, zaidi ya watu 450 walishapata madhara makubwa katika mapafu. Baadhi ya wataalamu walikuwa na shaka kuhusu wakiegemea wazo la ulazima wa kupigwa marufuku bidhaa hiyo inayomea.

Moja ya sababu kubwa ni mtandao mpana wa wavutaji sigara oevu sasa wamefikia wastani wa milioni 11 hivi. Taasisi ya Udhibiti wa Maradhi na Chama cha Madaktari Marekani, kwa pamoja walitoa mwito wavuta 'vepa' hao milioni 11 kuacha, wakiwaambia ni hatari kuliko kuvuta

Utawala wa Rais Trump, ulitamka Septemba 11 iliyopita kuwa unataka kupiga marufuku kimiminika hicho ambacho si cha tumbaku, lakini wapo ambao kupitia vyombo vya habari hawaridhishwi na hoja hiyo, wakiwa kinyume katika wanachokiita 'kutetea uhuru.'

Mtaalamu mmoja akichangia uchambuzi katika jarida la Uingereza, anasema dondoo muhimu za suala hilo zinaachwa pembeni kwani inapotokea hatari kwa afya watu wengi, mihemko inachukua nafasi ya uchambuzi wa kina, kuangalia hali halisi ilivyo.

Anatoa tahadhari kuwa bado utafiti wa ziada unahitajika, kwani ushahidi uliopo unaonyesha kuwa vifo vinavyohusishwa na 'kuvepa' nchini Marekani, havikutokana na bidhaa zilizouzwa dukani, ila kutokana na vitu vilivyotengenezwa bila umakini na kuuzwa baraba-




Hizi nd sigara kielekr za nam mbalim

# sigara alepale

## tumbaku a Trump





lizo
za
oniki
na
bali.



Mwanamama akivuta sigara ya kieketroniki.



Sigara ya kieletrokiki na kawaida.

rani.

Msomi huyo katika hoja yake, anadai vifo vitano kati ya sita vilivyohusishwa na kimiminika kilichotumika kilinunuliwa kienyeji, wakati kifo kimoja kilitokana na kimiminika kilichonunuliwa katika duka lililosajiliwa la bidhaa za jamii ya tumbaku (cannabis), jimboni Oregon.

Anasema, kuna nadharia inayoelezea athari mbaya za kimiminika husika kilichanganywa na Vitamini E, akifafanua ni mafuta na hayatakiwi kabisa kuingia katika mapafu. Anasema mtu anayevuta mafuta yanamletea madhara kama hayo ya 'wavepaji.'

Taasisi ya Kuzuia Maradhi, inasisitiza katika taarifa kuwa yake kuwa bidhaa za kuokotwa barabarani ndizo zinazua hatari kubwa, siyo kwa 'wavepaji' peke yao, hata wanunuzi wa 'bangi' za mitaani katika maduka yasiyosajiliwa.

Hivyo, watengenezaji bidhaa za 'kuvepa' wanatakiwa kuboresha bidhaa na mahitaji yao yamtandao, yenye ladha, katika juhudi za kukabiliana na magonjwa ya mapafu yanayohusishwa na 'kuvepa.'

Zaidi ya majimbo 25 nchini Marekani kati ya takriban 50 wameeleza kushtushwa na hali ya magonjwa ya mapafu yanayohusishwa na 'kuvepa' kudhihirisha kuwa tatizo ni kubwa na linaenea.

> **Katika vita ya kutetea usalama wa mazingira naye ameku-wa mstari wa mbele, katika moja ya ho-tuba zake ak-iwashambu-lia Wapagani wa Bara la Ulaya kuwa wanachangia uharibifu wa mazingira.**

Jarida la Uingereza lilitofautiana na taasisi hiyo ya Marekani katika mapendekezo yake, likitahadharisha kuwa watu wanaojali afya zao wasiguse kabisa sigara 'oevu' za mtandaoni, bali watafute ushauri wa daktari wanapojitahidi kuacha kuvuta sigara za kawaida.

Taasisi hiyo inasisitiza kuwa sigara za mtandaoni zisitumiwe na vijana wadogo wanaofikia umri wa kuwa wakubwa kisheria, mama wajawazito na watu wazima ambao hawatumii bidhaa za tumbaku.

Asasi hizo zinawaasa hasa vijana kuwa mtumiaji sigara oevu za mtandaoni, achunge afya yake kwa kuangalia dalili za magonjwa, kwa mfano kukohoa, kukosa hewa, maumivu kifuani na ikibidi atafute ushauri haraka kutoka kwa wataalamu wa afya.

Idadi ya wenye matatizo makubwa ya kupumua sasa ilishafikia 2,156 katika majimbo 25 na kuanzia mwisho wa Juni iliyopita, wengi wamelazwa hospitalini wakiwa na matatizo ya mapafu yanayoonekana kuwa sugu.

Hao ni wanaoelezwa kuwa wanahitaji msaada wa mashine wapumue na kuangaliwa kwa karibu hali zao, hivyo sifa zao ni kuwa katika chumba cha uangalizi maalumu hospitalini (ICU).

### VIFO JE?

Mishtuko ilienea baada ya kuwapo taarifa za mwanamke mwenye umri miaka 30 hivi karibuni alikufa jimboni Illinois, alipoanza 'kuvepa.'

Maofisa wa afya wanaeleza kusubiri vielelezo kuhusu sumu mwilini mwake na uchunguzi wa aina tofauti, kutambua kilichomsibu hadi kifo.

Baadhi ya waathirika wanasema, walitumia sigara mtandao yenye kemikali inayoitwa THC ambayo ina 'marijuana' (bangi laini zinazouzwa Marekani) kuweza kuwapatia hisia za ulevi au 'nishai.'

Baadhi ya madaktari walifuatilia matukio ya magonjwa hayo, wanasema kuwa mafuta ya bangi ambayo yamegandishwa kuwa na unyevu kujazwa kwa kifaa katika 'flash' yanaweza kusababisha kuungua mapafu.

Waathirika wengine waliohojiwa wanasema, walitumia sigara mtandao zenye 'nicotine' (kiungo cha kawaida cha sigara) na katika matukio mengi zaidi, waathirika walielezea kuongezeka polepole viashiria vya athari hasi.

Hapo ina maana ya kupumua kwa tabu na maumivu kifuani kabla ya kulazwa hospitalini, kupata chanzo cha pamoja, bado ilikuwa ngumu.

Baadhi ya wataalamu walikuwa wanajiuliza kama kuna magonjwa tofauti mwenye viashiria vinavyofanana, huku mtaalamu wa The Economist aking'ang'ania kuwa ufahamu uliopo kuhusu kemikali za sigara mtandao bado ni mdogo licha ya kuwa hazina 'lami' (mgando) na visabishi vingine vya saratani katika bidhaa jadi za tumbaku.

Ila mtaalamu anakubali 'kuvepa' kuna changamoto za wazi, kwani ili kuweza kupulizwa nikotini ya kawaida au THC, lazima mtu ichanganywe na vimimino vinayoyeyusha na hivyo 'kuopoa' kinachotakiwa kuvuta, au kilevi kinachotakiwa.

Kiongozi wa zamani wa Mamlaka ya Chakula na Dawa, Dk. Scott Gottlieb, anasema baadhi ya kemikali hatari zinahusiana na vimelea vya bangi au THC.

'Inaelekea ni kitu kipya kilichoingiwa sokoni na kiwanda kisichosajiliwa, kisababishi ladha kipya au njia mpya ya kuyeyusha THC ndiyo inaleta maumivu haya.' Mamlaka hiyo ilisema inafanya mchanganuo wa sampuli 80 za waathirika.

### VINASABA VYABOMOKA

Katika hatua nyingine wataalamu wa Kimarekani wamefanya utafiti na kugundua kwamba matumizi ya sigara za elektroniki yanakaribisha janga la kubomoa vinasaba vya mtumiaji na kukaribisha maradhi, ikiwamo moyo, mapafu na kansa.

Inaelezwa, uvutaji wa sigara hizo unaleta hatari ya tabu kiafya zaidi katika maeneo kama mapafu na utumbo, kuliko hata kwa namna ilivyo, kwa anayetumia sigara za kawaida. Timu ya madaktari mabingwa wa Marekani, ikiongozwa na daktari Moon-shong Tang, kutoka Shule ya Tiba ya Chuo Kikuu cha New York, anasema ni aina ya sigara inayoweka hatarini zaidi afya ya mtumiaji.

Kupitia ripoti yao inayopatikana katika Jarida la kitaaluma la kisayansi, wanasema uvutaji sigara hiyo ya kielektroniki inasababisha zaidi kansa ya utumbo na magonjwa ya moyo.

Madaktari hao walipozamisha ujuzi wao kulinganisha athari za mtumiaji sigara kielektroniki na namna ilivyo karibu na kansa, katika namna ileile alivyo mtumiaji sigara za kawaida, afya inadhurika katika namna inayofanana.

Watafiti wanasema, wakati hali ni hiyo, utumiaji wa sigara hizo uko juu kwa vijana wadogo wanaojihisi wako mbali na kudhurika, kutokana uhalisia wa umri walio nao

"Pia, ni muhimu kufahamu kwamba watumiaji wa sigara za kielektroniki wanaichukulia kama tabia na si mbadala kuacha sigara za tumbaku, wako katika mtazamo wa jumla kwamba 'e -cigarette' ni salama," wanaeleza wasomi hao.

Wakati ripoti ya kiserikali ikionyesha kuwapo wavutaji milioni 11, wasomi hao kupitia utafiti wanabashiri wapo milioni 18 nchini Marekani na kati yao asilimia 16, (million 28.8) ni wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

***Makala hii imeandaliwa kwa mujibu wa mitandao na taarifa mbalimbali za kitaalamu.***

AFYA

KINARA WA MASOMO CUBA...

# Daktari anayeanza mafunzo kazini asimulia 'kimbembe' darasa uzazi

• Afunguka ilivyo 'bifu' lake na ushirikina

**Na Beatrice Moses**

***JUMAMOSI iliyopita gazeti hili lilibeba makala hii sehemu ya kwanza, simulizi mwanamke kijana wa Kitanzania aliyekuwa mwanafunzi bora katika kozi ya udaktari tiba ya binadamu chuoni kwake. Endelea kumfuatilia, kuhusu dira yake katika taaluma anayoianza.***

IRENE Mageni ni mhitimu wa masomo ya udaktari nchini Cuba, ambaye amefanikiwa kuwa miongoni mwa wachache waliotunukiwa tuzo hivyo kuweka historia nzuri. Alikuwa mwanafunzi bora chuoni kwake.

Ukimuona ni mrembo hasa, katika tafsiri rasmi ya urembo, lakini ndani yake ana faida ya ziada kuwa ni daktari wa kutibu binadamu.

Ana mwezi mmoja tangu arejee nchini, akiwa kwenye mchakato wa kukamilisha taratibu za kutambulika nchini, kushiriki kwenye mafunzo ya vitendo kwa mwaka mmoja.

Dk. Irene baada ya kutimiza ndoto yake, tayari kuna mambo kadhaa ambayo amekusudia kuhakikisha kuwa anashirikiana kikamilifu na watangulizi wake, katika kuisaidia jamii akiamini ataweza.

Anabainisha kuwa, imani ya kishirikina ni miongoni mwa mambo yanayowatesa baadhi ya wanajamii, kuumia kiafya na hata kisaikolojia.

Daktari huyo mwanamke kijana, anaamini wapo watu kadhaa wamepoteza maisha kwa magonjwa, ilhali wangewahi kwenda hospitali, wangepata matibabu sahihi na pengine yangewasaidia kuendelea kuishi.

Dk. Irene anaeleza kuwa amebaini kuwapo watu wanaochelewa kwenda hospitali kutibiwa kila wanapougua. Imani katika hilo ni kwamba, wanabweteka katika dhana kuwa wamelogwa.

Hivyo, wanaamua kuzunguka kwa waganga wa jadi, licha ya magonjwa wanayougua yana tiba hivyo wangewahi kwenda kufanyiwa vipimo sahihi ili watibiwe ipasavyo.

"Baada ya kumaliza masomo yangu nakusudia kuitatumia elimu niliyoipata vyema, ikiwamo kuelimisha baadhi ya wanajamii kuacha kuamini masuala ya ushirikina na badala yake watambua umuhimu wa kupata tiba sahihi,' anasema daktari huyo.

Pia, anafafanua kuwa, magonjwa mbalimbali ambayo yamekuwa yakihusishwa na imani za kishirikina, anayataja kuwa ni kifafa, malaria na shinikizo la damu.

### UJUZI WAKE?

Anaeleza imani yake kuwa ameiva katika fani ya utabibu, kutokana na mafunzo ya vitendo aliyopata,



Dk Irene Mageni, akiwa na Waziri wa Afya Cuba. Dk José Ángel Portal Miranda, kwenye mahafali aliyotunukiwa tuzo ya Mwanafunzi Bora Mgeni, katika chuo cha Latin American School of Medicine, nchini Cuba. **NA MPIGAPICHA WETU**

> **Hata hivyo, siku niliposhuhudia mjamzito anajifungua kwa njia ya kawaida, nilikumbwa na hali ya ajabu tofauti na mengine. Nilijikuta nashikwa na woga hadi machozi yalinitoka.**

ambayo kwa upande wake alikuwa akiyafanya kwa moyo wa ushujaa ikiwamo upasuaji mjamzito.

" Hata hivyo, siku niliposhuhudia mjamzito anajifungua kwa njia ya kawaida, nilikumbwa na hali ya ajabu tofauti na mengine. Nilijikuta nashikwa na woga hadi machozi yalinitoka," anasema Dk. Irene.

Anaeleza kadri alivyokuwa anashiriki mafunzo hayo, ndivyo alijikuta anapata ujasiri, kiasi cha kufikia kushiriki kusaidia mjamzito kujifungua kwa njia ya kawaida, aliyoihofia awali.

Daktari huyo anasema, haikuwa kazi rahisi kwake kutimiza ndoto yake, kwani kuna mambo alikutana nayo yaliyomtia woga, lakini hakukata tamaa kwa kuwa wazazi wake walijenga katika dhana ya kutovunjika moyo na kujitambua.

Matokeo hayo mazuri aliyoyapata katika Latin American School of Medicine, anabainisha anaamini yatakuwa chachu itakayowavutia wanafunzi wengine hasa wa kike kusoma kwa bidii, nao watimize ndoto zao.

### ALIKOTOKEA

Irene, elimu yake ya msingi aliipata katika shule ya Gangilonga mjini Iringa na kisha akahamia katika Shule ya Msingi, Karakata, Dar es Salaam, kabla ya kurejeshwa tena mjini Iringa kwenye Shule ya Msingi Lugalo, alikohitimu darasa la saba.

Baada ya hapo, alijiunga na Shule Sekondari ya St. Francis jijini Mbeya, alikomaliza kidato cha nne na akajiunga na kidato cha tano na sita, katika shule ya Marian Girls iliyoko Bagamoyo, alikohitimu mwaka 2012 na akapata nafasi ya kwenda nchini Cuba kusomea udaktari wa binadamu.

Wahenga wanasema 'usione vyaelea jua vimeundwa.' Ndivyo ilivyo kwa Dk Irene, ambaye ni zao la kutimiza ndoto kutokana na ushirikiano mzuri aliopata kutoka kwa wazazi wake.

Mama mzazi wa Irene, Dorothy Magese, anayejitambulisha ni mhitimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Rugambwa, iliyoko mjini Bukoba, anaeleza hisia yake ya furaha kuona mtoto wake ametimiza ndoto ya kuwa daktari na kuongeza idadi ya madaktari wanawake.

"Wazazi jukumu letu kuhakikisha tunawapa moyo watoto wetu kwa kuhakikisha tunawawezesha, tunawashauri ili kuwasaidia kufanikisha kupata elimu ili waweze kutimiza ndoto za kufanya kazi za wanazozipenda, kwa kuwa watakuwa wanafanya kazi hizo kwa bidii hivyo kutakuwa na mafanikio kwa nchi na jamii," anasema

### SERA YA AFYA

Juhudi mbalimbali zinafanywa na serikali, taasisi binafsi na wataalam wa afya kuelimisha jamii kutambua umuhimu wa kupata matibabu mapema, badala ya kujichelewesha kwa kukibilia wenda kuagua kwa waganga wa jadi ambao wengi wanatajwa kuwa ni wadanganyifu na wachumia tumbo.

Sera ya Afya ya Mwaka 2007, inaeleza kuwa elimu ya afya na uhamasishaji ni njia mojawapo katika utoaji wa huduma za afya.

"Njia hii inatumia utaalamu wa mawasiliano na kutayarisha na kuwasilisha ujumbe mbalimbali kwa mtu binafsi, familia na jamii kwa lengo la kubadilisha mienendo na tabia zinazochangia kuwapo au kutokuwapo kwa maradhi katika jamii," inaeleza.

Kwa mujibu wa sera hiyo, mbinu mbalimbali ikiwamo ya kutumia vyombo vya habari, mabango, vipeperushi, majarida, vitabu na wavuti hutumika kushawishi na kuwasilisha ujumbe huo.

Sera hiyo inaeleza kuwa katika utekelezaji wa elimu ya afya na uhamasishaji, serikali imefanikiwa kutoa elimu ya afya kwa wananchi pamoja na kuwahamasisha namna ya kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Magonjwa mengi yamedhibitiwa, hasa yale yanayoweza kuzuilika kwa chanjo.

"Hata hivyo, elimu ya afya inayotolewa bado haijaleta mabadiliko makubwa ya tabia na mienendo inayotarajiwa katika jamii," inaelezwa.

Mambo kadhaa yanatajwa, ikiwamo mazingira yaliyopo kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa hayatoshelezi kila mtu kuweza kukuza, kulinda na kuendeleza afya yake.

Kunaorodheshwa madhumuni makuu ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kumuwezesha kila mtu kulinda na kuendeleza afya yake kwa ufanisi.

Tamko linalotolewa kwenye sera hiyo, ni kwamba serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaimarisha utoaji elimu ya afya, ili kumhamasisha na kumuwezesha kila mtu kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya na maisha bora.

Pia, inaelezwa serikali kwa kushirikiana na wadau, itaandaa sheria, miongozo na mikakati itakayowezesha kila mtu kupata elimu, ili kulinda, kukuza na kuendeleza afya bora.



## HABARI MBEYA

## Mil. 7/- zatengwa kununua taulo za kike

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

BAADHI ya wadau wanaotetea ustawi na maendeleo ya watoto wa kike wameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa kutenga Sh. milioni 7.5 katika mwaka wa fedha 2019/ 2020 za ununuzi wa taulo za kike.

Walisifu hatua hiyo kuwa itapunguza utoro na kuongeza ufaulu kwa wasichana.

Wakizungumza juzi wakati wa kikao cha uchambuzi wa bajeti kilichoandaliwa na Mtandao wa Jinsia TGNP na kuwahusisha viongozi wa vituo vya taarifa na maarifa pamoja na viongozi wa halmashauri walisema hatua hiyo ni muhimu katika kumwezesha mtoto wa kike kusoma kwa utulivu.

Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, alisema uamuzi wa kuweka bajeti ya Sh. milioni 7.5 kwa ajili ya ununuzi wa taulo za kike ulichagizwa na ushawishi wa kutoka TGNP-Mtandao ambao ulitoa hoja mbalimbali zinazoeleza faida ya kuwanunulia watoto wa kike pedi.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imekuwa ya mfano nchini kutenga bajeti ya ununuzi wa pedi ambapo kwa mara ya kwanza mwaka 2017/2018 walitenga Sh. milioni moja, mwaka 2018/2019, Sh. milioni tano na sasa Sh. milioni 7.5

"Sisi vituo vya taarifa vya maarifa kama sehemu ya mtandao wa jinsia Tanzania tunajivunia kuwa sehemu ya kuwezesha watoto wa kike kusoma kwenye mazingira ya utulivu, tunaipongeza halmashauri kwa kutambua adha wanazozipata watoto wa kike na kuona haja ya kutenga bajeti kwa ajili ya kuwasaidia pedi," alisema Mlowezi.

Ofisa Programu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia, Zainab Mmari, alisema hatua hiyo ni muhimu kwa mtoto wa kike kwani itachagiza ufaulu wa masomo na kupunguza utoro ukilinganisha na hali ilivyo sasa.

Alisema katika tathmini zao miongoni mwa sababu zinazosababisha watoto wa kike kufanya vibaya kwenye masomo yao inatokana na suala la hedhi kwani kipindi hicho humfanya mtoto kushindwa kuzingatia masomo kutokana na hali hiyo na mbaya zaidi wengine hushindwa hata kumudu gharama za kununua pedi kwa sababu ya umaskini kwenye familia zao. Mmari alisema TGNP-Mtandao wataendelea kufanya kazi kwa karibu na Wilaya ya Mbeya kwa sababu imeonyesha mwitikio kwa masuala mbalimbali yahusuyo jinsia ikiwamo sekta ya elimu, afya, kilimo na maji.

Kaimu Mkurugenzi wa Wilaya ya Mbeya ambaye ni Ofisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji, Gidion Mapunda, alisema katika mwaka wa fedha 2018/2019 shule 16 zikiwamo za msingi na sekondari ziligawiwa pedi.

Alifafanua kuwa jumla ya shule 4,720 za msingi na sekondari wanafunzi wake walinufaika na pedi hizo wakiwamo wanafunzi wa Sekondari za Iwiji, Imezu, Itala, Ilunga, Teule na msingi ni Mshewe, Chang'ombe na Nsongwi juu.

# Jiji lajipanga kuwa mji wa kisasa Afrika

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

JIJI la Mbeya wakati wowote litaanza kutekeleza mpango kabambe wa maboresho unaotarajiwa kulifanya kuwa miongoni mwa miji ya kisasa barani Afrika ifikapo mwaka 2039.

Katika mpango huo, jiji litapangwa na kufanya marekebisho ya kasoro za matumizi ya ardhi, na kwamba Mbeya haijawahi kuwa na mipango miji kwa muda wa miaka 15 baada ya uliokuwa unatumika awali kufikia ukomo mwaka 2004, hali iliyosababisha wananchi kujenga makazi holela na kuingilia hata maeneo ya wazi.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Ardhi wa Jiji, Esau Pwele, alisema mpango kabambe unaandaliwa na kampuni ya kizalendo kwa gharama ya Sh. milioni 900, ndiyo dira itakayotumika.

Alisema utekelezaji wa mpango huo unashirikisha wadau mbalimbali wa mkoa huo wakiwamo wananchi, madiwani na taasisi mbalimbali za serikali zinazotoa huduma kwa jamii na kwamba kwa sasa wapo kwenye hatua ya kutathmini mwonekano wa sasa wa jiji na wadau kutoa mapendekezo ya namna wanavyotaka mji uwe.

"Tulikuwa hatuna master plan tangu mwaka 2004 baada ya ule wa awali kufikia mwisho. Kutokana na changamoto ya uchumi, lakini hata hivyo ilikuwapo miradi mingine iliyokuwa inaendelea ndiyo maana makazi yako holela," alisema Pwele. Wakati wa utekelezaji wa mpango huo huenda baadhi ya nyumba za wananchi zitabomolewa ili kuupanga vizuri mji ikiwa ni pamoja na kunyoosha na kupanua miundombinu ya barabara ili kila eneo liwe linafikika.

Alisisitiza kuwa katika mpango huo kuna baadhi ya maeneo yatatakiwa yabaki kama yalivyo kama sehemu za wazi, bustani na hata sehemu za kilimo ili kuliacha jiji katika uhalisia wake wa kijani (green city).

Alisema kazi hiyo inafadhiliwa na Benki ya Dunia (WB), kupitia mradi wa uendelezaji wa miji ya kimkakati na kwamba mipango miji itakuwa suluhisho la makazi holela.

Aidha, alisema mbali na mradi huo, jiji linaendelea na mradi wa upimaji viwanja katika eneo la Iziwa chini ya Mbeya Peak Project kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 600 ambazo ni mkopo usio na riba kutoka katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Alisema katika mradi huo vimepatikana viwanja 500 kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama makazi, biashara, makazi na biashara pamoja na huduma za kijamii kama shule na hospitali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, akitoa maelezo yake aliwatahadharisha waliojenga kwenye maeneo ya wazi kujiandaa kisaikolojia kwa maelezo kuwa maeneo yao yanaainishwa.

Alisema baada ya kuyaainisha operesheni maalumu ya kubomoa nyumba hizo bila kujali hadhi wala mmiliki itaanza ili maeneo hayo yabaki kwa ajili ya shughuli zilizokusudiwa.



Baadhi ya wanachama wapya wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mbeya Vijijini, waliohamia kutoka vyama vya upinzani wakiapishwa wilayani humo mkoani Mbeya juzi, kwa kusoma Ilani ya CCM, wakiongozwa na viongozi wa chama hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vigogo, wanachama 190 upinzani watimkia CCM

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

VIGOGO wakiwamo wanachama wa Chadema na wa ACT-Wazalendo takriban 190, katika Wilaya ya Mbeya Vijijini wamemtimkia CCM.

Baada ya kujiunga na Chama Cha Mapinduzi wageni hao walipokelewa na viongozi wa chama hicho wilayani akiwamo mbunge wa jimbo hilo, Oran Njeza.

Baadhi ya vigogo waliopokelewa ni pamoja na aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Chadema, Elia Kaolile na Katibu wa chama cha ACT- Wazalendo wa wilaya hiyo, Izrael Mamba.

Akizungumza baada ya kupokelewa, Kaolile alisema aliamua kuihama Chadema baada ya kubaini kuwa viongozi wake hawautambui mchango aliokuwa anautoa ndani ya chama hicho ikiwamo kukijenga kuanzia ngazi ya chini pamoja na kuwapigania wagombea.

Alijigamba kuwa alikuwa ni dhahabu ndani ya Chadema, lakini viongozi wa chama hicho walikuwa hawatambui umuhimu wake na kwamba sasa wataanza kuuona baada ya kukihama chama.

"Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiamini kuwa wanaohama vyama vya upinzani na kujiunga na CCM wananunuliwa, huo ni uongo na upotoshaji wa hali ya juu, mimi nimeamua mwenyewe kuondoka ili nisaidiane vizuri na wenzangu kuleta maendeleo kwa wananchi," alisema Kaolile.

Alisema kabla hajahama aliwatanguliza watoto wake ambao tayari walishajiunga na CCM na baadaye akaamua kuhama kuungana na familia yake.

Naye aliyekuwa Katibu wa ACT- Wazalendo, Mamba alisema aliamua kujiunga na CCM ili kumuunga mkono Rais John Magufuli, kwenye maendeleo anayofanya katika maeneo mbalimbali nchini ikiwamo barabara, viwanja vya ndege, reli na vituo vya afya.

Alisema kwa sasa hakuna sababu ya kuwa mpinzani kwa madai kuwa mambo yote waliyokuwa wanayapinga, Rais Magufuli kwa kushirikiana na wasaidizi wake ameshayarekebisha.

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Njeza alisema mbali na watu hao waliopokelewa, pia wapo wengine zaidi ya 100 ambao ni viongozi wakubwa wa Chadema ambao wameomba kujiunga na chama hicho na taratibu zitaendelea kufanyika ndani ya CCM ili nao wapokelewe.

Alisema kwa muda mrefu alikuwa anashirikiana na Kaolile kwenye shughuli za maendeleo bila kujali tofauti za itikadi zao za kisiasa ikiwamo kushughulikia changamoto za maji katika Mji wa Mbalizi pamoja na miundombinu ya barabara.





# Nakala za mikataba ya ajira changamoto

Na Augusta Njoji, DODOMA

IMEELEZWA wafanyakazi wa kampuni za kibiashara nchini wanakabiliwa na changamoto ya kutopewa nakala za mikataba ya ajira hali inayosababisha kushindwa kujua haki zao za msingi.

Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2017 iliyotolewa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu(LHRC), asilimia 74 ya wafanyakazi wana mikataba, lakini baadhi hawapewi nakala huku asilimia 26 hawana kabisa mikataba.

Hayo yalielezwa na mtoa mada, Paul Ngongoti kutoka LHRC alipokuwa akiwasilisha mada ya dhana ya haki za binadamu na biashara na hali halisi ilivyo nchini, katika mjadala wa kitaifa juu ya haki za binadamu na biashara.

Alisema maeneo ambayo yameonekana kuwa na matatizo katika utekelezaji wa masuala ya haki za binadamu na biashara kuwa ni maeneo ya makazini, ardhi, mazingira na masuala ya kodi.

"Utoaji wa mikataba imeimarika, lakini wengi hawapewi nakala za mikataba, wengine mikataba haikidhi vigezo na hasa kwenye kampuni hizi za Kichina zina changamoto sana," alisema.

Aidha, alisema asilimia 95 ya wafanyakazi wanaondoka kazini baada ya muda wa kazi, huku asilimia tano wao wakishindwa kuondoka baada ya muda huo.

Kuhusu mafunzo ya afya mahala pa kazi, Ngongoti alisema asilimia 55 ya wafanyakazi wamepewa mafunzo hayo huku asilimia 45 wakiwa hawana elimu hiyo, pia elimu ya sheria ya kazi wanaojua ni asilimia 23 huku asilimia 77 wana uelewa mdogo na wengine hawana kabisa.

Akizungumzia suala la fidia ya ardhi inayochukuliwa kwa ajili ya uwekezaji, mtoa mada huyo alisema asilimia 42 ya wananchi hawana uhakika na fidia inayolipwa, huku asilimia 64 wanadai kuwa wawekezaji wamekuwa hawaruhusu maeneo yao kutumiwa na wananchi.

Kuhusu ulipaji kodi, Ngongoti alisema asilimia 41 ya waajiri walisema kodi ni kubwa na ndio sababu inayowasababisha wakwepe.

Alisema kampuni hizo zina wajibu mkubwa wa kulinda na kusimamia haki za binadamu katika maeneo yake kwa kujibu wa matakwa ya kidunia masuala ya haki za binadamu na biashara ambayo yamewekewa utaratibu ili kutosababisha athari zozote za kibinadamu.

"Suala la kulinda haki za binadamu haliepukiki, hata kampuni inapokuja kufanya kazi Tanzania lazima ifuate huo utaratibu wa kidunia," alisema.

" Mfano mzuri ni kwenye kampuni za simu ambazo zinataarifa zote za wateja, hivyo kampuni zinatakiwa kutekeleza haki ya binadamu ya usiri wa taarifa zake."

Alisema ili kampuni iweze kutekeleza masuala ya haki za binadamu, kampuni zinatakiwa kuwa na miongozo ya ndani ya kulinda haki za wafanyakazi.

# Wasambazaji, wazalishaji pembejeo waililia serikali

Na Renatha Msungu, DODOMA

MWENYEKITI wa Chama cha Ushirika cha Wazalishaji na Wasambazaji wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo (TADCOS LTD), Gerald Mlenge, ameiomba serikali kuingilia kati changamoto zinazowakabili wasambaaji na wauzaji wa pembejeo.

Changamoto hizo ni gharama za mafunzo za wasambazaji na wauzaji wa pembejeo za kilimo na mifugo (Agrodillers) wastani wa Sh. 350,000 hadi 450,000.

Ombi hilo lilitolewa hivi karibuni jijini hapa wakati wa kongamano la kitaifa la wauzaji na wasambazaji wa pembejeo za kilimo Tanzania, ambao wanashindwa kuendelea kutokana na gharama hizo na nyingine za kibali cha Sh. 170,000.

"Kuna vitu vingi ambavyo matokeo yake huyu mtu anayeenda kuuza viuatilifu, atakwama kwenda kupeleka kwa wananchi au wakulima kwa sababu hana uwezo mzuri kutokana na kukwepa kwenda kupata mafunzo kutokana na gharama kubwa ya mafunzo," alisema Mlenge.

Aidha, alisema kuwa dawa hizo kwao ni biashara hali inayosababisha kwenda kuuza na kutoa maelekezo yaliyo chini ya kiwango ambapo madhara yake ni makubwa sana ikiwamo kuharibu mimea ya watu, mifugo na hata yeye mwenyewe.

"Kama mtu haijui mbegu vizuri inafanyaje kazi na inatunzwaje, hajui mbolea inahifadhiwaje ili isipoteze ubora, mtu huyo kwenda kujifunza unamwambia alipe fedha nyingi wakati anaisaidia serikali kumfanya mkulima aweze kufanya vizuri zaidi," alisema Mlenge.

Mwenyekiti huyo alitaja changamoto inayowakumba wakulima ni pamoja na kuwa na bei kubwa ya mbolea na mbegu kwani pakti moja ya mbegu ya kilo mbili inauzwa Sh. 10,000 hadi 12,000.

Mkulima kutoka katika kijiji cha Blambila, Kata ya Mwalukwa Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Rogers Donald, alisema wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea hali ambayo imekuwa ikiwapa wakati mgumu kuweza kufanikiwa.

"Naishauri serikali ipite katika maeneo ya vijijini ichukue aina ya udongo, tujue tunatakiwa kulima mazao ya aina gani hii itatusaidia tuweze kulima kilimo chenye tija na kuacha kukata tamaa katika mavuno," alisema Donald.

Akifungua kongamano hilo, Kaimu Naibu Mrajisi Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, (TCDC), Charles Malunde, alisema ili Tanzania iwe na kilimo chenye tija ni muhimu wasambazaji wa pembejeo za kilimo kusambaza mbegu bora na kuacha kuwasambazia mbegu feki.

"Ninaimani kuwa uwapo wenu kwenye kongamano hili litaleta tija kwani hapo zamani wakulima walikuwa wakiuziwa mbegu zisizokuwa na ubora na kusababisha kipato chao kushuka," alisema Malunde.



Ofisa Tarafa ya Chilonwa wilayani Chamwino, Mohamed Mfaki, akizungumza na wanawake wa kijiji cha Kawawa, Kata ya Msanga mkoani Dodoma jana, alipokuwa akihamasisha umuhimu wa kujiunga na mpango wa mfuko wa bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa. PICHA: PETER MKWAVILA

# Watakiwa kuhamasisha wananchi kujiunga CHF

Na Peter Mkwavila, CHAMWINO

WATENDAJI wa kata na vijiji wametakiwa kuunda kamati zitakazohamasisha wananchi kujiunga na mpango wa Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (CHF) ili kuondokana na gharama za matibabu.

Wito huo ulitolewa jana na Ofisa Tarafa ya Chilonwa Wilaya ya Chamwino, Mohamed Mfaki, alipokuwa akihamasisha umuhimu wa kujiunga na mfuko huo kwa wananchi wa wilaya hiyo.

Alisema viongozi hao wana wajibu kuhakikisha bima hiyo inamfikia kila mwananchi na awe amejiandikisha kama ilivyoagizwa na serikali.

"Agizo hili kwenu nyinyi maofisa watendaji ni la siku 30, hivyo hakikisheni wananchi mnaowasimamia kwenye kata zenu ambao hawajajiunga na mfuko huu wa bima ya afya ya (CHF) iliyoboreshwa wanajiunga," alisema.

Alisema serikali inataka kuona wananchi wake wanapata huduma za kiafya bila kikwazo chochote.

Kwa upande wao, wananchi waliomba serikali kutoa elimu zaidi itakayowashawishi kuona umuhimu wa bima hiyo.

Mkazi wa Kijiji cha Bwawani, Feibo Ndahani, alisema kuwa changamoto kubwa iliyopo kwa wakazi wa vijijini ya kutojiunga na bima hiyo ni ukosefu wa elimu ya kutosha.

"Serikali itoe wataalamu ambao wataelimisha wananchi kutoka ngazi ya vitongoji hadi kwenye kata, ili zoezi hili lifanikishe kwa kuwa ni muhimu, na kuhakikisha kuna upatikanaji wa dawa kwa kipindi cha mwaka mzima," alisema.

Naye Mkazi wa Msanga, Janet Nyamayausi, aliwataka wanawake kuchangamkia fursa hiyo muhimu kwao kutokana na wao ndio wahitaji wakubwa wa huduma za afya.



# Uchaguzi 2020

## Vikosi vya usalama kupiga kura siku moja kabla

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), imeeleza kuwa kwa mara ya kwanza vikosi vya ulinzi na usalama vitapiga kura mapema siku moja kabla ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka 2020.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous, alisema kuwa kura hiyo itawahusisha vikosi vya ulinzi na usalama pamoja na watendaji wa tume hiyo, ili wawezesha kutekeleza majukumu yao siku ya uchaguzi mkuu.

Aliyasema hayo wakati akifunguwa mafunzo ya siku tatu kwa wanahabari kuhusu kuandika habari za uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na mtandao wa asasi za kiraia wa kuangalia uchaguzi Tanzania ( Tacceo) kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanahabari za Maendeleo Zanzibar (Wahamaza).

Idarous alisema hatua hiyo ya kura ya mapema imetokana na marekebisho ya Sheria ya ZEC NO.4 ya Mwaka 2018 ambayo inatoa nafasi kwa makundi hayo.

Alisema marekebisho hayo yamekuja baada ya kubainika kwamba wapiganaji wa vikosi vya ulinzi hawaitumii haki yao ya kidemokrasia kupiga kura na kuwachagua viongozi kutokana na kutingwa na majukumu ya kazi siku hiyo ya kupiga kura.

"Marekebisho hayo sasa yatawapa nafasi baadhi ya watendaji waliokabidhiwa majukumu muhimu kupiga kura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika," alisema.

Aidha, alisema kazi kubwa inayokusudiwa kufanywa na Tume ya Uchaguzi ni kuanza kwa kazi ya maandalizi ya kuandikisha wapiga kura wapya katika uchaguzi mkuu ujao pamoja na kufanya uhakiki katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Alisema kazi hizo ni muhimu kufanyika kabla ya uchaguzi mkuu kwa sababu huwezi kupiga kura bila ya kusajiliwa katika daftari la kudumu la wapigakura.

"Tunakusudia kuanza kuandikisha wapigakura wapya wenye sifa kwa ajili ya uchaguzi mkuu pamoja na kulihakiki daftari la kudumu la wapigakura na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa ikiwamo waliokufa," alisema.

Mwenyekiti wa asasi ya kiraia ya Tacceo, Martina Kabisama, aliwataka waandishi wa habari kuzingatia na kufuata maadili ili kuhakikisha wanaelimisha jamii vizuri katika kipindi cha uchaguzi.

Aliwataka waandishi wa habari kuwahamasisha wananchi kwenda kupiga kura siku ya uchaguzi ili kutumia haki yao ya demokrasia kwa sababu baadhi ya wananchi hawapigi kura na kukosa haki yao hiyo, wakati wana sifa zote za kupiga kura.

"Msiwakatishe tamaa wananchi wajengeeni ushujaa na kuwashajihisha waende kupiga kura ili kuwa na demokrasia iliyokomaa. Waandishi wa habari mna nguvu ya kubadili maisha ya watu," alisema Kabisama. Aidha, alisema kipindi cha uchaguzi mkuu jamii inahitaji kupewa taarifa sahihi ambazo hazitakuwa na mwelekeo wa kuhatarisha na kuvunja amani.

"Tunaelekea katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 na watu ambao watafanya kazi kubwa ya kutoa taarifa za uchaguzi huo ni ninyi wanahabari, ambapo mnatakiwa kuandika na kutoa taarifa zilizokamilika zenye kujenga na sio kubomoa taifa," alisema.

# SMZ yajivunia mafanikio SADC

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imejifunza mambo mengi yenye manufaa katika mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Nchi Wanachama wa Ushirikiano wa Maendeleo (SADC), uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Wizara ya Biashara na Viwanda, pamoja na mkutano huo, pia imenufaika na maadhimisho na maonyesho ya nne ya wiki ya viwanda ya nchi wanachama wa SADC.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri Hassan Khamis Hafidh, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu suali aliloulizwa na mwakilishi wa Jimbo la Mpendae Mohammed Said, aliyetaka kujua ni faida gani zilizopatikana katika kuhakikisha viwanda na bidhaa za Zanzibar zinapata masoko mapya katika nchi wanachama wa SADC.

Naibu Waziri, alisema miongoni mwa faida zilizopatikana ni kuanzisha mahusiano ya kibiashara kati ya wazalishaji wa viwanda kutoka Zanzibar na wanachama wa SADC.

Alisema pia Zanzibar imepata masoko mapya ya bidhaa ambayo yatawezesha kuinua uchumi wa wafanyabiashara na taifa kwa ujumla.

Naibu Waziri alieleza kuwa pia wameweza kujifunza namna ya kuhifadhi bidhaa na umuhimu wa vifungashio katika kuuza bidhaa katika soko la kimataifa la ukanda wa Kusini mwa Afrika.

"Faida nyingine ni kupata fedha kutokana na mauzo ya bidhaa za wajasiriamali katika wiki ya maadhimisho na maonyesho," aliongeza.

Aidha, akijibu swali lingine la ziada lililoulizwa na mwakilishi huyo, aliyetaka kujua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejifunza nini katika mkutano huo mkubwa na wa kihistoria katika kuharakisha shughuli za maendeleo, Naibu Waziri Hafidh, alisema:

"Serikali imejifunza ushirikishwaji wa sekta binafsi katika masuala ya kimaendeleo, kuongeza nguvu katika sekta ya kilimo na kuziongezea thamani bidhaa kwa maendeleo ya kiuchumi na viwanda."



Wakazi wa Kijiji cha Seka Musoma Vijijini mkoani Mara, wakikinga maji juzi, katika moja ya mabomba yaliyowekwa na mwekezaji na kuwapunguzia usumbufu wa kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo kwenye Ziwa Victoria. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wizara yakerwa watoto kufeli

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imeeleza kutoridhishwa na matokeo ya mtihani ya kidato cha pili na dasara la sita ya wanafunzi wa mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja.

Kutokana na hali hiyo, wizara imefuatilia na kubaini kwamba kuna sababu mbalimbali zinazopelekea hali hiyo ikiwamo utoro kwa wanafunzi.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Muhammed Said, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa nafasi za wanawake Hidaya Ali Makame.

Makame alitaka kujua wizara imejipanga vipi kuhakikisha kwamba wanafunzi hawafeli katika miaka ijayo.

Saidi, alitaja sababu nyingine iliyopelekea wanafunzi kufeli kwa mikoa hiyo ni ushirikiano duni baina ya wazazi na walimu kufuatilia na kusimamia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

"Pia ajira katika umri mdogo, uhaba wa walimu wenye sifa hasa wa sayansi na hisabati ni changamoto zinazopelekea hali hiyo," alisema Said.

Aidha, alisema upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwamo vifaa vya sayansi na kemikali ni sababu inayochangia wanafunzi kufeli kutokana na kukosa kusoma kwa vitendo na badala yake husoma kwa nadharia.

Simai alieleza kuwa katika kuhakikisha kwamba matokeo ya shule zilizomo katika mikoa hiyo yanaimarika wizara yake imekuchukua hatua mbalimbali kama kupeleka vifaa vya kufundishia na kujifunza, vingine kwa ajili ya maabara, kompyuta na vitabu. "Pia tumewajengea uwezo walimu 650 wa masomo ya sanaa na wenye uwezo wa kufundisha masomo ya sayansi, hisabati na Kiingereza," alisema Naibu Waziri.

Aliahidi kuwa wizara hiyo inatarajia kukutana na kamati za shule katika mikoa hiyo kujadili na kuzitatua changamoto zilizopo katika jamii zao likiwamo suala la utoro, ajira za ututoni na hali duni ya kushirikiana baina ya walimu, wazazi na jamii katika maendeleo ya wanafunzi.

Alisema pia wataimarisha ukaguzi wa mara kwa mara katika mikoa hiyo ili kubaini upungufu katika ufundishaji na kuyafanyia kazi mambo yatakayoonekana yana changamoto.

# Balozi Ndobho alivyoenziwa

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa MUSOMA**

WAKAZI wa Kata ya Ifulifu, Musoma Vijijini mkoani Mara, wamependekeza sekondari inayojengwa katika kijiji cha Kabegi ipewe jina la Balozi Paul James Casmir Ndobho.

Lengo la kufanya hivyo ni kutambua mchango wake kwa maendeleo na ustawi wa taifa, Mkoa wa Mara, Wilaya ya Musoma, kata na vijiji vyote 68 vya Jimbo la Musoma Vijijini.

Balozi Ndobho alifariki dunia Septemba 9, mwaka huu na kuzikwa Jumamosi iliyopita, mjini Musoma, ambapo waombolezaji wakajulishwa hatua hiyo kuipa shule hiyo jina la 'James Ndobho Secondary School'.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma, ndiye aliyesema hayo na kufafanua kuwa hilo limefanyika kwa ajili ya kutunza kumbukumbu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

"Wanavijiji wa Jimbo la Musoma Vijijini wameamua kuwatambua na kuwaenzi ndugu zao, wenye mchango kwa maendeleo na ustawi wa taifa letu, mkoa wetu, wilaya yetu, kata zetu na vijiji vyetu," alisema Magoma.

Paul James Casmir Ndobho alizaliwa katika kijiji cha Murunyigo, Kata ya Ifulifu na alifanya kazi mbalimbali na kwenye ngazi mbalimbali, ikiwamo Mbunge wa Musoma Vijijini kuanzia mwaka 1965 hadi 1970.

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na Balozi wa Tanzania nchini Urusi na nchi za Ulaya Mashariki (USSR na Eastern Europe) na nchini Kongo (DRC, iliyojulikana kama Zaire).

Katika uchaguzi wa ndani ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1995, Balozi Ndobho alijitosa kuwania ubunge wa Musoma Vijijini kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi na kufanikiwa kutwaa jimbo hilo.

Baada ya kumaliza kipindi cha miaka mitano cha ubunge, aliamua kurudi katika Chama Cha Mapinduzi (CCM), hadi mauti yalipomkuta, alikuwa ni mwanachama wa chama hicho tawala.

Kuanzia mwaka jana hadi sasa, Balozi Ndobho anakuwa mtu wa pili kuenziwa jimboni humo baada ya Jaji Dan Mapigano ambaye jina lake limetumika kwa sekondari mpya inayojengwa katika Kata ya Bugoji.

Shule hiyo inayotarajiwa kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka ujao wa 2020, inaitwa Dan Mapigano Memorial Secondary School ikiwa ni kwa ajili ya kumuenzi jaji huyo.

**Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma, ndiye aliyesema hayo na kufafanua kuwa hilo limefanyika kwa ajili ya kutunza kumbukumbu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.**

# Wananchi wahofia vyandarua kupunguza nguvu za kiume

**Na Happy Severine, MASWA**

WANANCHI wilayani Maswa mkoani Simiyu, wameeleza hofu yao kubwa ya kuendelea kutumia vyandarua vinavyosaidia kuzuia na kujikinga na maambukizi dhidi ya malaria, kwa madai kuwa vinapunguza nguvu za kiume.

Pia wamesema kuwa vyandarua hivyo vimekuwa vikieneza na kuzalisha wadudu aina ya kunguni ambao huwasababishia homa kali.

Hayo yameelezwa jana na wahudumu wa afya ngazi ya jamii walipokuwa wakipokea vifaa vya kazi ambavyo vitawasaidia kurahisisha utendaji, vilivyotolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Kawiye Social Development Fund (KASODEFO) chini ya ufadhili wa Tanzania Marketing and Communication (TMarc) Mjini Maswa.

Wahudumu hao walisema asilimia kubwa ya jamii ya watu wa wilaya hiyo, bado ina mitazamo hasi juu ya matumizi ya vyandarua, hali inayosababisha wengi wao kukataa kuvitumia wakihofia kuingiliwa na kunguni na kupoteza nguvu za kiume.

Mhudumu wa afya ngazi ya jamii kutoka Kata ya Busilili wilayani Maswa, Mary Emmanuel, alisema licha ya kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria mkoani Simiyu, bado kuwa jamii ina uelewa mdogo dhidi ya ugonjwa huo, hivyo kupitia vifaa zikiwamo baiskeli vilivyotolewa vitawasaidia kurahisisha katika kutoa elimu sahihi kila kijiji.

Mratibu wa malaria Mkoa wa Simiyu, Dk. Mugune Maheka, alisema ugonjwa wa malaria umepungua mkoani humo na kufikia asilimia sita na kubaini kuwa uelewa wa wananchi bado upo chini, huku matarajio ya mkoa yakiwa ni kumaliza kabisa tatizo hilo.

Alisema mkoa huo una mpango wa kuweka viuadudu kwenye maji yaliyotuama ili kuzuia mazalia ya mbu ambayo husababisha ugonjwa huo.

Pia alitoa wito kwa jamii kuacha dhana potofu dhidi ya dawa hizo na matumizi ya vyandarua kuwa yanasababisha kupunguza nguvu za kiume, hivyo kueleza kuwa hazina madhara yoyote kwa binadamu na zipo kwa ajili ya kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.

Mratibu wa Kasodefo, Marius Isavika, alisema jamii imeweza kufikiwa kupitia matamasha, mikutano ya hadhara, matembezi ya nyumba kwa nyumba, mazungumzo ya mtu mmoja na mmoja na majadiliano ya vikundi ambapo wanalenga kuzifikia kata 87 za Wilaya za Itilima, Maswa na Meatu ili kukabiliana na kuutokomeza ugonjwa huo.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe (kushoto), akipata maelezo kutoka Mkurugenzi wa Veridoc Global, Alex Mhagama, wakati alipotembelea banda la kampuni hiyo, katika Mkutano wa 39 wa Makatibu Wakuu (Tehama) wa Nchi Wanachama wa SADC, unaoendelea jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mikakati kumaliza dosari soko nyama nje yasukwa

**Na Mariam Magili**

SERIKALI imesema inaendelea na mikakati ya kukabiliana na changamoto za soko la nyama nje ya nchi ili kuwapatia wafugaji fursa ya kufanya biashara hiyo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliyasema hayo jana kwenye ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani Kagera.

Katika ziara yake hiyo, Ulega alitembelea ranchi za Kikulula na Mabale na kuzungumza na wawekezaji katika ranchi hizo kisha kufanya mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Katanda, Kata ya Kihanga wilayani Karagwe.

Naibu waziri huyo aliwataka wawekezaji walioko katika maeneo hayo kueleza changamoto ambazo zinazowakwamisha kusafirisha nyama nje ya nchi.

"Ranchi ya Kikulula lazima iendelezwe na kuwa ya mfano kwa kuwekewa mikakati mbalimbali ili iweze kuwa na tija kwa mfugaji na taifa kwa ujumla," alisema. Aliwataka wawekezaji kuendelea vitalu vyao kwa kuweka miundombinu imara bila kuwa na hofu ya uwapo wa mkataba wa muda mfupi ya mwaka mmoja.

Prof. Phillemon Wambura, Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (Narco), aliwataka wawekezaji kufuata sheria katika kumiliki vitalu ili kuepuka migogoro ya ardhi.

Baada ya kumaliza ziara yake, Ulega alikutana na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ambaye aliiomba Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuboresha zaidi sekta hiyo ili wafanyabiashara wanufaike.

Baadhi ya changamoto zinazoikwamisha Tanzania kuuza nyama nje ya mipaka yake ni magonjwa wa ngozi, unenepeshaji kufanyika kwa mifugo umri mkubwa na kutokuwa na machinjio mengi ya kisasa.

## HABARI KIMATAIFA

# Netanyahu hali tete matokeo uchaguzi

**YERUSALEM, Israel**

RIPOTI ya awali kuhusu matokeo ya uchaguzi mkuu nchini Israel zinaonyesha Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu ameendelea kukabana koo na mpinzani wake mkubwa, Jenerali mstaafu Benny Grantz.

Vyombo vya habari nchini Israel vimeripoti kwamba chama cha Netanyahu mrengo wa kulia cha Likud na kile cha Bluu na Nyeupe cha mpinzani wake, Grantz kila kimoja kimepata viti 32 kati ya viti 120 vya bunge baada ya takribani asilimia 90 ya kura kuhesabiwa.

Ripoti hizo zilinukuu duru kutoka Tume ya Uchaguzi Israel kwani kiwango hicho cha matokeo kilikuwa hakijachapishwa rasmi na hakikutarajiwa kutolewa kabla ya jana alasiri.

Matokeo ya awali katika uchaguzi wa Israel kwa kawaida huwa si ya uhakika na huku matokeo rasmi yakitarajiwa kutolewa muda wowote.

Huenda Netanyahu akapata ushindi, ingawa vituo vyote vitatu vimeonyesha matokeo sawa.

Kwa matokeo hayo, pande zote zitatakiwa kuunda serikali itakayojumuisha vyama vingine bungeni hali inayoibua uwezekano wa mazungumzo kuelekea kuundwa kwa serikali ya umoja.

Iwapo matokeo hayo ya awali yatabakia hivyo hadi mwisho, itakuwa ni pigo kubwa kwa Netanyahu, aliyekuwa na matarajio ya kuunda serikali ya muungano wa vyama vya mrengo wa kulia, sawasawa na ule uliopo sasa, huku akikabiliwa na uwezekano wa kufunguliwa mashtaka ya ufisadi wiki chache zijazo.

Kwenye mkutano na wafuasi wa chama chake baada ya uchaguzi mjini Tel Aviv jana usiku, Netanyahu aliashiria kwamba tayari amejiandaa kwa makubaliano magumu ya kuunda serikali ijayo ya muungano ya Israel, huku akisisitiza umuhimu wa Israel kuwa na serikali imara itakayoutetea kwa nguvu zote Uyahudi.

Alisema, bado anasubiri matokeo rasmi akisisitiza kwamba Israel iko njia panda kihistoria, lakini ikiwa na fursa pana pamoja na changamoto kubwa katika siku za usoni.

Dalili zinaonyesha kuwa hakuna mgombea yoyote anayeweza kupata idadi kubwa ya wabunge kati ya Netanyahu na Gantz bila uungaji mkono wa Avigdor Lieberman aliyekuwa Waziri wa Ulinzi wa Netanyahu.

Lieberman aliibuka kama mshindi wa kweli, kwani kuna uwezekano mkubwa kwamba ndiye atakayeamua juu ya atakayejumuishwa katika serikali ijayo. Chama chake cha Yisrael Beitenu kimepata viti tisa.

Baada ya matokeo hayo ya awali, Lieberman alitoa wito wa serikali ya muungano wa chama chake, Likud na Bluu na Nyeupe akisema taifa hilo linakabiliwa na hali ya dharura.

Huu ni uchaguzi wa pili katika kipindi cha miezi mitano nchini humo na Rais Reuven Rivlin ambaye anatakiwa kuchagua mtu wa kuunda serikali ijayo akisema, ni lazima wajizuie kufanya uchaguzi mwingine.

*DW*

## Bunge lawaita mkurugenzi, mhandisi kutoa ushahidi

**WASHINGTON, Marekani**

MWENYEKITI wa Kamati ya Usafiri na Miundombinu bungeni Marekani, Peter DeFazio, amewaita Mkurugenzi wa Shirika la Boeing, Dennis Muilenburg na Mkuu wa Uhandisi, John Hamilton wa kitengo cha biashara cha Boeing kufika bungeni kutoa ushahidi Oktoba 30, 2019.

Kamati ya usafiri na miundombinu katika bunge la Marekani juzi ilimtaka mkurugenzi huyo kutoa ushahidi juu ya ndege aina ya 737 MAX ambayo hivi sasa imezuiliwa kusafiri kutokana na ajali mbili zilizosababisha vifo vya watu 346 tangu Oktoba mwaka jana.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni mbunge, Peter DeFazio pia alimtaka John Hamilton Mkuu wa uhandisi katika kitengo cha biashara cha Boeing kufika bungeni kutoa ushahidi wake. Wawili hao wanatakiwa kufika bungeni Oktoba 30 mwaka huu.

Wiki iliyopita DeFazio alimwomba Muilenburg kuwatayarisha wafanyakazi kadhaa wa kampuni hiyo kwa ajili ya kufanyiwa mahojiano kama sehemu ya uchunguzi wa bunge la Marekani kuhusiana na namna ndege hiyo ilivyotengenezwa, maendeleo pamoja na utendaji kazi wa ndege hiyo aina ya 737 MAX.

*DW*

**Mwenyekiti wa kamati hiyo ambaye ni mbunge, Peter DeFazio pia alimtaka John Hamilton Mkuu wa uhandisi katika kitengo cha biashara cha Boeing kufika bungeni kutoa ushahidi wake. Wawili hao wanatakiwa kufika bungeni Oktoba 30 mwaka huu.**



Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Félix Tshisekedi, atia saini kitabu cha dhahabu cha wageni wa heshima cha Mfalme wa Ubelgiji, Philippe, wakati wa ziara yake ya kiserikali. **PICHA: RFI**

# Ziara ya Tshisekedi Ubelgiji yazua gumzo

**BRUSSELS, Ubelgiji**

ZIARA ya kiserikali ya Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi nchini Ubelgiji imeendelea.

Lakini mapokezi ya Rais wa DRC kwa viongozi wa Brussels yameibua maswali mengi, ikiwa ndani na nje ya nchi.

Nchi hizo mbili zimesaini nakala kadhaa kuashiria kuanza tena kwa ushirikiano kabla ya Rais Tshisekedi kupokelewa na Mfalme wa Ubelgiji.

Lakini ziara hiyo yenye lengo la kufufua ushirikiano na kuboresha uhusiano kati ya DRC na Ubelgiji haikuwafurahisha wananchi wa DRC, baadhi wamekosoa na wengine wamekaribisha.

Baadhi ya wananchi wa DRC walijaribu kuandamana kabla ya Jeshi la Polisi Ubelgiji kuingilia kati na kuwatawanya, mbali na maeneo rasmi. Wanalaumu Ubelgiji kwa kumpokea Rais Tshisekedi wakati uchaguzi wake ulipingwa.

"Tuko hapa kuelezea kutoridhishwa kwetu kwa kukaribishwa Tshisekedi hapa Ubelgiji. Wakongo mnaowaona hapa hawamtambui Tshisekedi kama Rais wa DRC. Kwetu sisi, tunaona kuwa alifanya mapinduzi ya uchaguzi nchini DRC," mmoja kati ya waandamanaji amesema alipokuwa akihojiwa na waandishi wa habari.

Nchini DRC, wapinzani nao walionyesha kutoridhika na ziara hiyo ya Rais Tshisekedi nchini Ubelgiji.

Kwa upande wa Martin Fayulu, mgombea urais aliyeshindwa katika uchaguzi wa urais na ambaye anaendelea kupinga matokeo ya uchaguzi, alisema Ubelgiji imempokea mtu ambaye hana uhalali wa kisiasa.

"Baada ya taarifa zilizotolewa na wanasiasa wa Ubelgiji, nadhani ni ukosefu wa heshima kwa wananchi wa DRC. Wanampokea mtu anayepuuzia demokrasia? Tshisekedi hataweza kufanya chochote mwenyewe kwa sababu hana uwezo wa sera yake. Kabila bado yupo, anasubiri na anaongoza kila kitu," alisema Fayulu.

RFI

# Kozi kimataifa ya uratibu matukio yazinduliwa Dar

**Na Beatrice Moses**

UKUAJI wa sekta ya utalii duniani na nchini umechochea Chuo cha Taifa cha Utalii kuanzisha kozi mpya ya kimataifa ya uratibu wa matukio (Event Management).

Akizungumzia hatua hiyo jana kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa programu hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shongo Sedoyeka, alisema kozi hiyo inalenga kuwajengea uwezo na weledi waandaaji na waratibu wa matukio.

"Tunalenga kuwajengea uwezo ambao wamenza kujihusisha na kazi hii, lakini pia na wale wanaopenda kujiunga na fani hii nchini na kwenye mataifa mengine," Dk. Sedoyeka alisema.

Alisema hatua hiyo imefikiwa kutokana na ushirikiano kati ya chuo hicho na Chuo Kikuu cha Visiwa vya Vancouver cha Canada.

"Pia katika kuunga mkono juhudi za serikali za ukuaji wa viwanda katika kufikia uchumi wa kati," alisema.

Alibainisha kuwa wakala wa chuo hicho una jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika fani za utalii na ukarimu.

Dk. Sedoyeka alisema kozi hiyo itaanza kutolewa kuanzia mwaka wa masomo 2019/2020 katika chuo hicho kilichopo jijini Dar es Salaam.

Mdau wa tasnia ya uandaaji wa matukio, Antoni Luvanda, aliushukuru uongozi wa wakala wa kuamua kuanzisha kozi hiyo ambayo anaamini itawasaidia kuwajengea njia ya kupata fursa nzuri zaidi.

"Kuna mikutano mikubwa ya kimataifa ambayo imefanyika nchini kwa sababu ya kutokuwa na cheti hatupewi uzito, mfano ukifuatilia kwa karibu mkutano wa SADC waratibu asilimia kubwa walitoka nje ya nchi, binafsi nafarajia kujiunga," Luvanda alisema.

Alifafanua kuwa licha ya kuwa anatambulika na wengi kwa shughuli zake, lakini amekuwa akizifanya kutokana na kipaji hakuwahi kusomea mahali popote. Mkurugenzi wa Mafunzo wa Chuo hicho, Stephen Madenge, alisema kozi hiyo inatolewa kwa ngazi ya astashahada na shahada kwa miaka miwili.

"Hii kozi ni muhimu hakuna chuo rasmi kinachotoa au kilichowahi kufundisha, ni fani yenye soko, mhitimu anaweza kujiajiri au kuajiriwa ," Madenge alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiangali ujazo tofauti wa sukari unaofanywa na kiwanda cha sukari Kilombero alipokitembelea kuangalia mchakato wa upanuzi wa kiwanda hicho juzi. Wa kwanza kulia ni Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, akifuatiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Guy Williams na kulia kwa Waziri Mkuu ni Mkuu wa Uhusiano wa kampuni hiyo, Joseph Rugaimukamu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki Standard Chartered Tanzania yang'ara Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Standard Chartered Tanzania imetajwa kuwa benki bora Afrika na kupata tuzo ya kutoa huduma za kifedha kidijitali kwa wateja wake kwa mwaka 2019.

Kwa Afrika Benki hiyo imeshinda tuzo nane kati ya 10 zilizotolewa kwa mwaka 2019.

Tuzo hiyo inatokana na huduma bora zinazotolewa na benki hiyo ya 'Mobile Banking App'.

Taarifa iliyotolewa na benki hiyo kwa vyombo vya habari jana, ilisema kuwa benki hiyo imetajwa kwenye jarida linaloandika habari za taasisi za kifedha la journal, Global Finance.

Pamoja na tuzo hiyo, benki hiyo pia imetambuliwa kwa usalama wa taarifa na kudhibiti uhalifu wa kifedha kupitia mtandao wa kidijitali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Standard Chartered, Sanjay Rughani, alisema tuzo hiyo inaonyesha jinsi gani benki ilivyojihakikishia kuifanyia kazi ajenda ya kidijitali na inavyoongoza njia katika kutatua matatizo ya kidijitali yanayoendana na mipango ya nchi ya ajenda za kifedha.

"Huduma zetu ni kielelezo cha jinsi benki yetu inavyoendelea kuweka kwenye teknolojia na kumridhisha mteja wetu," alisema.

Alisema huduma za kidijitali zinaondoa utamaduni wa zamani na kuleta mabadiliko ya huduma za biashara za kibenki kwa lengo la kuboresha matakwa ya wateja.

Akizungumzia tuzo hiyo, Ofisa Mtendaji Mkuu kwa upande wa Afrika na Mashariki ya Kati wa benki hiyo, Sunil Kaushal, alisema hiyo ni ushuhuda kuwa mabadiliko ya kidijitali yanalipa.

Vigezo vya ushindi pamoja na mambo mengine vilizingatia uimara wa kuvutia huduma za kidigitali kwa wateja, mafanikio ya kuvutia wateja katika huduma za kidijitali, ukuaji wa wateja kidijitali na faida zilizopatikana kutokana na huduma hizo.

## RC Pwani afagilia mmiliki Global Packaging

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Everest Ndikilo, amemmwagia sifa mmiliki wa Kampuni ya Global Packaging na Wande Printing and Packaging Ltd, Joseph Wasonga, katika jitihada zake za kuchangia shughuli za maendeleo mkoani humo.

Akizungumza na wanahabari wakati wa makabidhiano ya mifuko 200 ya saruji kusaidia ujenzi wa ukumbi na ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani mjini Kibaha, Mhandisi Ndikilo alisema kuwa mwenyekiti wa kampuni hizo amekuwa mfano wa kuigwa katika kuchagiza maendeleo katika mkoa wake.

"Kwa kipekee kabisa napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kampuni ya Global na Wande Printing kwa namna anavyojitoa katika kutimiza malengo ya chama na serikali mkoani hapa, jambo ambalo linapaswa kuigwa na kila mwekezaji na wadau wote wa maendeleo," alisema Mhandisi Ndikilo.

Kuhusu mchango wa mifuko 200 ya saruji ambayo ilikabidhiwa kwa Ofisi ya CCM Mkoa wa Pwani, alisema ujenzi wa ukumbi na ofisi za mkoa utaongeza fursa katika Mkoa wa Pwani.

"Mchango huu kwa CCM Mkoa ukitumika vizuri na hatimaye kukamilika kwa ujenzi wa ukumbi na ofisi utachangia sana kuongeza fursa za ajira, kuongezeka kwa mapato na kuendelea kuimarika kwa CCM ndani ya Mkoa wa Pwani," alisema Mkuu wa Mkoa.

Aidha, Ndikilo alitoa wito kwa wadau wengine wa chama na serikali kuendelea kuchangia ujenzi wa ukumbi huo kwani bado upo katika hatua za awali.

"Nitoe wito kwa wadau wa chama kuendelea kuchangia ujenzi wa ofisi hizi kama ambavyo Katibu Mkuu wa CCM Taifa Bwana Bashiru Ally amekuwa akisisitiza kwamba watu wa chama waone fahari kuchangia maendeleo ya chama chetu, Bwana Wasonga kaanza na wengine tufuate," alisisitiza Mhandisi Ndikilo.

Mkurugenzi wa Global Packaging ambaye alikabidhi mifuko hiyo kwa niaba ya mwenyekiti wa kampuni hizo, Benno Mwitumba, alisifu Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani chini ya Mhandisi Ndikilo kwa namna ambavyo imekuwa ikitoa ushirikiano kwa wawekezaji na wadau wa maendeleo mkoani humo.

"Tunaishukuru ofisi ya mkoa kwa kutuunga mkono na kwa kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji hali ambayo imeturahisishia sana katika kuendesha shughuli za uwekezaji katika viwanda na maeneo mengine ya kijamii," alisema Mwitumba.

Mwitumba alisema watajitahidi kuongeza ushawishi wao kwa kampuni na mashirika mbalimbali ya maendeleo ili kufanikisha ujenzi wa ukumbi kwa wakati.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.



NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI




**Selina Peter Galleti** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma ya Ualimu daraja la IIIA chenye index namba NSO361/0038/1982 kilichotolewa na chuo cha Kisanga mwaka 2017.

Yeyote atakaekiona cheti hiki atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/057672/2016**

215305002

## KUPOTEA KWA VYETI




**Selina Peter** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.361/38 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1982 katika shule ya Sekondari Singe na cheti cha Ualimu Daraja la III chenye index namba E.522/37 kilichotolewa na Chuo cha Kinampanda mwaka 1985.

Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/057672/2016**

115305002

## KUPOTEA KWA CHETI



ABDULHAMID SHEIKH KAISARY anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0671/0078 kilichotolewa na UBUNGO ISLAMIC HIGH SCHOOL mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: MBL/RB/11751/2019.

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**ZUWENA PETER MKOMBOZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili T661CLK, Chassis Na.**LH1231014773,** Engine Na. **3LFEIN5.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/310156/2019.**

115424802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AZIZ HILAL HUSSEIN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina TOYOTA SIENTA yenye namba za usajili T 849 DDH. Chassis No.NCP810086643, Engine No.1NZB520617.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: KON/ RB/1750/2019.

215424602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;186/2019

Ombi la **BONIFACE F.KIWALE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **CHÀRLES MICHAEL MDETE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/09/2019.

115424502


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie*

*0767 223 311*

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# FABIAN AGOMBEWA MADRID, BARCA

**MADRID,** Hispania

GAZETI la Daily Mail limeripoti kwamba, klabu za Real Madrid na Barcelona zipo kwenye mbio moja za kuwania saini ya nyota wa Napoli, Fabian.

Fabian amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa viungo bora Ulaya na miamba hao wa Hispania sasa wanapigania kuipata saini yake.

Wapinzani hao wa La Liga wote wameonyesha nia ya wazi kabisa ya kutaka kumsajili Fabian.

Fabian aliondoka Real Betis na kutua Napoli mwaka 2018 na mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania haraka ameonekana kuwa na kiwango cha juu zaidi.

Hata hivyo, klabu yake ya Napoli imebainisha wazi kwamba, hawana mpango wowote wa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kwani timu hiyo ina mipango naye ya muda mrefu.

# Sylvinho: Lyon imeanza vibaya Mabingwa Ulaya

**LYON,** Ufaransa

KOCHA wa Lyon, Sylvinho aliachwa amepagawa baada ya timu yake kuanza kwa sare ya kufungana bao 1-1 na Zenit kwenye mchezo wa kwanza wa makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Kocha huyo alisema kwamba, timu yake ilionekana kumpa 'stresi' mapema tu tangu mwanzo wa mchezo huo.

Zenit walianza kwa kufunga bao kabla ya kipindi cha pili, wakati Sardar Azmoun alipowatoa mabeki eneo la penalti na kupiga shuti lililojaa wavuni.

Lyon walisawazisha goli hilo mara tu baada ya kuanza kwa kipindi cha pili shukrani kwa Memphis Depay ambaye alifunga kwa penalti.

Lakini pia Depay aliikosesha bao Lyon wakati aliposhindwa kutumia nafasi aliyoipata kufunga akiwa peke yake na goli kwenye mchezo huo wa Kundi G.

Sylvinho ambaye alikuwa anaiongoza timu hiyo kwa mara ya kwanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya anaamini kwamba, Lyon walikuwa na nafasi ya kushinda mchezo huo.

"Tulianza vibaya, pengine kwa sababu wachezaji walionekana kama 'wanastresi'," alisema kocha huyo raia wa Brazil akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulikuwa na nafasi nzuri kwa pamoja na tungetulia tungeweza kupata mabao zaidi, lakini wachezaji hawakuonekana kuwa kwenye kiwango chao."



# *Sancho: Kuondoka? Nitabaki Dortmund*

**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho amesema kwamba, hajui majaliwa yake yako wapi, lakini nyota huyo wa Borussia Dortmund amesema anataka kushinda mataji na miamba hao wa Ujerumani licha ya kuhusishwa na mpango wa kutakiwa kule Manchester United.

Sancho ameripotiwa kwamba yupo kwenye rada za United kwa ajili ya kumsajili na kutua pale kwenye Uwanja wa Old Trafford.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 19, alionyesha kiwango cha juu wakati Dortmund ikitoka sare ya bila kufungana na Barcelona kwenye mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Alipoulizwa baada ya mchezo huo kuhusu majaliwa yake, Sancho aliiambia Viasport: "Siwezi kuzungumza kuhusu majaliwa yangu ya baadaye. Nataka tu kucheza mpira. Nataka kujitoa kwa asilimia 100 hapa Borussia Dortmund.

"Nataka kufanya vizuri zaidi nikiwa na Dortmund. Kwa uhakika kabisa nataka kushinda mataji na kila kitu."

Sancho amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji makinda wenye kipaji cha hali ya juu baada ya kuondoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City mwaka 2017.

Alifunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 14 wakati Dortmund ilipomaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, nyuma ya Bayern Munich msimu uliopita, huku tayari Sancho akiwa na mabao mawili na pasi za mwisho nne msimu huu.



# Barkley mpiga penalti Chelsea - Lampard

**LIVERPOOPL,** England

FRANK Lampard amethibitisha kwamba, Ross Barkley ndiye ameteuliwa kuwa mpigaji penalti wa Chelsea baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kukosa wakati wakifungwa bao 1-0 na Valencia kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, juzi Jumanne.

Lampard akiiongoza kwa mara ya kwanza Chelsea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, alipoteza mchezo huo kwa bao la Rodrigo Moreno la kipindi cha pili na kumfanya kocha Ibert Celades kupata ushindi wake wa kwanza kwa Valencia.

Chelsea walipewa penalti kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge baada ya mwamuzi, Cuneyt Cakir kutumia VAR kuthibitisha kama Daniel Wass aliushika kwa mkopo mpira wa kichwa uliopigwa na Fikayo Tomori.

Barkley akitokea benchi alipewa nafasi ya kupiga penalti hiyo baada ya kutokea majadiliano kati yake na Willian na Jorginho, lakini shuti lake likagonga mwamba wa juu.

Lakini Lampard alithibitisha mara baada ya mchezo huo, kuwa Barkley ataendelea kuwa chaguo la kwanza kwa kupiga penalti za Chelsea kama ambavyo alipewa nafasi hiyo wakati klabu hiyo ikiwa kwenye maandalizi ya msimu mpya.

"Ross ndiye mpiga penalti wetu. Alifunga penalti nyingi wakati wa maandalizi ya msimu mpya wa ligi na alipewa yeye alipoingia uwanjani," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari.

"Ataendelea kupiga penalti, kwani alikuwa akipiga tangu mwanzo, lakini leo (juzi) alikosa. Sioni tatizo ataendelea kupiga penalti za Chelsea.

"Sijui majadiliano kati yao (Jorginho na Willian) yalitoka wapi, kwani wanajua kwamba, Ross ndiye mpiga penalti wetu na alikosa."







# MESSI KAFANYA YA KUTOSHA - VALVERDE

**DORTMUND,** Ujerumani

LIONEL Messi "alifanya yakutosha" aliporudi dimbani wakati Barcelona ikitoka sare ya bila kufungana na Borussia Dortmund kweye mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya juzi Jumanne, amesisitiza kocha Ernesto Valverde.

Messi alicheza mechi yake ya kwanza msimu huu baada ya kupona kigimbi cha mguu wakati Barca ikilazimishwa sare na Dortmund ugenini kwenye mchezo huo wa Kundi F.

Nahodha huyo wa Barca alikaa benchi hadi kipindi cha pili kwenye mchezo huo, na alipoingia alionekana kucheza vizuri.

"Yeye ni kama mchezaji yeyote ambaye hajacheza wakati wa maandalizi ya msimu mpya," alisema Valverde.

"Alicheza kwa kiwango cha kuvutia na kasi, ambapo hakuwa na maandalizi ya kutosha.

"Ni dakika zake 30 za kwanza. Alifanya ya kutosha. Pia ulikuwa mchezo wa kwanza kwa Luis Suarez kucheza kwa dakika zote."

Barca itamshukuru golikipa wake, Marc-Andre ter Stegen ambaye aliokoa penalti ya Marco Reus katika kipindi cha pili.

# *Klopp: Napoli inaweza kubeba ubingwa Ulaya*

**NAPLES,** Italia

JURGEN Klopp amesema kwamba Napoli inaweza kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku kocha huyo wa Liverpool alikisifia kikosi chake kilicheza vizuri licha ya kufungwa.

Liverpool mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya walifungwa mabao 2-0 na Napoli kwenye mchezo wa kwanza wa Kundi E, juzi Jumanne.

Dries Mertens alifunga penalti dakika ya 82 baada ya Jose Callejon kudondoshwa na Andy Robertson kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa San Paolo, ambapo VAR ndio ilitumika kuamua penalti hiyo, na Fernando Llorente akafunga la pili.

Kocha wa Liverpool, Klopp, ambaye msimu uliopita walifungwa bao 1-0 na Napoli kwenye hatua ya makundi, alionekana kutoridhishwa na maamuzi ya penalti na wakati alipoulizwa kuhusu nafasi ya kikosi hicho cha Carlo Ancelotti kwenye michuano hiyo, alisema: "Wanaweza kushinda mashindano, hivyo ndivyo ilivyo.

"Kama una mipango na mabao, kama ukiwa na wachezaji wazuri, ambapo wao walikuwa nao, wanaweza kushinda mashindano.

"Kwenye mashindano haya unatakiwa kuwa na bahati pia, lakini wao walikuwa na kikosi kizuri na wana nafasi nzuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ndio, wanaweza kushinda bila shaka yoyote."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GRIEZMANN: NAHITAJI MUDA KUNOGA NA MESSI, SUAREZ

## ●●● Huu ni mwezi wangu wa pili tangu nitue hapa, napaswa kuendelea kutumika, kucheza...

**DORTMUND,** Ujerumani

ANTOINE Griezmann amesisitiza kuwa itachukua muda kwake kuweza kuzoeana na kufanya kazi vizuri na Lionel Messi na Luis Suarez, kauli hiyo akiitoa baada ya Barcelona kuondoka na pointi moja dhidi ya Borussia Dortmund kwenye mechi yao ya ufunguzi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

**Barcelona iliambualia sare tasa ugenini dhidi ya miamba hiyo ya Bundesliga, Dortmund katika mechi ya Kundi F baada ya kipa Marc-Andre ter Stegen kuokoa penalti ya Marco Reus.**

Nyota wa Barca, Messi alicheza mechi yake ya kwanza msimu huu baada ya kupona majeraha ya kigimbi cha mguu, akiingia akitokea benchi kipindi cha pili lakini ulikuwa usiku wa kuchanganya kwa mabingwa hao wa La Liga, ambao kikosi chao kilimjumuisha Suarez na usajili mpya wa majira ya joto, Griezmann.

"Huu ni mwezi wangu wa pili tangu nitue hapa, ninapaswa kuendelea kutumika na kucheza zaidi nao kuweza kuelewa namna wanavyocheza Suarez na Leo," Griezmann, ambaye alisajiliwa kwa euro milioni 120 akitokea Atletico Madrid alikiri kupitia Movistar +.

"Hatujagonga mlango vyakutosha na lazima tujizatiti na kufanyia kazi hilo. Ni pointi lakini Marc alizuia penalti na kuokoa michomo mingine."

Kocha Mkuu wa Barca, Valverde alifunguka, wanapaswa kumshukuru Ter Stegen kwa kuokoa vizuri ikiwa ni pamoja na kuucheza mkwaju wa Mjerumani mwenzake, Reus katika dakika ya 57.

"Ilikuwa ni mechi ngumu katika hamasa kubwa ya mashabiki," Valverde alisema. "Tulilazimika kuhaha sana, zaidi baada ya mapumziko wakati tulipopoteza udhibiti na walikuwa hatari sana.

"Katika kipindi cha kwanza tulitawala zaidi kidogo. Tulikuwa tunakosa theluthi ya mwisho. Tunapaswa kumshukuru Marc-Andre ter Stegen kwa kiwango chake cha kuokoa.

"Tunajua tunapaswa kujizatiti ugenini. Tulijaribu kumpa dakika chache Messi na Luis Suarez alicheza tangu mwanzo."

Ter Stegen aliongeza: "Watu wanajua kile ninachoweza. Ninachotaka tu ni kuzingatia zaidi katika kazi na kiwango kwa asilimia 100 ya uwezo wangu. Leo nadhani nimeonyesha hilo."

Nahodha wa Dortmund, Reus alikiri kuchanganyikiwa kwake kufuatia kukosa nafasi kama hiyo ya kipekee ya kuwafunga miamba hiyo ya Hispania. Alisema: "Marc ni kipa wa daraja la juu duniani. Penalti yangu sikupiga vizuri. Nitarudi katika uwanja wa mazoezi kwa hilo."

## ZISIKUPITE

### WILSON AANDALIWA OFA UTD

MANCHESTER United inajiandaa kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Bournemouth, Muingereza Callum Wilson, 27, ambaye amefunga mabao mawili katika mechi zake mbili zilizopita. ***(Sun)***

### RUIZ AVUTIA VIGOGO ULAYA

REAL Madrid, Barcelona na Liverpool zinaitaka saini ya kiungo wa Napoli, Mhispania Fabian Ruiz, 23. ***(Mail)***

### SANCHO AULIZIWA UNITED

MANCHESTER United iliulizia kuhusu uwezekano wa kumpata winga wa Borussia Dortmund, Muingereza Jadon Sancho, 19. ***(Viasport Football - via Manchester Evening News)***

### FATI ANUKIA MITANO BARCA

WINGA wa Barcelona, mzaliwa wa Guinea-Bissau, Ansu Fati, 16, yupo mbioni kukubali mkataba mpya wa miaka mitano na klabu hiyo baada ya kufumania nyavu mara mbili kwenye mechi tatu za La Liga alizocheza. ***(AS - in Spanish)***

### COUTINHO ANOGEWA BAYERN

KIUNGO Mbrazil Philippe Coutinho, 27, amesema Bayern Munich ambayo anaichezea kwa mkopo akitokea Barcelona ni "zaidi ya familia" kuliko Barca na klabu yake ya zamani ya Liverpool. ***(Liverpool Echo)***

### ROONEY AFUNGUKA MALIPO MLS

MSHAMBULIAJI wa DC United na aliyewahi kuichezea Manchester United na England, Wayne Rooney, 33, amesema wachezaji wa Ligi Kuu Marekani (MLS) wanapaswa kulipwa zaidi. (ESPN)

### ISCO SASA AWINDWA JUVE

NYOTA wa Real Madrid na Hispania, Isco, 27, ambaye aliivutia Manchester City na Liverpool, anatakiwa na Juventus, ambayo inaandaa pauni milioni 66 kwa ajili ya kutoa ofa kwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Malaga. ***(Sun)***

### STERLING KUMRITHI MESSI, CR7

WINGA wa Manchester City, Raheem Sterling, 24, "anashinda mbio" za kumrithi mshambuliaji wa Barcelona Lionel Messi, 32, na straika wa Juventus, Cristiano Ronaldo, 34, kama mchezaji bora duniani, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa kimataifa, Xavi. ***(Mirror)***

### LARSSON AMULIKWA SOUTHEND

KLABU ya Southend United inayohaha kwenye League One, inamtaka mshambuliaji wa zamani wa Sweden, Celtic, Barcelona na Manchester United, Henrik Larsson kuwa kocha wao mpya. ***(Mail)***

### LLORIS AIFIKIRIA SPURS, MLS

KIPA wa Tottenham na Ufaransa, Hugo Lloris, 32, amesema kuna uwezekano kumalizia soka lake klabuni hapo na anavutiwa kwenda kucheza soka Ligi Kuu Marekani (MLS), kabla ya kutundika daluga. ***(France Football - in French)***

### UBAHILI WAMGHARIMU PEP

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amekosa wachezaji aliokuwa akiwawinda kwa sababu alikataa kulipa dau kubwa. ***(Guardian)***

HABARI MICHEZO

# KATWILA ATAMBA BARA KUBEBA U-20 CECAFA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 20, Zuberi Katwila, amesema wachezaji wake wameimarika na wako tayari kutwaa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati ambayo yanatarajiwa kuanza keshokutwa, Jumamosi nchini Uganda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila, alisema wachezaji wake wameimarika na kila mmoja amejipanga kwenda kupeperusha vema bendera ya Tanzania Bara katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Katwila alisema mechi za kirafiki ambazo wamecheza zimewaimarisha na wanaamini watatimiza malengo yao.

"Morali iko juu, wanajua Watanzania wanataka nini, wamedhamiria kuweka heshima na kuweka rekodi, wanajua wanapokuwa kwenye timu ya Taifa wanatakiwa wafanye nini, malengo ni kurudi na kikombe," alisema Katwila.

Kocha huyo aliongeza kuwa hana majeruhi katika kikosi chake na ushindani wa namba ni mkubwa, kutokana na kila mchezaji kuonyesha uwezo mzuri kuanzia kwenye mazoezi hadi katika mechi za kirafiki ambazo wamecheza.

Naye nahodha wa timu hiyo, Dickson Job, alisema kuwa kila mchezaji amejipanga kufanya vizuri katika mashindano hayo na hawana wasiwasi wa aina yoyote.

"Kundi letu liko kawaida kutokana na tulivyojiandaa, tunaamini tutafanya vizuri na kuvuka hatua ya makundi, tunachosubiri ni michuano ianze," alisema nahodha huyo.

Tanzania Bara itakayokuwa kwenye kituo cha Jinja, imepangwa katika Kundi B ikiwa pamoja na Kenya, Ethiopia na "ndugu" zao, Zanzibar.

Wenyeji Uganda wanatarajia kufungua mashindano hayo kwa kuwakaribisha yosso wenzao kutoka Eritrea kwenye Uwanja wa Gulu wakati Tanzania Bara wataanza kampeni ya kuwania ubingwa huo Jumapili



Mshambuliaji wa Liverpool, Mmisri Mohamed Salah akidhibitiwa na beki wa Napoli, Msenegal Kalidou Koulibaly, katika mchezo wa Kundi E wa Ligi ya Mabingwa Ulaya uliopigwa Uwanja wa San Paolo mjini Napoli juzi na wenyeji kushinda 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Wasanii nchini kuandaa katiba

**Na Philip Nyiti, Tudarco**

SHIRIKISHO la Filamu Tanzania (TAFF), kwa kushirikiana na Bodi ya Filamu nchini wanatarajia kutambulisha rasmi mchakato wa rasimu mpya ya katiba ya filamu kwa wasanii na wadau wanaofanya kazi kwenye tasnia hiyo, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Rais wa TAFF, Simon Mwakifamba, alisema baada ya kuitambulisha rasimu hiyo mpya, mchakato utakaofuata ni ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa sanaa hiyo ya filamu.

Mwakifamba alisema wanatarajia kupokea maoni kwa njia mbalimbali ikiwamo mitandao ya kijamii ya Facebook, magazeti, blogs na kuongeza kuwa mchakato huo utachukua muda wa mwezi mmoja.

"Tunatoa wito kwa wadau wote wenye nia njema kutoa mawazo yao ambayo yataleta tija kwenye tasnia hii ili kuujenga umoja wa tasnia na kuukuza mchango kiuchumi, kwenda katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025," alisema Mwakifamba.

Naye Kaimu Katibu wa bodi ya filamu, Kiago Kilonzo, alisema serikali imetoa baraka kuanza kwa mchakato huo na rasimu hiyo itakapokamilika itaweza kuwatetea wasanii wa tasnia hiyo ambao watafanya kazi zao kwa kufuata sheria.

# Klabu zabanwa usajili Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limewataka viongozi wa timu mbalimbali visiwani hapa kuacha tabia ya kuandika taarifa zisizo sahihi za wachezaji wao wakati wanapofanya mchakato wa kuwahamisha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa Mashindano wa ZFF, Ali Mohammed, alisema tabia hiyo itawaweka viongozi wahusika katika matatizo pale itakapobainika wametenda kosa hilo.

Mohammed alisema tabia hiyo inakwamisha wachezaji kuanza kutumikia klabu mpya kutokana na kuwapo kwa pingamizi au kutokamilika mapema kwa usajili wa nyota wanaotakiwa kuhama kwa wakati.

"Udanganyifu huo unachangia kukwamisha usajili wa wachezaji wengi, usajili na uhamisho wao kutokuwa halali, wanasababisha hata kuleta usumbufu katika mchakato wa kupitisha fomu za usajili wao kwenye timu walizohamia," alisema kiongozi huyo.

Alisema timu nyingi zimekuwa zikikiuka taratibu za usajili na kutaja sababu mojawapo inayowakwamisha ni kuanza kufanya mazungumzo na mchezaji badala ya klabu yake anayoitumikia.

"Malalamiko hayo ni mengi, hususan kutoka katika timu ndogo, klabu za Ligi Kuu zimekuwa zikichukua wachezaji kutoka katika madaraja ya chini bila kuwapo kwa makubaliano na uongozi husika, badala yake makubaliano yanafanywa baina ya mchezaji na timu anayokwenda, hii si sahihi," Mohammed alisema.

Hata hivyo, alisema ZFF kupitia kamati yake ya mashindano imejipanga kuhakikisha inasimamia kanuni na wachezaji wote wenye mkataba watahamishwa kihalali kwa mujibu wa kanuni za mashindano zinavyoelekeza.

# TWIGA STARS WAILILIA SERIKALI

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), kimeomba serikali na wadau mbalimbali kuongeza nguvu katika kuwekeza kwenye soka la wanawake ili nchi iweze kupata mafanikio zaidi, imeelezwa.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa TWFA, Amina Karuma, katika hafla ya kuwapongeza wachezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana ya wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), ambao walitwaa ubingwa wa mashindano ya COSAFA mwezi uliopita.

Karuma alisema timu za wanawake zimekuwa zikifanya vema katika mashindano mbalimbali, lakini wanaamini wakiendelea kupewa nguvu, watafika mbali.


"Kama serikali na wadau, wakiwekeza japo robo ya nguvu wanayotumia kwa wanaume, nina hakika tutacheza Kombe la Dunia la Wanawake," alisema Karuma.

Kwa sasa kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kinajiandaa kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika Novemba mwaka huu hapa nchini.

Michezo

Alhamisi Septemba 19, 2019

Nipashe



Griezmann: Nahitaji muda kunoga na Messi, Suarez HABARI UK 30

MSHIKEMSHIKE...



Mshambuliaji wa KRC Genk, Mtanzania Mbwana Samatta, katika harakati za kuwania kumiliki mpira dhidi ya beki Red Bull Salzburg, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi iliyopigwa Uwanja wa Red Bull Arena mjini Wals-Siezenheim, Austria na wenyeji kushinda 6-2. **PICHA: MTANDAO**

# SAMATTA AANDIKA REKODI KALI ULAYA

●●● KRC Genk pia yaruhusu rekodi ya hat-trick ya Raul, Rooney kufikiwa wakati ikitobolewa mabao 6-2, lakini...

**Wals-Siezenheim, Austria**

STRAIKA wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa ya Stars, Mbwana Samatta ameweka rekodi mbili kwa mpigo, kwa kuwa Mtanzania wa kwanza kucheza na kufunga kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini akishuhudia pia timu yake ya KRC Genk ikichapwa mabao 6-2 na wenyeji wao, Red Bull Salzburg ya Austria.

Kwa rekodi hiyo Samatta ambaye alirejea uwanjani baada ya kukosekana kwenye mchezo wa Ligi ya Ubelgiji Ijumaa iliyopita kufuatia kuumia akiichezea Taifa Stars, sasa amempiku Kassim Manara aliyekuwa akishikilia rekodi ya muda mrefu ya kuwa Mtanzania pekee aliyecheza michuano ya klabu barani Ulaya, iliyokuwa ikijulikana kama Kombe la Washindi akiwa na klabu ya SK Austria Klagenfurt, michuano ambayo sasa inajulikana kama Europa League.

Katika mechi hiyo ya Kundi E, linalozijumuisha pia mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Liverpool ya England na Napoli ya Italia, iliyopigwa kwenye Uwanja wa Red Bull Arena mjini Wals-Siezenheim, Samatta alifunga bao hilo dakika ya 52 kwa kichwa ikiwa ni baada ya lile la kwanza la Jhon Lucumi la dakika ya 40.

Mbali na rekodi hiyo ya Samatta, lakini pia mechi hiyo iliandika rekodi kibao ambapo kinda wa Salzburg, Erling Haaland alijitangaza mwenyewe kuwa mchezaji wa kwanza katika michuano hiyo hatua ya makundi msimu huu kuweza kutupia hat-trick.

Aidha, Salzburg imefunga mabao mengi katika dakika 45 za kwanza (mabao matano) kuliko ilivyofanya msimu wa 1994-95 (mabao manne katika mechi sita).

Kwa ujumla Genk (imecheza mechi 13, haijashinda na kupoteza sita), sasa imecheza mechi nyingi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya bila kuibuka na ushindi kuliko timu yoyote ile kwenye historia ya michuano hiyo.

Hata hivyo, mabao nane yaliyofungwa katika mechi hiyo kati ya Salzburg na Genk kwa ujumla ndiyo idadi kubwa katika siku moja ya kwanza ya michuano hiyo, idadi nyingine ikiwa ni mechi kati ya Hamburg na Juventus msimu wa 2000-01 iliyomalizika kwa mabao 4-4 na Olympiacos dhidi ya Bayer Leverkusen msimu wa 2002-03 ikimalizika kwa mabao 6-2.

Haaland akiwa na umri wa miaka 19 na siku 58 - ni mchezaji wa tatu kinda zaidi kuweza kufunga hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa nyuma ya Raul (miaka 18 na siku 113, akifanya hivyo mwaka 1995) na Wayne Rooney (miaka 18 na siku 340, mwaka 2004).

Samatta na Genk yake sasa wanasubiri kuwakaribisha wababe wa Liverpool, Napoli hapo Oktoba 2, mwaka huu wakati Salzburg ikitarajia kuwafuata mabingwa hao watetezi katika Uwanja wa Anfield siku hiyo.

Licha ya ushindi huo wa kishindo wa Salzburg, bado ina kazi ngumu kuhakikisha inafuzu hatua ya 16-bora na mtihani wa kwanza itapaswa kuuthibitisha itakapokutana na Liverpool ambayo imetoka kuchezea kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Napoli.

Mabao mengi ya Salzburg katika mechi hiyo yalifungwa na Hwang Hee-chan, Dominik Szoboszlai na Andreas Ulmer.

## Kuiona Yanga Zambia nauli hii

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa Yanga umesema mchezo wao wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco ya Zambia utakuwa ni "wa kawaida" na wanaamini wana nafasi kubwa ya kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa, huku wakitangaza gharama ya kwenda na kurudi Ndola, Zambia kwa mashabiki wanaovutiwa kwenda kuisapoti kuwa ni Sh. 150,000 kwa ajili ya usafiri tu.

Zesco ambayo ililazimisha sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Taifa, itawakaribisha wawakilishi hao wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano hayo, Yanga ifikapo Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema kikosi chao kinaendelea kuimarika na uongozi wa klabu hiyo kwa kushirikiana na benchi la ufundi, wamejipanga kufanya maandalizi bora ili kuhakikisha wanashinda mchezo huo na kusonga mbele.

"Tumepanga kuwaandaa wachezaji kimwili na kisaikolojia ili wafanye vizuri katika mechi inayotukabili, pia tunapenda kuwaambia watu, mashabiki wa Yanga na Watanzania kuwa mechi hii ni ya kawaida, mapungufu ambayo mwalimu aliyaona, ameahidi atayafanyia kazi na anatarajia kuwa na kikosi imara zaidi katika mchezo huo," alisema Mwakalebela.

Kiongozi huyo alisema kuwa kwa sasa kikosi cha Yanga kimekamilika baada ya wachezaji waliokosekana katika mchezo uliopita kutokana na sababu mbalimbali kurejea katika timu hiyo. Alisema pia tayari wameshaandaa ujumbe utakaotangulia Zambia ili kuandaa mazingira bora na kikosi chao kitaondoka nchini Jumatatu ili kwenda Ndola kukamilisha kazi waliyoianza hapa jijini.

Wakati huo huo, Kamati ya Hamasa ya Yanga inawashukuru mashabiki wa timu hiyo na wadau wote waliojitokeza kuishangilia timu yao katika mchezo wao uliopita dhidi ya Zesco ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1. Katibu wa kamati hiyo, Deo Mutta, alisema kuwa mashabiki wanaotaka kwenda Zambia kuishangilia timu yao wanatakiwa kulipa kiasi cha Sh. 150,000 kwa ajili ya gharama ya usafiri wa kwenda Ndola na kurudi nchini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >